**MADA**

# MAUDHUI NA MTINDO KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*


**NA**

**ZIPPORAH M. KITIKU**

**C50/83426/2015**



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA


**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**


**IDARA YA KISWAHILI**



*1702329*
UoN Thesis
2017


**2017**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwa ufahamu wangu haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

______________________ 21/11/2017.

**ZIPPORAH M. KITIKU** TAREHE

(MWANAFUNZI)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 21ST NOV 2017

**PROF. RAYYA TIMAMMY** TAREHE

(MSIMAMIZI)

______________________ 21/11/2017

**DR. SWALEH AMIRI** TAREHE

(MSIMAMIZI)

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia marehemu wazazi wangu wapendwa, Bw. Jonathan Kitiku na Bi. Esther Kitiku kwa kujinyima anasa zote ili kunilea na kunipa msingi bora maishani. Aidha, nawatabarukia mume wangu mpenzi Bwana Joseph Ndutu, mwanangu Hope Neema na dadangu mpendwa, Bi. Agnes Nzei ambaye alijitwika jukuma la kunielimisha tangu utotoni hadi nikaweza kujisimamia. Mungu awabariki nyote.

## SHUKRANI

Hakuna binadamu aliyejitosheleza. Kila binadamu huhitaji msaada wa wenzake ili afanikiwe katika jambo fulani. Kazi hii isingefaulu wala kukamilika kama ningelijitwika jukumu la kuifanya peke yangu bila msaada wowote. Isingekuwa ni kwa usaidizi wa watu wengi nitakaowataja kwa majina na wengine ambao sitawataja, nisingeikamilisha kazi hii kwa wakati.

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kunipa fursa ya kutimiza ndoto yangu. Kwa neema zake, nimefika nilipo sasa. Pili, natoa shukrani za dhati kwa mume wangu Bwana Joseph Ndutu aliyesimama nami, akanishauri na kunitia moyo kila wakati hasa mambo yaliponiwia magumu. Ulinifaa kwa hali na mali, Mungu akulinde. Shukrani zaidi zimwendee binti yangu Hope Neema ambaye licha ya kuwa mdogo wa umri, amenivumilia na kunielewa wakati wote ambapo sikuwa naye aliponihitaji. Aidha, shukrani zaidi nazitoa kwa Tume ya Kuwaajiri Walimu kwa kunipa likizo ya kurudi chuoni ili niendelee na masomo.

Shukrani za dhati pia nazitoa kwa wasimamizi wangu Profesa Rayya Timammy na Daktari Amiri Swaleh kwa kunisimamia, kuisoma kazi yangu, kunielekeza na kunishauri kwa moyo mkunjufu. Asanteni sana na Mungu awabariki.

Nawapa shukrani zangu wahadhiri wa Idara ya Kiswahili katika Chuo kikuu cha Nairobi kwa mchango wao wa moja kwa moja ambao umeacha athari kubwa katika maisha na masomo yangu. Hawa ni pamoja na Profesa Mohamed Abdulaziz, Profesa Rayya Timammy, Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa John Habwe, Daktari Alfred Buregeya wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, Daktari Tom Olali, Profesa Mbatiah, Daktari Zaja Omboga, Bw. Mungania, Daktari Ayubu Mukhwana, Daktari Hannah Mwaliwa na Daktari Evans Mbuthia, wote wa Idara ya Kiswahili. Asanteni sana.

Nawashukuru wazamili wenzangu niliosoma nao kwa kila aina ya msaada na wema wenu wa kila wakati. Hawa ni pamoja na Ngulamu Mwaviro, Albert Otwera, Edwin Muna (Pastor), Ngunyi Samuel, Purity Kolongei, Lilian Chacha na mwakilishi wetu wa darasa, Joshua Anusu.  Asanteni kwa kuwa marafiki, nashukuru kukutana nanyi na Mungu awabariki.

# IKISIRI

Utafiti huu umehusu maudhui na mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* wa Haji Chum (1959). Tumechunguza maudhui mbalimbali yanayojitokeza kwenye utenzi huu. Tumeshughulikia vipengele mbalimbali vya kimtindo vikiwemo wahusika, dayolojia, tamathali za semi na kunga nyinginezo. Tamathali za semi tulizozishughulikia ni pamoja na sitiari, tashbihi, chuku, uhuishaji, maswali ya balagha na tabaini. Kunga nyingine tulizozishughulikia ni urudiaji, takriri, misemo na ukiushi wa kisintaksia. Tumeongozwa na nadharia mbili: nadharia ya Umuundo na ile ya Uhalisia. Tumeongozwa na malengo matatu ya utafiti: kwanza, tumechunguza maudhui yanayojitokeza kwenye utenzi, pili, tumeeleza jinsi wahusika wanavyoendeleza maudhui hayo na tatu, tumechunguza jinsi baadhi ya vipengele vingine vya kimtindo vinavyoendeleza maudhui. Tumebaini kuwa maudhui ya dini, ushujaa, vita na mauaji yamejitokeza katika utenzi. Pia, mtunzi amefanikiwa kuwatumia wahusika kuendeleza maudhui haya na mwisho, mbinu nyinginezo za kimtindo alizotumia mtunzi ni pamoja na taswira, dayolojia na tamathali za usemi ambazo kwa pamoja zimefanikisha kuchimuza maudhui. Hatimaye, tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

YALIYOMO

**IKIRARI** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKRANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ v

**SURA YA KWANZA** ........ 1

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........ 5

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........ 6

1.3 Sababu za Kuchagua Mada ........ 6

1.4 Upeo na Mipaka ........ 7

1.5 Nadharia Tete ........ 8

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 8

1.7 Msingi wa Kinadharia ........ 11

1.7.1 Nadharia ya Umuundo ........ 12

1.7.2 Nadharia ya Uhalisia ........ 14

1.8 Njia za Utafiti ........ 17

**SURA YA PILI: UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*** ........ 18

2.0 Utangulizi ........ 18

2.1 Dhana ya Maudhui ........ 18

2.2 Maudhui ya Ushujaa ........ 19

2.3 Sifa za Mtume Muhammad kama Shujaa ........ 21

2.3.1 Shujaa huwa na Majina au Sifa Nzuri ........ 21

2.3.2 Shujaa Anapendwa Sana na Wanajamii ........ 22

2.3.3 Shujaa Aghalabu huwa Mwanamume ........ 22

2.3.4 Shujaa huwa na Maadui/Wapinzani Wengi ........ 23

2.3.5 Kusalitiwa kwa Shujaa ........ 24

2.3.6 Shujaa ana Uwezo wa Kung'amua au Kutabiri ........ 25

2.3.7 Shujaa huwa Gwiji Vitani ........ 26

2.3.8 Maisha ya Shujaa na Matendo yake huwa ya Kimiujiza ........ 27

2.3.9 Maisha ya Shujaa ni ya Dhiki Tupu ........ 28

2.3.10 Shujaa huwa na Wafuasi ........ 28

2.3.11 Shujaa Huhusishwa na Zaidi ya Jamii Yake ........ 29

2.3.12 Mapenzi ya Mama kwa Shujaa....29
2.3.13 Shujaa huwa Mpole na Msamehevu....30
2.3.14 Shujaa Hutokana na Jamii Bora au ya Kifalme....30
2.3.15 Kugura/Kuhama kwa Shujaa....31
2.3.16 Utabiri na Miujiza Kabla na Baada ya Kuzaliwa....32
2.3.17 Mama wa Shujaa Aghalabu huwa Mnyonge au Maskini na Baba Huwa Hajulikani....33
2.3.18 Maisha ya Ujana wa Shujaa Hayajulikani kwa Uwazi....33
2.3.19 Shujaa na Swala la Ndoa....34
2.3.20 Kifo cha Shujaa....35
2.4 Maudhui ya Dini Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*....36
2.4.1 Kutanguliza kwa Maombi/ Kumtambua Mungu....36
2.4.2 Mtume Muhammad....37
2.4.3 Vita Vitakatifu....38
2.4.4 Bendera ya Uislamu....38
2.4.5 Kusilimu kwa Makureshi....39
2.4.6 Kupigana Vita Siku ya Ijumaa....39
2.4.7 Maombi Kabla ya Vita....39
2.4.8 Kujibiwa kwa Maombi na Usamehevu wa Mtume....40
2.4.9 Kushuka/Kuteremka kwa Wahyi/Aya za Kurani....41
2.4.10 Mashahidi wa Kiislamu....42
2.5 Maudhui ya Vita na Mauaji....42
2.5.1 Mtume Kama Amiri Jeshi wa Waislamu....44
2.5.2 Ukali wa Vita....44
2.5.3 Vifo....45
2.6 Hitimisho....46
**SURA YA TATU: WAHUSIKA NA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*....47**
3.0 Utangulizi....47
3.1 Dhana ya Wahusika....47
3.2 Aina za Wahusika....50
3.2.1 Mhusika Mkuu....50
3.2.2 Mhusika Msaidizi....51
3.2.3 Mhusika Bapa....51

3.2.4 Mhusika Duara....52
3.3. Wahusika na Uendelezaji wa Maudhui....52
3.3.1 Wahusika wa Makundi....52
3.3.1.1 Jeshi la Waislamu....52
3.3.1.2 Jeshi la Makureshi....54
3.3.1.3 Wanawake Makureshi....55
3.3.1.4 Wanawake Waislamu....56
3.3.1.5 Maswahaba wa Mtume....57
3.3.1.6 Abdallah Bin Ubayyi na Wenzake....58
3.3.1.7 Ukoo wa Banu Abdi-Dari....59
3.3.1.8 Walenga Mishale Hamsini....60
3.3.2 Wahusika Binafsi....62
3.3.2.1 Mtume Muhammad....62
3.3.2.2 Munsabu....64
3.3.2.3. Ubayyi Bin Khalifu....65
3.3.2.4. Utuba na Abdillahi Bin Shihabi....68
3.3.2.5 Abu Sufiani na Hindi....68
3.4 Hitimisho....70
**SURA YA NNE: VIPENGELE VYA KIMTINDO NA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*....71**
4.0 Utangulizi....71
4.1 Tamathali za Semi....71
4.1.1 Sitiari....72
4.1.2 Tashbihi....73
4.1.3 Chuku....75
4.1.4 Uhuishaji/Tashihisi....76
4.1.5 Maswali za Balagha....76
4.1.6 Tabaini....77
4.1.7 Urudiaji na Takriri....78
4.1.8 Semi/Misemo....79
4.1.9 Ukiushi wa Kisintaksia....79
4.2. Dayolojia....80
4.3 Taswira....82
4.4 Hitimisho....84

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .................................. 85
5.0 Utangulizi ........................................................................................................ 85
5.1 Muhtasari wa Utafiti ........................................................................................ 85
5.2 Changamoto ..................................................................................................... 86
5.3 Mapendekezo .................................................................................................... 87
**MAREJELEO** ...................................................................................................... **88**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayojumlisha sanaa za kimaandishi au kimazungumzo mkiwemo hadithi au riwaya, tamthilia na ushairi. Ni aina ya sanaa inayotumia lugha kueleza tajriba za binadamu. Imegawika katika matawi mawili ambayo ni fasihi simulizi na fasihi andishi. Utanzu wa ushairi katika fasihi andishi ndio tunaoushughulikia. Utafiti wetu unahusu *Utenzi wa Vita vya Uhud* wa Haji Chum. Tunachunguza mtindo na maudhui katika utenzi huu.

Wataalamu wametoa fasiri mbalimbali za mtindo. Senkoro (1982) anasema kwamba, mtindo katika fasihi ni namna ambavyo msanii huitunga kazi yake na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui, huainishia kanuni zilizofuatwa za kimapokeo. Fani na maudhui hupangwa ili kuonyesha upekee wa mtunzi husika. Kazi ya mtunzi huweza kuangaliwa kwa namna alivyoipanga. Uwasilishaji wa jambo moja kupitia kwa watunzi wawili huweza kutofautiana. Kwamba, kuna upekee katika uwasilishaji wa kila mmoja wao.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kwamba, mseto wa fani na maudhui ndio mtindo. Mbatia (2001) anasema kwamba mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza. Uchanganuzi wa kazi kimtindo unahusu mambo kama uteuzi wa msamiati, tamathali za semi zilizotumiwa, miundo ya sentensi, aya, beti na kadhalika. Anaendelea kusema kwamba mtindo unahusu vipengele vyote vya lugha. Wamitila (2003) kwa upande wake anaeleza mtindo kama jumla ya mbinu anazozitumia mtunzi katika kutunga kazi ya fasihi. Anaendelea kusema kuwa mtindo ni mbinu za kijumla za uandishi wa kazi husika kama vile uteuzi wa msamiati, aina za sentensi, uakifishi, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, na kadhalika. Kwa jumla, mtaalamu huyu anasema kuwa mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya fasihi. Uchunguzi wetu unahusu mtindo na maudhui katika *Utenzi wa vita vya Uhud.*

Katika utafiti wetu, tutafafanua dhana ya utenzi kwani ndio utanzu wa ushairi tunaoushughulikia. Tenzi hujipambanua kwa sifa zake maalum tofauti na aina nyingine za mashairi. Wataalamu wametoa fasiri mbalimbali za tenzi. Hawa ni pamoja na Abedi (1954), Allen (1971), Harries (1962), Abdulaziz (1968), Lienhardt (1968), Massamba (1983), Knappert (1967), Mulokozi (1999), Mbatiah (2001), Wamitila (2002), miongoni mwa wengine.

Abedi (1954) anasema utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mistari, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho katika kila ubeti ambao huendelea na kina cha namna moja kinachoitwa *bahari.* Abdulaziz (1968) anasema kwamba beti za utenzi huwa na mishororo minne minne yenye vina *aaax, bbbx, cccx,* na kadhalika. Anaendelea kusema kwamba *a, b,* na *c* hubadilikabadilika lakini *x* haibadiliki kwa sababu ndicho kina. Anasema kwamba mizani hutofautiana kutoka utenzi hadi mwingine, lakini kwenye utenzi wote mizani haibadiliki. Kila ubeti, kwa kawaida huwa na mizani nane kwenye kila mshororo. Huu ni mpangilio unaopatikana katika baadhi ya tenzi. Katika utenzi tunaoushughulikia wa *Vita vya Uhud*, mtunzi amefuata muundo huu.

Allen (1971) anasema kuwa wachanganuzi wengi hudai kuwa utenzi waweza kuwa hata na beti mbili. Anapinga madai haya kwa kusema kuwa utenzi wowote unapaswa kuwa na utangulizi, mwili na kiishio, mambo ambayo hayawezi kupatikana katika chini ya beti ishirini. Hivyo, beti za chini ni ishirini na anasema kuwa hakuna kiwango kilichowekwa cha juu cha beti.

Massamba (1983) anasema kuwa utenzi ni mojawapo ya tanzu za ushairi na ni utungo ambao kimaudhui unaelezea tukio fulani linalotokea katika jamii au lililowahi kutokea. Pengine huweza kuwa ni maelezo juu ya wasifu wa mtu, historia au jambo lolote zito lililoelezwa kwa maelezo marefu. Anaendelea kusema kuwa tenzi huwa na beti nyingi kati ya mia na elfu moja na mia tano. Mbatiah (2001) naye anadai kuwa utenzi ni aina ya ushairi unaojipambanua kwa urefu na uzito wa masuala unayoyashughulikia. Utenzi huwa ni mseto wa masimulizi na maelezo yenye urefu wa mamia na maelfu ya beti juu ya wahusika, tukio au jambo zito. Mtindo wake pia ni wa hadhi ya juu.

Wamitila (2002) anasema kuwa utendi hutumiwa kuelezea shairi refu kisimulizi linalozungumzia kwa mapana mtindo wa hali ya juu matendo ya mashujaa au shujaa mmoja. Anaeleza kuwa tenzi nyingi za Kiswahili zinafanana kidhamira na kifani. Asilimia kubwa zina maudhui ya dini ya Kiislamu. Kimtindo, zinatumia fomula sawa za ufunguzi na ufungizi. Mfano, tenzi zote huanza kwa dua na kumalizia kwa dua. Mfano mzuri ni *Utenzi wa Vita vya Uhud* tunaoushughulikia ambapo mtunzi ameanza kwa kumtambua Mungu na kuutaja ukuu wake na akamalizia kwa kumshukuru pia.

Tunaafikiana na maoni ya baadhi ya wataalamu hawa kwamba, utenzi hubeba maudhui mengi na yenye uzito mkuu. Kwa hivyo, idadi ya chini kabisa ya beti isiwe chini ya ishirini, na hakuna kiwango cha juu cha beti. Utenzi unapaswa kuwa mrefu kiasi cha kuwa na utangulizi, mwili na kimalizio (ufungizi) na haya yote hayawezi kuandikwa kwenye beti zilizo chini ya ishirini. Ni maoni yetu kwamba, utenzi hauwezi kuwa na beti chini ya ishirini kwani zitakuwa chache mno kubeba maudhui yanayoshughulikiwa kwa kina. Pia, hakuna kiwango cha juu cha beti.

*Utenzi wa Vita vya Uhud* ni utenzi wa kihistoria unaohusu vita vya kidini. Ni utenzi uliotungwa kwa kutumia lahaja ya Kiamu. Mtunzi wake hajulikani, lakini ulikusanywa na Haji Chum na kuhaririwa na H.E. Lambert mnamo mwaka wa 1959. Ulipigwa chapa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1962. Ni utenzi wenye beti 739.

Haji Chum anasema kuwa alimaliza kuukusanya utenzi huu mwaka wa 1949 huko Mtende, Unguja. Hakuweza kuutia machoni wala masikioni mwa watu hadi mwaka wa 1951, miaka miwili baada ya kuukusanya. Ulichapishwa kwa mara ya kwanza katika gazeti moja la kila mwezi lililoitwa *Mazungumzo ya Walimu* huko Unguja. Ndipo baadaye mwaka wa 1959 ukachapishwa kitabu. Ni utenzi uliotungwa kitambo sana na unamzungumzia Mtume Muhammad.

*Utenzi wa Vita Vya Uhud* unahusu vita vilivyokuwa kati ya Waislamu na Makureshi. Margoliouth (2003) anasema kuwa mlima wa Uhud unaovipa vita hivi jina, uko upande wa Kaskazini Magharibi mwa Madina, takribani maili nne kutoka mji wa Madina. Vita vya Uhud vilikuwa kati ya Makureshi na jeshi la Waislamu la Mtume Muhammad, ambalo Mtume mwenyewe alikuwa amiri jeshi. Vilikuwa vya kulipiza kisasi dhidi ya Waislamu kufuatia vile vya Badr. Badr ni jina la mji ulio kiasi cha kilomita mia na hamsini mbali na mji wa Madina, na ni mahali ambapo hapakuwa na chochote isipokuwa bonde tu na kisima kilichokuwa milki ya mtu mmoja aliyeitwa Badr na kwa ajili hiyo, mahala hapo pakaitwa 'Badr'. Katika vita hivi vya Badr, Waislamu waliwashinda Makureshi.

Vita vya Uhud vilitokea mwaka mmoja baada ya vile vya Badr, na katika muda huu wote, kiongozi wa Makureshi, Abu Sufiyani, alikuwa akilitayarisha jeshi lake la jumla ya wapiganaji elfu tatu. Walipoenda vitani, wanajeshi hawa wa Makureshi waliandamana na wake zao ambao waliwapa motisha katika vita kwa kuimba, kupiga vigoma na kuwakariria mashairi. Mtume Muhammad hakuwa na ufahamu kwamba,

maadui walikuwa tayari kumshambulia, lakini alipothibitisha habari hii, alichukua jeshi la wanaume mashujaa elfu moja waliojulikana kwa ushujaa wao hadi wakapewa jina *panga kali.* Aliondoka Ijumaa na jeshi lake kuelekea Uhud kukutana na Makureshi kwa vita. Makundi haya mawili, hata hivyo yalikubaliana kupigana siku iliyofuata kwani usiku ulikuwa umeingia tayari. Kabla ya kupambazuka siku ya vita, Muhammad na jeshi lake walienda kusali. Abdallah bin Ubaya, aliyekuwa Mwislamu wa uongo aliasi na kukimbia na kundi la wapiganaji mia tatu, wakabaki wapiganaji wa Kiislamu mia saba.

Mtume aliwagawa watu wake katika makundi. Aliwaweka walenga mishale hamsini juu ya mlima kushika doria akiwapa onyo kwamba, wasiondoke mahali hapo mpaka waruhusiwe lakini baadaye walipoona kuwa wenzao wamewashinda nguvu Makureshi, wakaondoka na kujiunga nao kuwakimbiza na kukusanya ngawira. Makureshi walipoona kuwa walinda mlima wameondoka na kuacha mahali hapo bila ulinzi, walitumia fursa hiyo na kupanda mlimani, hivyo wakawashambulia kutoka upande wa nyuma na wakawashinda nguvu. Margoliouth (2003) anaendelea kusema kuwa Makureshi waliouawa walikuwa ishirini na watatu, nao Waislamu walikuwa jumla ya sabini na nne.

Vita hivi vilipiganwa katika awamu kadhaa. Katika awamu ya kwanza, makabiliano makali yalikuwa kati ya Makureshi na jeshi la Mtume ambapo Makureshi walishindwa nguvu na Waislamu na wakakimbia. Jeshi la Mtume likawafuata nyuma wakiokota mali waliyokuwa wameacha. Kwenye awamu ya pili, waliokuwa wameshika doria mlimani walipoona wenzao wameshinda na kulifukuza jeshi la Makureshi, waliona ni heri wafuatane na wenzao kukusanya ngawira kuliko kulinda eneo waliloagizwa. Kwa hivyo, wakakimbia wakaacha mlima bila ulinzi ili wakaungane na wenzao. Makureshi walipoona wapiganaji wa mishale wameondoka mlimani, waliamua kurudi na kuwashambulia Waislamu kutoka nyuma (kutoka mlimani). Hawakuwa na habari hivyo, katika hali hiyo ya kuchanganyikiwa, Waislamu walipigwa sana na wengi wakauawa. Ni katika awamu hii ya vita ambapo Munsabu bin Omar, aliyefanana sana na Mtume, aliuawa. Kutokana na kifo chake, ikasemekana Mtume ameuawa, jambo lililowafurahisha sana Makureshi.

Vita vya awamu ya tatu vilizuka wakati Makureshi walipogundua kwamba, Mtume hakuwa amekufa, wakakasirika sana na kutia juhudi zaidi wamwue. Ubayyi bin

Khalifu, aliyekuwa adui mkubwa wa Mtume na dini yake, jasiri na shujaa, aliamua kupigana ili amwue Mtume. Mtume naye akajihami kwa kijambia cha mmoja wa maswahaba wake na kutoka kukabiliana na adui. Alimchoma Ubayyi kwa kile kijambia shingoni. Ubayyi kwa uchungu mwingi, alikimbia akatoroka. Alikufa akielekea Makka mahali paitwapo Sarifu.

Kifo cha Ubayyi ndicho kilipelekea awamu ya nne ya vita. Baada ya kifo chake, Makureshi waliamua kumwua Mtume kwa vyovyote vile. Ni wakati wa vita hivi ambapo Mtume aliumizwa sana kwa kupigwa mawe kwani hawangemfikia kwa panga zao kutokana na ulinzi aliokuwa nao. Masahaba wake walimbeba na kumficha pangoni walipomlinda. Ni katika pango hili ambapo Bibi Fatima, bintiye Mtume, alichoma nguo za Mtume zilizochanika na kumpaka jivu kwenye majeraha ili kumtibu. Katika vita hivi, Makureshi waliwashinda Waislamu. Makureshi walouawa walikuwa ishirini na watatu nao Waislamu wakauawa sabini na wanne. Waislamu wengine wengi walikuwa wameumizwa vibaya.

Kama tulivyotaja hapo awali, tunashughulikia mtindo na maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa misingi ya nadharia za Umuundo na Uhalisia.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Tenzi nyingi zimefanyiwa utafiti na wahakiki mbalimbali. Hata hivyo, katika uchunguzi wetu kuhusu tahakiki ambazo zimefanyiwa tenzi, hakuna uhakiki wowote tunaoujua wa kiusomi uliofanyiwa *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Kazi iliyopo ni ya utarjumi iliyofanywa na H.E Lambert mwaka wa 1959.

Watafiti wengi wameshughulikia mtindo na maudhui katika baadhi ya tenzi. Wameshughulikia mtindo kivyake na maudhui kivyake. Hawa, miongoni mwa wengine ni pamoja na Wa Mutiso (1985) aliyeshughulikia maudhui ya Hurafa na Uyakinifu katika *Utenzi wa Hamziyya* na Lugwiri (2011) ambaye ameshughulikia mtindo katika *Utenzi wa Tambuka.*

Japo dhana hizi mbili zinaweza kuchunguzwa kila moja kivyake, katika uchunguzi wetu tutaangazia mawazo ya mtaalamu Wamitila (2003) anayesema kwamba dhana hizi zinachangizana na haziwezi kutenganishwa. Ndipo tukaona ni muhimu kuchunguza maudhui na mtindo vinavyojengana katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Katika uchunguzi wetu, tunapania kujaza pengo lililopo la kukosa uchambuzi wa

kimtindo na kimaudhui kwa pamoja kuhusu utenzi huu haswa namna mtindo unavyoendeleza maudhui. Tumeona kuwa kuna haja ya kuuchunguza utenzi huu kwa misingi hiyo ili tubaini mbinu mbalimbali alizotumia mtunzi kuwasilisha ujumbe.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Katika utafiti wetu, tuna madhumuni yafuatayo:

1. Kuchunguza maudhui katika *Utenzi wa Vita* vya *Uhud.*
2. Kuchunguza wahusika na maudhui na mchango wao katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*
3. Kuchunguza baadhi ya vipengele teule vya kimtindo na maudhui na mchango wao katika *Utenzi wa vita vya Uhud.*

## 1.3 Sababu za Kuchagua Mada

Tumepitia tahakiki mbalimbali zilizofanywa kuhusu tenzi za Kiswahili na tukagundua ya kwamba, utenzi huu ulishughulikiwa tu na wageni wa Kizungu ambao waliufanyia tafsiri ya Kiingereza. Kazi hizi zimetusaidia sana katika kuelewa utenzi wenyewe, hasa kwa upande wa lugha kwani lugha iliyotumiwa ni ya zamani na haitumiki katika Kiswahili cha sasa. Pia wageni hawa wameyaorodhesha baadhi ya maneno ya kilahaja yaliyotumiwa kwenye utenzi na kupeana maana na maelezo yake kwa lugha ya Kiswahili na pia Kiingereza. Maelezo haya yatasaidia sana katika utafiti wetu. Ilitubidi tuwahusishe wasimamizi wetu katika jambo hili kwa ufahamu kwamba, wazungu hao si wenyeji wa lugha hii na vile vile kwa kuwa si Waislamu, huenda hawakueleza baadhi ya dhana za dini kwa uhalisi wake. Hata hivyo, kwa ufahamu wetu, hakuna utafiti wowote wa kiusomi uliofanyiwa utenzi huu. Kwa hivyo tumefanya uhakiki wa kimaudhui na kimtindo ili kuziba pengo hili.

Sababu iliyotufanya tuuchambue *Utenzi wa Vita vya Uhud* kimtindo na kimaudhui ni umuhimu na ukongwe wa utanzu wa ushairi wa Kiswahili na pia kutokuwepo kwa kazi za kihakiki za kiusomi za utenzi huu. Kama tulivyotangulia kusema, wageni kama vile Lambert walikusanya, kuhariri na kutafsiri tenzi hizi pasi na kushughulikia maswala ya kiusomi kama vile mtindo na maudhui. Kazi hii ya wageni, japo inamsaidia msomaji wa tenzi kuzielewa zaidi, haina manufaa mengine kwa msomaji kama vile kumkuza kiusomi katika fani ya fasihi ya Kiswahili. Pia, ni utenzi ulio na matukio muhimu sana ya historia ya dini ya Kiislamu. Mambo haya yametutia ari ya kuufanyia utenzi huu utafiti wa kimaudhui na kimtindo.

*Utenzi wa Vita vya Uhud* ni mojawapo ya tenzi za kale uliotungwa kwa kutumia msamiati wa kale usiotumika katika Kiswahili cha sasa. Halikadhalika, mtunzi wake ametumia mseto wa lahaja. Uchangamano huu wa lugha huwafanya wasomaji wengi kutousoma kwani huwawia vigumu kuupata au kuuelewa ujumbe anaodhamiria kuupitisha mtunzi. Kulingana na Mutiso (1996), tenzi hizi za zamani zinaogopewa na wanafunzi hata wale wanaotumia Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Hali hii ndiyo imetupa changamoto kuuchanganua *Utenzi wa Vita vya Uhud* ili kuwafaidi wasomi wa fasihi ya Kiswahili kwa kuwarahisishia uelewaji wake. Pamoja na kutoa mchango wetu wa kiusomi katika ushairi na fasihi kwa jumla, tunatarajia kuwa uchunguzi huu utamwezesha msomaji wa fasihi ya Kiswahili kulinganisha matumizi ya lugha yalivyokuwa nyakati za kale na yalivyo hii leo. Matarajio yetu ni kuwa utafiti huu utachangia pakubwa katika fasihi ya Kiswahili hasa kwenye kipera cha tenzi na pia kuwakuza wasomi wa fasihi kwa jumla. Tunatarajia kuwa utafiti wetu utawasaidia wasomaji wa fasihi na kuelewa kipera hiki kwa urahisi na kwa njia iliyo bora.

## 1.4 Upeo na Mipaka

Katika utafiti wetu, tunashughulikia mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Utenzi wa Vita* vya *Uhud.* Utafiti wetu unaongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Umuundo na nadharia ya Uhalisia. Nadharia ya Umuundo husisitiza kuhakiki kimuundo bila urejelezi wa nje. Ni nadharia iliyotuongoza katika kushughulikia matumizi ya lugha. Ni nadharia inayompuuza mwandishi na kushughulikia lugha anayoitumia pekee. Nadharia ya Uhalisia nayo inatuongoza kushughulikia maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Ni nadharia inayotazama mambo yalivyo katika hali yake halisi katika kipindi fulani cha historia na katika muktadha huo huo tu.

Dhana hizi mbili (maudhui na mtindo), kulingana na Wamitila (2003), haziwezi kutenganishwa na kama anavyosema Mishra (2011) akimnukuu Kant kwamba, fani bila maudhui ni utupu nayo maudhui bila fani ni upofu na huwezi kushughulikia kimoja na kupuuza kingine. Tukitilia maanani kuwa mtindo ndiyo malighafi yanayojenga kazi yoyote ya fasihi na kwamba, ndiyo husitiri maudhui, tutashughulikia maudhui ya ushujaa, vita, mauaji na dini ambayo ndiyo maudhui yaliyoutawala utenzi. Yapo maudhui mengi yanayojitokeza kwenye utenzi, lakini

utafiti wetu utajibana kwa haya manne. Tumeyateua kwa sababu ndiyo yametumiwa na mtunzi kumkuza Mtume Muhammad kama shujaa wa Uislamu na jamii yake.

Kuna vipengele vingi vya kimtindo, lakini katika utafiti wetu tumejibana katika wahusika na matumizi ya lugha, taswira na kunga nyinginezo za kimtindo. Tumechunguza jinsi vipengele hivi vinavyochimuza maudhui haya ya ushujaa, vita, mauaji na dini. Kuna wahusika wengi kwenye utenzi, lakini katika kuchunguza maudhui ya ushujaa, tumemteua Mtume Mohammad ambaye ndiye amechukua nafasi kubwa sana kuyakuza maudhui haya kwani licha ya kuwa mhusika mkuu, yeye ni mtume/nabii wa Mungu na ni tofauti na wahusika wengine. Kwamba, yeye si binadamu wa kawaida kama walivyo wahusika wengine. Hivyo, mtunzi amemkuza kwa njia ya kipekee na ana sifa za kipekee, sawa na za mashujaa wengine duniani. Tutanukuu mifano moja kwa moja kutoka katika utenzi wenyewe ili kuthibitisha mtunzi ametumia kunga zipi na kwa nini. Pia, kwa kuwa Mtume ni shujaa wa kidini, tumemlinganisha kwa kiasi fulani na mashujaa wengine wa kidini, hasa Nabii Isa (Yesu) wa Kikristo, pale ambapo tutaona pana haja ya kufanya hivyo.

## 1.5 Nadharia Tete

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Maudhui ya kidini ndiyo maudhui yanayotawala *Utenzi wa Vita vya Uhud.*
2. Mtunzi amewatumia wahusika kuendeleza maudhui ya kidini pekee katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*
3. Vipengele vya kimtindo vilivyotumiwa vimesaidia kuchimuza maudhui ya kidini katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Licha ya ukweli kwamba historia ya tenzi inarudi nyuma hadi karne ya kumi na tatu pwani ya Afrika Mashariki na katika fasihi ya Kiswahili, ni kazi chache sana zilizofanyiwa uchanganuzi na uhakiki wa kiusomi. Baadhi ya kazi zilizopo zilifanywa na wageni hasa wa Kizungu ambao walikusanya miswada kutoka kwa wenyeji, wakaihariri na wakaitarjumi kwa lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, kuna wahakiki wengine ambao wamezifanyia tafiti za kiusomi baadhi ya tenzi za zamani. Wageni hawa ni kama vile H. E Lambert ambaye alitafsiri na kuhariri *Utenzi wa Vita vya*

*Uhud* (1959) miongoni mwa tenzi nyingine na Allen (1971) aliyehariri *Utenzi wa Abdirrahman na Sufiyani*. Wengine waliofanya tafiti za aina hii ni pamoja na Harries (1962), Knappert (1967, 1979, 1983), na Hichens (1972) miongoni mwa wengine. Knappert (1979) ameshughulikia mashairi ya Kiswahili na historia yake katika karne za 17, 18, 19 na 20 ambapo anatoa muhtasari wa utunzi wa Afrika Mashariki na kuonyeha jinsi utamaduni wa Waswahili wenyewe ulivyoathiri kazi za kishairi wakati huo. Harries (1962) ameshughulikia tenzi mbalimbali. Hizi ni pamoja na *Utendi wa Mwanakupona* miongoni mwa nyingine. Allen (1971) alitafsiri *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* kwa lugha ya Kiingereza miongoni mwa nyingine. Wageni hawa hawakushughulikia muundo wa kazi hizi kwa undani. Licha ya bidii zao za kutarjumi na kuhariri baadhi ya kazi za Kiswahili, wamepuuziliwa mbali na wasomi wa kisasa wa fasihi. Kwa mfano, Mulokozi (1999) anadai kwamba wageni hao, japo walifanya juhudi kukiendeleza na kukikuza Kiswahili, walikuwa na ujuzi mdogo sana wa fasihi; waliloweza kufanya ni kukusanya maandishi ya Kiswahili na kutafsiri kwa lugha yao ili wajinufaishe wenyewe.

Ingawa ukweli huu una mashiko kwa kiasi fulani, ni maoni yetu kwamba, tafsiri zao na kazi finyu walizozifanya ziliweka msingi mzuri wa uelewa na uhakiki wa tenzi za Kiswahili. Uhakiki wa tenzi mbalimbali umeshughulikiwa kwa kiwango kidogo, sababu ikiwa matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili na pia matumizi ya msamiati wa Kiarabu kwa upana ambao huwatatiza wasomaji wasiokuwa Waswahili au Waislamu. Licha ya tatizo hili, baadhi ya tenzi za kale zimetafitiwa. *Utenzi wa Vita vya Uhud*, hata hivyo, haujafanyiwa utafiti wowote wa kiusomi kulingana na ufahamu wetu.

Kando na kazi zilizofanywa na wageni hao, kuna watafiti wengine wa fasihi ya Kiswahili ambao pia wameshughulikia tenzi. Tumepitia baadhi ya kazi zao ambazo tumeona kuwa zitakuwa za manufaa kwetu.

Kadenge (1982) anachunguza dhana za ukiushi na uchimuzi katika fasihi ya Kiswahili. Anasema uchimuzi na ukiushi ni dhana za kukiuka sheria zinazotawala matumizi ya lugha. Anaendelea kusema kuwa huu ni ukiushi wa kimakusudi wa lugha kwa madhumuni ya kusisitiza ujumbe kwenye kazi fulani ya kifasihi. Vipengele vya ukiushi, kulingana na mhakiki huyu, vina jukumu la mawasiliano kwa hivyo, inachukuliwa kuwa mwandishi anavitumia ili kupitisha ujumbe wake kwa hadhira au

kwa msomaji. Kazi alizozishughulikia ni utenzi wa *Swifa ya Nguvumali*, riwaya ya *Asali Chungu* na tamthilia ya *Wakati Ukuta*. Kati ya kazi hizi tatu, matumizi ya lugha katika *Swifa ya Nguvumali* ndiyo inatuhusu na itakuwa ya manufaa kwetu kwani kazi yenyewe inahusu utenzi sawa na yetu na ameshughulikia swala la maudhui na mtindo ambalo pia sisi tumeshughulikia katika utafiti wetu. Tofauti iliyopo ni kwamba tunashughulikia kazi tofauti na tutaangazia jinsi baadhi ya vipengee vya kimtindo vinavyomchimuza Mtume Muhammad.

Wa Mutiso (1985) ameshughulikia maudhui ya Hurafa na Uyakinifu katika *Kasida ya Hamziyya*. Katika tasnifu yake amelinganisha sifa za Mtume Muhammad na za mashujaa wengine wa jamii nyingine. Mtafiti yuyu huyu (2005) alishughulikia *Kasida ya Hamziyya* ambapo alitafitia fani yake. Kazi hizi zimetufaa sana katika uhakiki wa mtindo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Pia, kwa upande wa wahusika, kazi zake zitatufaidi pakubwa hasa tuakapokuwa tukimshughulikia mhusika mkuu Mtume Muhammad katika utenzi huu kwa upande wa sifa zake kama shujaa. Wa Mberia (1989) anahakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Anachanganua sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa kimasimulizi. Ni kazi iliyotuongoza tulipokuwa tukishughulikia kipengele cha wahusika. Tofauti iliyopo ni kwamba, yeye Mberia ameshughulikia shujaa wa kijamii nasi tunamshughulikia shujaa wa kidini. Swaleh (1992) anashughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Mtafiti huyu ameangazia swala la maudhui kwa undani sana. Kazi hii imetupa mwelekeo katika uhakiki wa maudhui. Mojawapo wa maudhui aliyoyashughulikia ni yale ya kidini, ambayo pia nasi tunayashughulukia. Tofauti yetu na mtafiti huyu ni kwamba, tunashughulikia kazi tofauti, ambapo utenzi tunaoushughulikia ni wa kidini ilhali alioushughulikia ni wa kijamii japo umetungwa katika mazingira sawa na ya *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Omwayo (1997) ameshughulikia fani katika Ushairi wa Mwalimu Mbega, anahakiki *Upisho wa Malenga na Dafina ya Umalenga* akitumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Anachukulia kuwa fani ina mchango mkubwa katika kufumbata malengo ya msanii. Katika utafiti wetu, tumechunguza mtindo na maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* tukitumia nadharia ya umuundo na ya uhalisia. Utafiti wa Omwayo (1997) umetusaidia tulipokuwa tukichunguza jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui katika utenzi teule. Mungai (2005) amefanya ulinganishi wa tenzi za *Swifa ya Nguvumali* na *Mikidadi na Mayasa* kwa misingi ya nadharia ya Urasimu, kazi ambayo imetusaidia katika uhakiki wetu wa fani, japo ameshughulikia vipengele vichache mno zaidi yetu.

Wesah (2005) ameshughulikia uhakiki wa fani katika *Utenzi wa Mwanafatuma* na *Utenzi wa Siri Li Asirali* kwa misingi ya nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Ameshughulikia vipengele mbalimbali ambavyo amevieleza pasi na kuonyesha matumizi na ufaafu wake katika ujenzi wa tenzi zenyewe. Katika uchunguzi wetu, tumeonyesha jinsi kunga hizi zilivyotumiwa na kujengana ili kuwasilisha ujumbe wa utenzi. Hata hivyo, kazi ya mtafiti huyu imetusaidia katika ufafanuzi wa vipengele vya kimtindo tunavyovishughulikia katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Mukuthuria (2007) ametafiti upekee wa utenzi wa *Swifa ya Nguvumali* ambapo ameshughulikia wahusika kwa kina. Kazi yake pia imetupa mwanga katika uhakiki wa kipengele cha wahusika. Kofa (2009) anahakiki fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* akitumia nadharia ya Umuundo. Anachunguza matumizi ya fani baada ya kuzirodhesha fani zenyewe. Kazi yake imetufaa sana katika uchanganuzi wa kimtindo katika *Utenzi wa Vita Vya Uhud* kwa kuwa baadhi ya vipengele vya kimtindo vilivyomo kwenye utenzi alioushughulikia vilevile vipo kwenye utenzi tunaoushughulikia. Tofauti iliyopo ni kwamba, kwenye utafiti wetu tunachunguza baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyokuza maudhui.

Lugwiri (2011) anashughulikia mtindo katika *Utenzi wa Tambuka* ambapo alishughulikia sitiari, taashira na tashibiha na mchango wavyo katika uwasilishaji wa dhamira ya mtunzi. Ametumia nadharia ya Umitindo. Kazi yake imetufaa sana kwa sababu tunashughulikia maudhui na mtindo pia. Hata hivyo, tumetofautiana na mhakiki huyu kwa sababu ametumia nadharia ya umitindo lakini sisi tumetumia nadharia mbili, ya umuundo na ya uhalisia. Murumba (2011) amehakiki mtindo unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala*, naye Muthoni (2014) akahakiki maudhui katika *Tikitimaji.* Kazi hizi zimetupatia mwanga katika utafiti wetu kwa upande wa matumizi ya lugha na maudhui kwa kuwa baadhi ya vipengele vya kimtindo walivyovitumia pia nasi tutavishughulikia. Tofauti kuu ni kwamba tunashughulikia utenzi na wao wametafitia tamthilia na riwaya, mtawalia.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti wetu unaongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Umuundo na nadharia ya Uhalisia. Nadharia ya umuundo imetuongoza katika uchunguzi wa lugha nayo Nadharia ya uhalisia imetuongoza tuliposhughulikia maudhui.

### 1.7.1 Nadharia ya Umuundo

Sababu ya kuchagua nadharia hii ni kuwa imetufaa katika uchanganuzi wetu wa vipengele vya kimtindo tunavyovishughulikia katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* ili kubainisha jinsi vipengele hivyo vinavyoungana kuunda umbo la kazi nzima na kufanikisha ujumbe. Ufaafu wake unatokana na sifa ya nadharia yenyewe ya kuangalia uhakiki wa kazi za kifasihi kwa misingi ya kunga zilizotumika katika matini bila urejelezi wa nje.

Mbatiah (2001) anasema kwamba umuundo ni nadharia ya uhakiki iliyoibuka katika kipindi cha miaka ya hamsini hadi sitini. Ni nadharia inayoshughulikia fasihi katika mawazo ya mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Katika mwelekeo wa Umuundo, fasihi inaangaliwa kama mfumo wa ngazi ya pili unaotegemea mfumo wa ngazi ya kwanza ambao ni lugha. Uhakiki wa kimuundo unatumia dhana za kiisimu katika uchambuzi wa matini za kifasihi. Umuundo unaangaliwa na wahakiki wengi kama nadharia iliyotokana na ufani. Wamitila (2003) anasema kuwa umuundo ni istilahi inayotumiwa kueleza aina za uhakiki ambao unachunguza kaida zilizopo katika uundaji wa kazi fulani. Ukuaji wa nadharia ya umuundo unahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Umuundo unatilia mkazo kwenye muundo wa kazi. Wanaumuundo wanashikilia kuwa fasihi imepangwa kama lugha. Hii ina maana kwamba, kwa vile lugha ni mfumo, fasihi nayo ni mfumo. Kwamba, mfumo wa fasihi umejengwa kwa kutumia kunga mbalimbali za fani kama mfumo wa lugha unavyojumlisha sauti na ishara.

Nadharia ya umuundo iliasisiwa na wasomi kama R. Jakobson, N. Trubetzkoy, J. Mukarovsky, miongoni mwa wengine kati ya miaka ya 1928 na 1946 ambao walihusika na Urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Wasomi hawa walibuni kundi lililojulikana kama "Shule ya Isimu ya Prague" na wakaitumia kuendeleza mawazo yao. Umuundo ni mwendelezo wa jitihada za urasimu za kubuni sayansi huru ya mtalaa wa fasihi. Miongoni mwa wataalamu wengine, Scholes (1974) anasisitiza kwamba, msingi wa umuundo ni urasimu. Baadhi ya wanazuoni waliohusishwa na ukuzaji wa urasimu pia walichangia katika kuasisi umuundo. Mfano ni Roman Jakobson. Kwa jumla, wanaisimu wa Shule ya Prague walitoa mchango muhimu katika kuchipuka kwa umuundo. Kama urasimu, uhakiki wa kimuundo una mwelekeo

wa kulenga matini ya kifasihi na kupuuza maswala mengine ya nje kama vile mawazo ya mtunzi na muktadha wa kijamii.

Waasisi wa umuundo walitumia mawazo ya mwanaisimu Fedinand de Saussure ambaye alibuni dhana mbalimbali za kiisimu na akawafundisha wanafunzi wake. Dhana zilizobuniwa na Saussure ni pamoja na *Langage* (lugha ijulikanayo na kutumiwa na jamii), *Langue* (sheria na kanuni za lugha au mfumolugha) na *parole* (matumuzi ya lugha katika mazungumzo na maandishi). Kwamba, mfumolugha ni jumla ya kanuni, kaida na sheria za lugha ambazo kila mtumiaji wa lugha hujifunza nayo "parole" ni utekelezaji wa kanuni za lugha kimatumizi. Wana-Umuundo walitumia dhana hizi kusisitiza kuwa ili kuuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, mhakiki anafaa kuchunguza matumizi ya lugha katika maandishi na mazungumzo, vipengele vyake na mahusiano yake.

Wana-Umuundo walielezea kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama *langue* na una kaida zake. Hivyo, kazi ya kifasihi inapaswa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni bia za utanzu zinazoitawala. Kwa mfano, katika Utenzi wa *Vita vya Uhud*, tumechagua lugha ilivyotumiwa na sheria zinazotawala utunzi wa utenzi. Kwa kufanya haya, tutaweza kubainisha kama mtunzi alizifuata sheria hizo.

Saussure alibaini kuwa *parole* ni lugha ya kimatumizi ilhali *langue* ni mfumo lugha ulio na jumla ya taratibu za lugha ambazo msemaji wa lugha anazifahamu. Fasihi inaweza kuangaliwa kama mfumo ulio na kanuni, taratibu na sheria zake. Kila msanii wa fasihi ni lazima aelewe jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa kama ya mawasiliano na hata kimuundo. Waasisi wa umuundo walitumia dhana za Saussure za kiashiria na kiashiriwa na wakaeleza kuwa lugha huundwa kwa viashiria na viashiriwa. Waliviona vipengele vya fani kama viashiria na maana inayotokana na vipengele hivi vya kimtindo kama viashiriwa. Pia, walijihusisha na uhakiki wa mashairi na tungo nyingine za kifasihi ambapo walichunguza upatanifu wa sauti, vina, mizani, na arudhi. Pia, katika usimulizi walizungumzia umbo la msuko, hadithi na usawiri wa wahusika. Vile vile walipendekeza mbinu za kifani kama vile jazanda, taswira na tamathali za usemi. Mbinu hizi hutofautisha lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida au ya taaluma nyingine.

Kwa mujibu wa wanaumuundo, kufaulu kwa kazi ya kifasihi hutokana na mbinu za kifani anazotumia mtunzi. Uhakiki wa kazi ya kifasihi haufai kuwa na urejelezi wa nje. Hawatilii maanani msanii wa kazi ya kifasihi wala dhamira yake. Muundo wa kazi ya kifasihi ndio unafaa kutiliwa maanani kuliko mandhari ya kijamii ya kazi husika. Pia, walipuuza kuhusishwa kwa fasihi na mtunzi wake.

Nadharia ya umuundo ina misingi yake katika mawazo ya Ferdinand de Saussure. Inasisitiza uhakiki wa kazi pasi na kuihusisha na jamii wala mwandishi na pia inapuuza ufasiri wa msomaji. Kulingana na nadharia hii, kilicho muhimu ni muundo wa kazi inayohusika wala sio maudhui au ujumbe wake. Mwandishi, hadhira na muktadha wa kijamii unapaswa kupuuzwa. Pia inaangalia jinsi maneno yalivyopangwa na kuhusiana ili kutoa maana bila urejelezi wa nje.

Kimsingi, wana-Umuundo hawatilii maanani msanii wa kazi ya kifasihi wala dhamira yake. Cha maana ni lugha iliyotumiwa. Ni mtazamo unaofichua uashiriaji ambapo viashiria vina maana zaidi kuliko viashiriwa. Kwa mfano katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, mtunzi ametumia sitiari *panga kali* kuashiria wapiganaji wa Mtume Muhammad. Hii ni sitiari iliyotumiwa kuashiria ukali wa wanajeshi hawa. Katika hali hii, mtafiti anapaswa kuchunguza tabia ya panga ili tuweze kuelewa mtu anayezungumziwa ni mhusika mwenye tabia ya aina gani. Katika utenzi, tabia zake hazijatajwa kwa njia ya moja kwa moja, ila zimebanwa kwenye sitiari iliyotumiwa. Muundo wa lugha hapa umepuuza tabia ya kiashiriwa (panga). Kwa hiyo, kiashiria, kulingana na wana-Umuundo, kina maana zaidi kuliko kiashiriwa. Kumaanisha kwamba, yule anayefananishwa na panga ni muhumu kuliko upanga wenyewe.

Nadharia ya umuundo inatufaa katika utafiti huu kwani inatilia mkazo mwingiliano wa vipengele vya kimtindo katika ujenzi wa umbo moja la kazi ya kifasihi, jambo ambalo linaafikiana na malengo ya utafiti wetu.

### 1.7.2 Nadharia ya Uhalisia

Ingawa Uhalisia kama tapo la kuwaelekeza watunzi ulianza kudhihirika mwaka wa 1800 enzi za Mfaransa Gustav Flaubert, ni dhana iliyoanza kujitokeza zamani sana, baina ya mwaka 1100 na 1500 Baada ya Kristo. Ilifanyiwa mabadiliko na wataalamu kama vile Emmanuel Kant (1790) na Schiller (1798). Wataalamu mbalimbali wamezungumzia nadharia hii.

Msokile (1993) anasema kwamba uhalisia ulianza mwaka wa 1820. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa inafaradhiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Pia, ni nadharia inayopendekeza ujenzi wa wahusika unaoingiliana na hali halisi, yaani mhusika awe na sura ile ile ya maisha ya kawaida. Hii ni kwa sababu sanaa inapaswa ieleze ukweli na iweze kueleweka. Kazi za kihalisia, hivyo basi zinatarajiwa kuakisi hali halisi za maisha katika jamii.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kwamba uhalisia ndiyo nadharia muhimu zaidi katika karne ya kumi na tisa na ishirini na huenda itaendelea kutuathiri katika karne ya ishirini na moja. Uhalisia, katika mawanda ya fasihi ulitokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu. Matatizo haya yaliwafanya wanasanaa kuutuhumu ulimbwende. Matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Walimbwende walijitungia mambo yasiyoweza kutimia, kwamba, waliishi ndotoni. Hivyo, uhalisia ulipinga ulimbwende. Gustav Flaubert, mmoja wa waanzilishi wa uhalisia, alishikilia kwamba, mtu hufikiria kwa kichwa chake wala si moyo. Kwa kusema haya, alilaani dhana iliyowaongoza walimbwende katika utungaji. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Akinukuliwa na Njogu na wenzake (1999), mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetics* (ujumi), alitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Mbatiah (2001) anasema kwamba, kimsingi, uhalisia ni istilahi inayorejelea mtindo wa uandishi na inajishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahsusi. Ni mkondo muhimu wa uandishi unaohusishwa hasa na utanzu wa riwaya. Uhalisia pia hutumiwa kwa maana ya tapo mahsusi la uandishi lililoibuka Ulaya katika karne ya kumi na nane na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Wasanii wa kiuhalisia walijishughulisha kuutafuta pamoja na kuubainisha ukweli wa maisha. Waliamini ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya binadamu. Hivyo, walijikita katika mazingira halisi ya kijamii na kujaribu kuyasawiri kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi.

Wamitila (2002) anasema kuwa nadharia hii iliwekewa msingi na Hegel (1979). Aliueleza uhalisia kama nadharia ya kifasihi ambayo inahusiana na ulimwengu na maisha ya kijamii ambayo ina mhusika anayetenda mambo kwa kuchochewa na hali

hiyo. Anaendelea kusema kuwa msingi mkubwa wa tapo hili ni usimulizi wa kimuhakati ambao ni usimulizi unaosimulia matukio kama yalivyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Hivyo, mwandishi au mwanasanaa anapaswa kuvielewa vipengele vya kijamii vinavyosababisha mabadiliko kama hayo na kuathiri hali ya uhalisia kila wakati. Wanafasihi wa tapo hili wanaamini kwamba, yale mambo au maswala yanayoshughulikiwa na mwandishi fulani yanapaswa kuthibitika katika ulimwengu halisi. Wamitila anasisitiza kwamba, kazi yoyote inayoandikwa katika msingi huu ni lazima ikaribiane na kueleza ukweli katika jamii husika. Uhalisia hutofautiana kulingana na jamii, kwamba, hakuna jamii iliyo na uhalisia sawa na nyingine.

Wamitila (2003) anasema kuwa uhalisia ulizuka kama vuguvugu la kuupinga mtazamo wa ki- ulimbwende. Ni mkondo unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku.

Wataalamu tuliotangulia kuwataja wanakubaliana kwamba, uhalisia unasisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama ilivyo katika maisha ya jamii ya kila siku. Nadharia hii imetuongoza katika utafiti wetu kwa sababu katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* tunashughulikia maswala halisi ambayo yalipatikana katika jamii ya Waislamu. Maswala haya ni kama vile vita vya kidini, imani na ushujaa wa Mtume Mohammad, ambaye ndiye mhusika mkuu na pia anayeendeleza dini ya Kiislamu. Haya ni maswala halisi ambayo kila Mwislamu anayatilia maanani katika maisha yake. Waandishi katika kazi za uhalisia huonyesha msimamo wao kuhusu yale wanayoyazungumzia. Kwamba, licha ya kujizatiti kuakisi hali halisi ya maisha, hutetea wahusika fulani na kuwashambulia wengine. Haya hutegemea msimamo wake. Jambo hili linajitokeza hadharani katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* ambapo mwandishi anapinga sana msimamo wa kidini wa Makureshi na kumtetea Mtume Muhammad, kama mtetezi wa dini inayofaa. Nadharia hii imetuongoza katika utafiti wa maudhui yanayopatikana kwenye utenzi na hasa ya ushujaa. Maudhui yanayojitokeza ni maswala yaliyopo katika ulimwengu na historia ya Uislamu na kiongozi wake Mtume Muhammad ni mambo halisi.

## 1.8 Njia za Utafiti

Tumeusoma *Utenzi wa Vita vya Uhud* kwa kina na pia kudurusu matini mbalimbali zilizokuwa na manufaa kwetu. Kazi hizi ni pamoja na vitabu, tasnifu na majarida yanayozungumzia maudhui na mtindo katika ushairi na tenzi kwa jumla, ambayo tumeyapata maktabani. Kwa upana, tumesoma baadhi ya vitabu vya dini, hasa vinavyozungumza kuhusu Mtume Muhammad ili kuthibitisha kuwa yale mtunzi aliyoyasema kumhusu ni ya ukweli au ni mbinu za utunzi hasa pale anapotumia chuku. Pia, tumetalii mitandao tupate marejeleo zaidi kuhusu nadharia ya Umuundo na Uhalisia na maendeleo yazo. Wasimamizi wetu pia wametufaa sana kwa sababu tumepata ushauri na mwongozo wa kimsingi kutoka kwao katika hatua zote za utafiti wetu. Uteuzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* kama malighafi ya utafiti wetu, ni wa kimakusudi.

# SURA YA PILI

## UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumechanganua maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Tumechunguza sifa bia za shujaa kisha tukamwangazia Mtume Muhammad kama shujaa wa kidini na sifa alizo nazo na zinazojitokeza kwenye utenzi, pia tumeshughulikia maudhui ya dini, vita na mauaji kama yanavyojitokeza katika utenzi.

### 2.1 Dhana ya Maudhui

Wataalamu wamefafanua dhana hii ya maudhui kwa njia mbalimbali. Hawa ni pamoja na: Njogu na Chimera (1999) wanaosema kwamba maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi iwe riwaya, tamthilia, shairi au wimbo. Ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa na mwandishi hujitokeza. Kulingana na maoni ya wataalamu hawa, tunaweza kusema ya kwamba maudhui ni maana ya ndani ya kazi ya fasihi, ni mawazo ya mtunzi kutegemea muktadha fulani.

Amata na King'ei (2001) wanaeleza maudhui kama jumla ya mambo, mawazo, mafundisho au ujumbe unaowasilishwa na mshairi kwa hadhira yake. Ni kiini cha shairi. Anaendelea kusema kuwa maudhui katika shairi hutokana na jamii ya mwandishi wala si kutokana na ombwe tupu. Yale ayatungayo hutokana na jamii anamoishi. Kwamba, hupata msukumo au kariha ya kutunga mashairi yake kutokana na mambo yanayomkera au yanayomgusa katika jamii yao. Maoni ya mwandishi huyu ni ya kweli kwani kulingana na utenzi tunaoushughulikia, mtunzi anazungumzia dini ya Kiislamu ambayo ndiyo dini ya kweli, na anapinga Makureshi ambao ni makafiri walioasi dini hiyo, jambo linalotokea katika jamii yake.

Mbatiah (2001) anasema maudhui, ambayo pia huitwa yaliyomo, ni jumla ya mawazo, fikra, dhamira na hisia zinazowasilishwa na kazi ya kifasihi. Kwa upande mmoja, anasema kuwa maudhui yanajibu swali la nini kazi ya kifasihi inazungumzia, na kwa upande mwingine, fani inajibu swali la vipi maudhui yanavyowasilishwa. Kimsingi, vipengele hivi havitenganishiki. Hivyo, katika utafiti wetu, tunachunguza

mtindo na maudhui ili kudhihirisha maoni ya mtaalamu huyu kwamba mtindo una mchango mkubwa katika ujenzi wa maudhui.

Wamitila (2003) anaeleza maudhui kama jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maudhui hujumuisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo. Wamitila (ametajwa) anaeleza kuwa falsafa ya mwandishi ni fikra kuu za mtunzi au mwandishi wa kisanaa. Fikra hizo hutokana na imani na msimamo wa mwandishi anayehusika na huathiri kwa kiasi kikubwa jinsi anavyotazama mazingira yake. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, falsafa na mazingira ya mtunzi ni ya dini ya Kiislamu.Anamsawiri Mtume Muhammadi kama mhusika wa kipekee kwa kuwa ni Nabii wa Mungu na pia kiongozi wa dini ya Kiislamu. Mtaalamu huyu anaelezea ujumbe kama taarifa aipatayo msomaji asomapo shairi au kazi ya fasihi. Ujumbe waweza ukawa mzuri au mbaya. Ujumbe tunaoupata katika utenzi tunaoushughulikia ni kwamba kutotii maagizo (ya Mtume) huleta maafa, na pia dini ya Kiislamu ndiyo dini ya kweli. Dhamira ni lengo la mtunzi katika utungo wake ambalo hutoka kwa wazo kuu ambalo hukuzwa katika utungo unaohusika kuanzia mwanzo hadi mwisho. Lengo la mtunzi katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* ni kuonyesha umuhimu wa dini ya Kiislamu na pia haja ya kumtii Mungu na kufuata maagizo ya Mtume.

## 2.2 Maudhui ya Ushujaa

Shujaa ni mtu mwenye ujasiri, awezaye kukabili mambo ya hatari bila hofu. Pia huitwa jasiri, nguli, nyamaume au jabari. Shujaa wa kifasihi ni kiumbe mwenye sifa zisizo za binadamu wa kawaida zinazoweza kuwa za kimaumbile, kitabia au kihisia. Shujaa wa dini, hata hivyo huwa ni kama binadamu wa kawaida, japo ana sifa za kipekee alizopewa na Mungu. Swala hili la mashujaa na sifa zao limeshughulikiwa na watalamu mbalimbali. Hawa ni pamoja na Carlyle (1924), Kunene (1971), Mutiso (1985, 1999) na Gaster (1987) miongoni mwa wengine. Tutataja tu baadhi yao walivyosema kuhusu shujaa.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kwamba majagina katika sehemu nyingi ulimwenguni huwa na sifa ya usikawaida. Huwa na uwezo ambao si wa kibinadamu. Majagina wengi huwa watu wakubwa sana wasioulika, wenye miili inayoonekana kuwa si ya nyama bali ya chuma; hivyo, silaha za kawaida haziwezi kupenya miili yao. Mtume Muhammad ndiye anayesawiriwa kama shujaa wa dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Hata hivyo, shujaa huyu ni binadamu wa kawaida

kimaumbile. Licha ya kuwa binadamu na anayetangamana na watu wengine, ana sifa za kipekee wanazokuwa nazo majagina wengine duniani, hasa wa kidini. Kwa mfano, Mtume anaapa kulipiza kisasi kwa kuuliwa kinyama kwa mjomba wake Hamzah, lakini Mungu anamshushia aya zinayomwonya kutofanya hivyo. Hili si jambo la kawaida linaloweza kufanyika kwa binadamu wa kawaida. Yeye ni jagina wa Kiisilamu.

Mutiso (1999) anadai kuwa shujaa ni kiumbe wa kweli mwenye sifa za kiajabu na ambaye amekuzwa na wanajamii pamoja na kwamba yeye mwenyewe amejikuza. Naye Gaster (1987) anaeleza shujaa kuwa ni mtu anayemiliki uwezo zaidi kuliko mtu wa kawaida na atumiaye uwezo huu kiujasiri. Ni mtu aliye tayari kuhatarisha maisha yake kwa manufaa ya wengine. Kwa mujibu wa maelezo haya, shujaa, hasa wa kijamii au kihistoria ni mtu jasiri na mkubwa wa mwili, yaani asiyeonekana kama binadamu wa kawaida. Kinyume na haya, shujaa wa kidini kwa kawaida huwa kimaumbile ni mtu wa kawaida, mnyenyekevu na mpole kama anavyosawiriwa Mtume Muhammad ambaye ni shujaa wa dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Katika dini ya Kikristo, Yesu Kristo (Nabii Issa) ana sifa sawa na za Mtume Muhammad. Tofauti ya mashujaa hawa wawili wa kidini na binadamu wa kawaida ni kwamba wao ni mitume wa Mungu na wana sifa za kipekee na za kimiujiza tofauti na binadamu wa kawaida.

Kwa kawaida, mashujaa huwa ni wa kiume japo kunao wa kike, kuna mashujaa wa kidini na pia wa kijamii. Mashujaa wa kidini ni kama vile Mtume Muhammad wa Kiislamu, Yesu Kristo wa Kikristo na Buddha wa jamii ya Wahindi. Kunao wengine katika jamii kama anavyowataja Gichamba (2005). Hawa ni pamoja na Fumo Liyongo wa Waswahili, Sakawa wa Wagusii, Luanda Magere wa Wajaluo, Dedan Kimathi kutoka jamii ya Wagikuyu miongoni mwa wengine. Majagina wa kike ni kama vile Syokimau wa Wakamba na Mekatilili wa Menza wa Wagiriama. Majagina hawa wana sifa zinazokaribiana ambazo tunaweza kusema ni bia na ambazo huwa ni za kipekee. Shujaa tunayemshughulikia ni Mtume Muhammad ambaye ni shujaa wa kidini. Tunachunguza jinsi ushujaa wake unavyojitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* na jinsi mtunzi anavyomkuza kama Mtume wa Mungu.

Kuna sifa nyingi za majagina. Tumeziangalia sifa hizo na kama tulivyotangulia kusema, tumemteua Mtume Muhammad ambaye ni shujaa wa dini ya Kiislamu kama mfano bora wa jagina kama anavyokuzwa na mtunzi. Pia tumeweza kutoa mifano ya majagina wengine wa kidini pale ambapo imetubidi kufanya hivyo. Sifa za shujaa huanza kudhihirika kabla ya kuzaliwa kwake ambapo huwa na utabiri wa kuzaliwa na huendelea kuonekana hadi anapokufa. Katika utenzi tunaoushughulikia, japo tumezitaja baadhi ya sifa hizi, kuna zile ambazo hazijitokezi japo Mtume anazo. Hizi ni zile zinazodhihirika kabla ya kuzaliwa, wakati wa kuzaliwa na wakati wa kifo chake. Hii ni kwa sababu utenzi haujumuishi maisha yake yote tangu kuzaliwa hadi kufa kwake, bali unashughulikia sehemu tu ya maisha yake ambapo anahusika kwenye vita vya kidini. Kwenye vita hivi, Mtume ndiye kiongozi na amiri jeshi wa jeshi lake na hapa ndipo baadhi ya sifa za ushujaa wake zinapojidhihirisha. Wapo wahusika wengine kwenye utenzi ambao wameonyesha ushujaa, lakini katika kazi yetu, tumemteua Mtume pekee kama shujaa wa dini ya Kiislamu.

## 2.3 Sifa za Mtume Muhammad kama Shujaa

Mtume Muhammad, kama shujaa wa dini ya Kiislamu, ana sifa ambazo kila jagina huwa nazo. Kwa kiasi kikubwa, kwa kuwa yeye si binadamu wa kawaida, sifa zake ni za kipekee kwani ni Mtume wa Mungu. Kama asemavyo Wa Mberia (1989), majagina wanatambuliwa kwa sifa zao za kiuhalisia ajabu, ambazo Mtume anazo. Kuna sifa nyingi za ushujaa wa Mtume zinazojidhihirisha katika utenzi huu. Hizi ni pamoja na kwamba:

### 2.3.1 Shujaa huwa na Majina au Sifa Nzuri

Aghalabu, jina la shujaa huwa ni lenye sifa nzuri. Jina hili huakisi hulka na matendo au tabia zake. Hupewa lakabu mbalimbali kutegemea jamii na pia umuhimu wake katika jamii husika. Mutiso (1999) anasama kuwa jagina anapewa jina hili pindi tu anapozaliwa. Yamkini apewe jina la muda na wazazi baada ya kuzaliwa, hadi kufikia pale ambapo ataweza kujitambulisha na kujipa jina mwenyewe. Katika utenzi tunaoushughulikia, Mtume kama shujaa amepewa majina ya sifa nzuri kama vile Tumwa, kwamba ndiye aliyetumwa na Mungu ulimwenguni kwa watu wake (ubeti 17), Kipamba, kwamba ana sura nzuri na ya kupendeza (19), Saburi, kwamba Mtume ni mwenye subira (20), Kipendwa/Kipenzi, kwamba anapendwa na watu wengi (23), Habiba, anayependwa (18), Nabia, kuwa yeye ndiye Nabii wa Mungu (441), Mtenga,

anayetenganisha mazuri na mabaya (438), Taji, Nuru, Badiru-l-Kamali, kuwa ndiye mwanga uletao nuru duniani (25), Rasuli, Mtume/nabii wa Mungu (177) miongoni mwa mengine. Haya ni majina yanayoonyesha ukuu na upekee wa Mtume Muhammad, na yamehusishwa na tabia zake na kazi alizokuja kuzifanya katika jamii. Mutiso (1999) ameorodhesha mifano ya majina ya majagina wa kijamii wenye majina ya sifa zao. Hawa ni kama vile Achillesi (nguvu), Orkoiyot (Mwenye nguvu), Musa (aliyeokotwa). Tukimwangalia shujaa Yesu Kristo kwenye Biblia, amepewa majina kama vile Nuru ya ulimwengu, Njia ya Uzima, Mwokozi, Emanueli, Uzima, Mzabibu wa kweli, Simba wa Yuda, Mshauri wa Ajabu, miongoni mwa mengine. Majina haya yanalingana na majukumu aliyo nayo katika jamii ya Wakristo.

### 2.3.2 Shujaa Anapendwa Sana na Wanajamii

Kwa kawaida, shujaa huwa ni mwokozi au mkombozi wa wanajamii. Hivyo, huwa wote wanampenda sana na huwa na matarajio makubwa kutoka kwake. Mtume Muhammad anapendwa sana na wanajamii na kama vile mtunzi anavyomsawiri, yeye ni kipenzi cha watu:

20. Muhammadi anapendwa
Apendeshwalo kapenda
Aswalo hakulitenda
Jambo lililobatili

18. Zendee na masahaba
Zidhihibu na akraba
Na wafuata habiba
Wote humo zinazili

Armstrong (2007:36) anasema kwamba Muhammad alipendwa sana Makka, alikuwa mtanashati, mwenye urefu wa wastani, nywele na ndevu zilizojikunja vizuri na alikuwa na tabasamu la kupendeza. Alifanya kila jambo kwa moyo wa kujitolea na alikuwa na ujasiri mwingi.

### 2.3.3 Shujaa Aghalabu huwa Mwanamume

Ingawa kuna mashujaa wa kike kama tulivyotangulia kusema, majagina hasa huwa ni wanaume. Hawa ndio huwa na sifa zote za ujagina tangu kutabiriwa kwa kuzaliwa kwao hadi kufa kwao. Mashujaa wa kike, japo wana baadhi ya sifa, baadhi yao hawana sifa hasa za utabiri wa kuzaliwa na miujiza wakati wa kuzaliwa. Sanasana huwa na sifa sawa na za binadamu wa kawaida. Pia, hawana matendo mengi ya

kishujaa kama walivyo mashujaa wanaume. Mashujaa waliopo wa kidini ni pamoja na Mtume Muhammad, Yesu Kristo na Buddha miongoni mwa wengine. Katika mada yetu, tunayemzungumzia ni Mtume Muhammad ambaye ni mwanaume.

### 2.3.4 Shujaa huwa na Maadui/Wapinzani Wengi

Njogu na Chimera (1999) wanasema mahali ambapo majagina huwa wema na hujishughulisha sana katika kupigania haki za kila mtu na hasa wanyonge, wakinzani wao (majahili) hawajali sana maslahi ya watu wengine. Aghalabu, huwa ni wakandamizaji na makatili wenye kuelemezwa zaidi na ubinafsi. Wakati mwingine, jagina hana mkinzani na hupambana na kundi zima la watu waovu au hata taifa zima ovu. Shujaa anaweza kushinda au akashindwa. Katika Vita vya Uhud, Waislamu wakiongozwa na Mtume Muhammad hatimaye wanashindwa. Shujaa yeyote yule huwa na wapinzani au watu wanaomwonea wivu kutokana na ufanisi wake na pia kwa kuwa anapendwa na watu wengi.

Anavyosema Mutiso (1999), lengo la kuwepo kwa shujaa ni kuikomboa jamii kutokana na maadui. Hivyo, ni lazima adui awepo ili shujaa awepo. Shujaa hujitokeza na sifa za kipekee tofauti na adui au wapinzani wake. Maadui, kama anavyosema mtaalamu huyu, ni muhimu katika kuendeleza au kuwafafanua mashujaa. Adui au wapinzani wakubwa wa Muhammad ni Makureshi ambao wanamchukia sana na kuipinga dini ya Kiislamu. Hata wengine wanaapa hadharani kwamba wangemwangamiza baada ya kuwashinda kwenye vita viliyotangulia vya Badr. Wanaahidi kutoa zawadi ya ngamia mia moja kwa yeyote atakayempata Mtume katika hali yoyote ile. Ajabu ni kwamba, hawa ni watu waliokuwa karibu sana kwa Mtume kabla ya kuanzisha dini ya Uislamu.

61. Nani ataempata
Muhammadi kumleta
Japokuwa chake kitwa
Pasi na kiwiliwili

62. Amlete yeyote
Kwa uzima au maiti
Tumejaalia sote
Kupma mia jamali

Pia, Makureshi wana uhasama na chuki kubwa sana mioyoni mwao dhidi ya Mtume baada ya kushindwa katika vita vya Badr, ndipo wanapanga vita kisiri dhidi yake baada ya mwaka mmoja (ubeti 74). Ubayyi bin Khalifu alimchukia sana Mtume.

Anapogundua kwamba Rasuli hajafa, anamkabili kwa hasira na kusema aachiwe amwue ili autulize moyo wake uliojaa chuki na hasira.

423. Na huku anabaini
Ali juu farasini
Niacheni niacheni
Na nimuue Rasuli

424. Nacheni siku ya leo
Niupoze wangu moyo
Na ili mimi na huyo
Tufikiane wawili

Tukilinganisha Mtume Muhammad na Yesu katika Biblia, tutapata kwamba hata yeye (Yesu) pia alichukiwa sana na Wayahudi ambao walimsulubisha na hatimaye kumwua. Haya ni kulingana na dini ya Kikristo ila Waislamu wanaamini kwamba Yesu hakufa kwani aliomba Mungu amwepushe na mabaya, ambayo aliyaita *kikombe* (Marko 14:36). Kwa mujibu wa Kurani Sura 4 Aya 158: *Kwa kusema kwao, hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, wala hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini hawakumwua.*

### 2.3.5 Kusalitiwa kwa Shujaa

Miongoni mwa wanajamii anamozuka shujaa, kuna watu ambao ni wasaliti. Shujaa anaweza kusalitiwa na watu walio karibu naye sana. Anaweza kusalitiwa katika harakati za maisha yake au pia akasalitiwa ili auawe. Mtume Muhammad anasalitiwa na wanajeshi wake mia tatu pamoja na kiongozi wao anaposali. Wanajeshi hawa ni miongoni mwa wale wanajeshi wa mtume elfu moja wanaojiandaa kwenda kupigana na Makureshi wakiongozwa na Abdallah bin Ubayyi.

177. Hajesha Sali Nabia
Jeshi lilimkimbia
La watu theletha mia
Likamuacha Rasuli

178. Mumule ndani ya sala
Waliondoka ghafla
Wakamuacha Rasula
Palepale anasali

Shujaa wa Kikristo, Yesu Kristo, naye alisalitiwa na mmoja wa mitume wake. Samsoni ambaye pia ni shujaa katika Biblia, anasalitiwa na mkewe Delila aliyemwamini na kumwambia siri za nguvu zake (Waamuzi 16:1-21).

Wale walenga mishale wanaowekwa na Mtume kulinda mlima wanamsaliti kwa kutofuata maagizo yake kwamba wasiondoke mahali hapo mlimani hadi pale watakapopata taarifa kutoka kwake. Badala yake, wanapoona wenzao wameshinda na wanawafuata Makureshi na kuokota ngawira, walikimbia na kujiunga nao na kuacha mahali pao pa ulinzi. Jambo hili linasababisha kushindwa kwa Waislamu kama tutakavyoona baadaye (ubeti 287- 296).

### 2.3.6 Shujaa ana Uwezo wa Kung'amua au Kutabiri

Shujaa huwa na uwezo wa kutabiri mambo ambayo yatakuja kutokea hatimaye. Hali hii huwasaidia kukwepa maadui na mitego yao, jambo linalowafanya waweze kuishi hadi pale watakapotekeleza jukumu lao kikamilifu katika jamii. Kulingana na mada yetu, Mtume ana uwezo wa kujua mambo yatakayotokea, yanayopangwa na pia anao uwezo wa kutabiri. Muhammad anasawiriwa na mtunzi kama mtu mwenye ufasaha mwingi.

24. Tena ali na nasaha
Na ulimi ni fasaha
Na akinena mzaha
kwake huthibiti kweli

Mtunzi anaeleza Muhammad kama aliyeweza kujua siri:

147. Muhammadi mkhubiri
Ali mjuzi wa siri
Alipopata habari
Kureshi hawako mbali

Mtume anajua kwamba Ubayyi ni mnafiki na kwamba angemsaliti pamoja na kundi lake, ila akajitia kutofahamu (ubeti 188- 191). Hali kadhalika, aliweza kutabiri ya kwamba yeye mwenyewe ndiye angemwua Ubayyi. Kwamba, kumwua Ubayyi kwa kijambia ni kutimia kwa utabiri wa Mtume huko Sarifu ambapo Ubayyi anapowalisha farasi wake, anamwona Mtume akitembea nje ya mji wa Makka na kumwonya kwamba asitoke tena, kwani angefanya hivyo angemwua. Mtume anamjibu kwamba ni yeye angemwua akiwa amempanda farasi wake (ubeti 492- 500).

499. Kampa tumwa Rasua
Ataibudi takuwa
Mimi ndo wa kukuua
Uli juu ya haili

Utabiri huu ulikuja kutimia wakati wa vita vya Uhud Mtume anapomchoma Ubayyi shingoni kwa kijambia na baadaye akafa akielekea Makka. Anapochomwa, anakiri kwamba Mtume alikuwa keshamwambia hivyo awali.

479. Nae kanipa ahadi
Kunambia Muhammadi
Kuwa atanihusudi
Mimi atanikutuli

**2.3.7 Shujaa huwa Gwiji Vitani**

Kwa kawaida, shujaa haogopi. Huwa jasiri na stadi wa kupigana ili kuikomboa jamii yake. Mtunzi anamsawiri Mtume Muhammad kama hodari na shujaa vitani. Anapopata habari kwamba Makureshi wanamvamia, hatikisika bali alinakusanya wanajeshi walio hodari sana vitani hadi wakapewa jina "panga kali" kutokana na uhodari wao (ubeti 15-155). Anawapanga katika makundi ambapo wapiga mishale hamsini wangeshika doria mlimani. Wale wengine mia sita hamsini wanaanza vita na Makureshi ambapo katika awamu ya kwanza Waislamu wanawashinda Makureshi (ubeti198, 236- 288). Wakati wa vita vya Badr, Mtume aliwashinda Makureshi (ubeti 70- 71).

70. Makureshi walishindwa
Wasiwe la kutenda
Wakirudi kama ng'onda
Kwa hali ya idhilali

Vita vya Uhud ndivyo vilikuwa vikuu zaidi ambavyo Mtume aliwahi kupigana, ambavyo ni vita vitakatifu (ubeti 86- 87). Mtume anapogundua kuwa wale askari mia tatù wametoroka na akabaki na wapiganaji mia saba dhidi ya Makureshi zaidi ya elfu tatu, hafadhaiki wala kukata tamaa, bali anabaki kuwa imara, kuonyesha kuwa ni shujaa vitani, anayejiamini na kuliamini jeshi lake. Pia, anapojitokeza kumkabili Ubayyi, hana ala zozote za kivita ila kile kijambia alichomwomba mmoja wa maswahaba wake. Anawataka wamwache akapigane peke yake. Hili pia ni dhihirisho la ushujaa wake, kwamba hahitaji msaada wa yeyote.

436. Hapa Tumwa kabaini
Kuwambia jitengeni
Peke yangu niacheni
Sitaki mtu wa pili

437. Masahaba waambiwe
Kuwa nisiingiliwe
Mniacheni mwenyewe
Baada hiyo kauli

### 2.3.8 Maisha ya Shujaa na Matendo yake huwa ya Kimiujiza

Mashujaa hujipambanua na binadamu wengine kutokana na uwezo wao wa kutenda miujiza. Mtume Muhammad, katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, anatenda kitendo ambacho ni cha kimiujiza. Ubayyi anapogundua kuwa Rasuli hajafa, anajihami na kwenda mlimani kumkabili. Anavalia nguo za kivita na kuufunika mwili wake wote isibaki nafasi yoyote ila sehemu ndogo sana iliyobaki sehemu ya shingoni (ubeti 420). Mtume naye anavalia kivita na kumuomba mmoja wa maswahaba wake kijambia. Anawaambia wanajeshi wamwache apigane peke yake. Wanapokabiliana, Mtume anamchoma Ubayyi kwa kile kijambia ile sehemu aliyokuwa ameiacha wazi.

442. Kampiga kwa utungo
Si jumla ya maungo
Alimchoma shingo
Ndipo penye afadhali

Mtunzi anaendelea kueleza ya kwamba uchungu aliouhisi Ubayyi haungemithilika wala kuvumilika. Anamgeuza farasi wake na kutoroka akilia, "ameniua Rasuli." Ubayyi anasema kwamba uchungu anaouhisi si wa kawaida na kama ungegawiwa kila mtu ulimwenguni, wake, waume na watoto, bado kila mtu angeupata na upitishwe kwa watu wote wa ulimwengu ujao.

472. Waama, uchungu wake
Huo mkwaruzo
Naona upeke yake
Siuonipo mithali

478. Kila mtu angepata
Walimwengu wote hata
Na baada ya kupata
Wote wangetanakali

Tendo hili ni la kimiujiza. Linaweza likalinganishwa na tendo la watu wawili kwenye Biblia: Daudi na Goliathi, ambapo kijana mdogo Daudi aliweza kumwua Goliathi kwa kutumia jiwe la kombeo. Goliathi kama Ubayyi, alikuwa amevalia nguo za kivita na kujifunika mwili mzima. Nafasi iliyoachwa wazi ni sehemu ya paji la uso ambapo jiwe alilotupa Daudi lilipenya na kumwua (1 Samueli 17). Daudi, kama Mtume Muhammad, ndiye shujaa katika makabiliano haya. Pia uchungu anaouzungumzia Ubayyi si uchungu wa kawaida anaoweza kuuhisi binadamu wa kawaida. Ni wa kimiujiza.

### 2.3.9 Maisha ya Shujaa ni ya Dhiki Tupu

Shujaa kwenye jamii huwa na wajibu wa kuitetea na kuikomboa jamii husika. Jambo hili humfanya shujaa awe na maadui wengi, achukiwe, atengwe; jambo linaloweza kumfanya ahame kutoka kwao na kuishi ugenini au uhamishoni, kutaka kuuawa na maadui, kusalitiwa na kadhalika. Haya yote husababisha dhiki kuu na ukiwa katika maisha ya jagina.

Wanajamii humchukulia shujaa kama mkombozi wao asiyeshindwa, hivyo huwa hana budi kupitia kwenye dhiki hizi ili kuwakomboa. Muhammad, katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, anateseka sana wakati wa vita maadui wake wanapotaka kumwua. Ameumizwa na ana majeraha yenye uchungu mwingi. Mawe anayolengwa nayo na maadui yanampasua usoni na kumng'oa meno licha ya kuwa na ulinzi kutoka kwa maswahaba wake. Kwa misingi hii, Mtume anapitia mateso na dhiki chungu nzima.

Tunaweza kumfananisha Mtume Muhammad na shujaa wa Kikristo, Yesu Kristo kwani naye pia alipitia dhiki kama hizi. Aliposhikwa baada ya kusalitiwa, askari wa Kirumi walimpiga, wakamtesa, wakambebesha jisalaba na hatimaye kumwangika na kumwua.

### 2.3.10 Shujaa huwa na Wafuasi

Gichamba (2005) anasema kwamba aghalabu, mashujaa huwa na wafuasi wao ambao huandamana nao katika maisha yao yote. Wafuasi hawa waweza kuwa watu, mnyama au ala fulani ambayo humsaidia katika utekelezaji wa dhamira yake ambayo ni kuikomboa jamii. Wafuasi hawa pia humkamilisha shujaa na huwa na uwezo wa kipekee. Huwa waaminifu zaidi kwa shujaa wao. Mtume Muhammad ana maswahaba wa karibu sana ambao hawamwachi wakati wa vita. Mtume anapoanguka shimoni,

Talha na Ali Abu Talibu, maswahaba wake, wanafika hapo mara moja kumtoa (ubeti 383- 387).

Pia, bintiye Mtume, Binti Fatima na wanawake wengine kama vile Aisha (Esha) na Batuli wanampenda sana mtume na wako naye wakati anapoumizwa.

Katika dini ya Kikristo, Yesu (Nabii Issa) pia ana wafuasi wake. Hawa ni wale mitume kumi na wawili ambao wanaambatana naye kila wakati kumsaidia katika kazi zake. Pia katika Agano la kale kwenye Biblia, Musa ana fimbo ambayo anaitumia kutenda miujiza kama vile kucharaza jiwe likatoa maji huko jangwani (Kutoka17:1-7), fimbo yenyewe kugeuka kuwa nyoka huko Misri (Kutoka 7:8-12) miongoni mwa mingine.

### 2.3.11 Shujaa Huhusishwa na Zaidi ya Jamii yake

Shujaa hachukuliwi kuwa mwana wa familia au jamii fulani. Ukombozi, ambao ndio dhamira yake kuu, hauhusishwi na jamii moja tu. Mashujaa wa kidini kama walivyo Muhammad, Yesu na Buddha walikuja kuokoa watu wa jamii zote ulimwenguni kote licha ya kwamba, walizaliwa katika jamii moja mahsusi. Waislamu kote duniani humtambua Muhammad kama shujaa wao, kama alivyo Yesu kwa Wakristo wote na Buddha kwa Wahindi wote kote duniani, wala si kwa jamii walimoibuka mashujaa hawa. Katika utenzi tunaoushughulikia, Muhammad anahusishwa na zaidi ya jamii yake kama inavyodhihirika katika ubeti wa 17, 18, 386, 387 na 528 miongoni mwa nyingine ambapo mtunzi anazungumzia ukoo wa Mtume na watu walio na uhusiano naye pamoja na maswahaba wake.

### 2.3.12 Mapenzi ya Mama kwa Shujaa

Shujaa, kama binadamu yeyote yule wa kawaida, huzaliwa na mama ambaye kwa kawaida huwa na mapenzi sana kwa mwanawe. Kwa hivyo, kuna mapenzi ya dhati kati ya mama na mwanawe jagina. Kutokana na kuwa karibu sana na mwanawe, mama huwa mfariji wake wakati wa shida na dhiki. Kama tulivyotangulia kusema, maisha ya shujaa huwa ya dhiki nyingi. Wakati wa kuchukiwa, kutengwa, kudharauliwa, kusalitiwa na hata kuumizwa, mama mzazi huwa mfariji wa mwanawe. Hata hivyo, katika utenzi tunaoushughulikia, mama mzazi wa Mtume hajatajwa, ila aliyetajwa ni bintiye, Binti Fatima, mwanawe Khadija. Mtume Muhammad anampenda sana bintiye huyu ambaye alilakabiwa 'Ummu abuha' (Mama wa

babake). Anapomwona babake ameumizwa sana, alimwendea, akamvua nguo zake zilizokuwa zimechanika, akazichoma na kuchukua jivu lake, akampaka usoni kwenye majeraha ili amtibu. Hili ni tendo na pia dhihirisho la mapenzi.

642 Nae Seyyidina Fatima
Pale pale kakwima
Akamgusa vitema
Hapo binti Rasuli

645. Katika vidonda vyake
Viliyo usoni mwake
Na vyote vibandike
Asipate mahali

Tendo hili linaashiria mapenzi na huruma za binti kwa baba yake. Vile vile, kuna wanawake wengine kama vile Aisha (Esha) na Batule ambao wanampenda Mtume sana, lakini hawangeweza kutenda tendo hili la ushujaa lililotendwa na bintiye, japo Esha ni mkewe Mtume. Hii inaonyesha kwamba Mtume na bintiye wana uhusiano wa karibu sana. Katika Biblia, Mariamu, mamake Yesu shujaa wa Kikristo, aliandamana na mwanawe tangu alipokamatwa hadi pale alipokufa msalabani.

### 2.3.13 Shujaa huwa Mpole na Msamehevu

Mtume Muhammad anasawiriwa kama jagina mpole na msamehevu. Anawasamehe Makureshi wanaomwua mjomba wake Hamzah kinyama. Kisha akawasamehe wale wanajeshi mia tatu waliotoroka wakati wa swala kabla ya vita. Halikadhalika, anawasamehe wale waliotoroka wakati wa vita waliposikia kwamba Mtume alikuwa ameuawa. Anawasamehe baada ya aya ya Kurani kushuka ikimwonya kuwa jukumu lake halikuwa kulipiza kisasi bali kusamehe (ubeti 717). Hii ni baada ya kuapa kwamba angewachinja Makureshi sabini kutokana na kifo cha baba yake mdogo Hamzah ambaye alimpenda sana.

### 2.3.14 Shujaa Hutokana na Jamii Bora au ya Kifalme

Inachukuliwa kwamba, shujaa hutokana na ukoo uliochaguliwa na Mungu. Hii ni kwa sababu shujaa huwa ameteuliwa ili kuiokoa au kuikomboa jamii. Mutiso (1999) anadai kwamba kuzaliwa kwa jagina huwa kumebashiriwa, na kama hakujabashiriwa, ushujaa wake unathibitika anapozaliwa. Anaendelea kusema kwamba atakayezaliwa, kulingana na utabiri, hutokana na ukoo wa kifalme kama vile ukoo wa Daudi, Gandhi, Sakya, Kureshi na kadhalika. Anaendelea kusema kuwa Nabii Issa alitokana na ukoo

wa Daudi, Mtume Muhammad alitokana na kabila la Kureshi, ukoo wa Banu Hasham, Guatama Buddha alitokana na ukoo ulioitwa Sakya, ambao unaaminika kuwa ulitokana na mayai ambayo yaliaguliwa na jua. Kulingana na Allen (1993), shujaa wa kijamii Fumo Liyongo alitokana na ukoo bora na akapewa jukumu la kuongoza jamii ya Waswahili wa Pate. Mringwari (wa kwanza), baba yake Liyongo, alikuwa Sultani wa taifa la Pate.

Armstrong (2007) anasema ya kwamba Muhammad alizaliwa katika ukoo wa Banu Hashim uliokuwa mmojawapo wa familia zilizojulikana huko Makka. Babu yake alikuwa mfanyibiashara mtajika, aliyefanya biashara zake hadi Syria na Yemen, na ukoo wake ndio uliowapa maji mahujaji na wasafiri wakati wa hija.

### 2.3.15 Kugura/Kuhama kwa Shujaa

Aghalabu, shujaa hutoroka kwao na kuhamia ugenini ambapo anaweza kuishi asirudi kwao, au arudi baada ya muda. Kuhama huku hutokana na uhasama wa mahasimu wao ambao sanasana huwa ni viongozi au watawala wa nchi zao. Huwa wanahofia kuwa mashujaa hawa, ambao huwa na uwezo usio wa kawaida, wanaweza kuzipindua serikali zao. Safari ya shujaa huwa ya muhimu sana kwa sababu humtayarisha kutekeleza majukumu yake katika jamii. Safari hii, kama anavyosema Mutiso (1999:31), huweza kuwa ya kiwakati, kimahali, kifikira au hata ikawa ya kisaikolojia. Katika safari ya kisaikolojia, shujaa huzinduka kutokana na elimu au mawazo mapya anayoyapata na baadaye huwafunza wafuasi wake, jambo ambalo linabadilisha mfumo wa jamii. Shujaa anapohama na kwenda katika nchi au sehemu nyingine, hupata mazingira tofauti na ya nyumbani, hivyo huwa na mtazamo mwingine.

Mtume Muhammad anahama kutoka Makka na kwenda Medina kutokana na uhasama wa Makureshi wanaotaka kumwangamiza kwa kusimamia dini ya Kiislamu. Mtume harudi nyumbani kama wafanyavyo mashujaa wengi. Vita vinapoisha, Mtunzi anasema kuwa Mtume alirudi Medina pamoja na masahaba wake.

731. Baada ya hapo tena
Kashika njia Amina
Wakarejea Medina
Asahabu na Rasuli

Tukimwangazia Yesu Kristo shujaa wa Kikristo, tunaona kwamba pia naye alihama japo akiwa mdogo. Mfalme wa wakati wake, mfalme Herode, alipoambiwa kuhusu kuzaliwa kwake alifadhaika sana kwani aliona kuwa shujaa huyu aliyezaliwa na kusifiwa na watu wote angemnyang'anya mamlaka pindi awapo mkubwa. Katika Biblia, kulingana na kitabu cha Mathayo 2 :13, malaika wa Mungu alimtokea Yusufu babake Yesu kwenye ndoto na kumwambia amchukue mtoto na mamake Mariamu na watorokee Misri kwa kuwa Herode alikuwa akimtafuta amwue. Waliagizwa wakaishi huko hadi malaika atakapowaambia. Tofauti na Mtume Muhammad, Yesu alirudishwa Nazareti baada ya kifo cha mfalme Herode.

Shujaa huwa na sifa nyingi na kama tulivyotangulia kusema, utenzi tunaoushughulikia unahusika tu na sehemu ya maisha ya Mtume Muhammad, hivyo sifa zote hazijajumuishwa. Hata hivyo, tumezitaja baadhi hata kama hazipo kwenye utenzi.

### 2.3.16 Utabiri na Miujiza Kabla na Baada ya Kuzaliwa

Mutiso (2005) anasema ya kwamba mitume na manabii wa Mwenyezi Mungu waliomtangulia Mtume Muhammad walibashiri na kuhubiri juu yake kwa umma; wao walihubiri habari njema kwamba Mtume atakuja. Alipozaliwa jumba la mfalme wa Kiajemi liliyumba na mito kukauka. Anaendelea kusema kuwa hii ni ishara ya ushindi wa Uislamu juu ya dini nyingine duniani.

Syed (1922:8-9) anasema kwamba kuzaliwa kwa Mtume kulikuwa na ubashiri ambao mataifa yote ya ulimwengu yalijua kwamba Mwokozi/Mkombozi amewasili. Tukimwangalia Nabii Issa (Yesu) kama shujaa wa Kikristo, kuzaliwa kwake pia kulitabiriwa na Nabii Isaya (Isaya 9:6-7). Pia Malaika Jibrili alimshukia mamake Mariamu usingizini na kumwambia kwamba angemzaa mtoto wa kiume atakayeuokoa ulimwengu (Luka 1:26-38). Mama mzazi wa shujaa hupitia dhiki nyingi kabla na wakati wa kuzaliwa kwa shujaa. Anaweza kumzalia mtoto katika mazingira duni sana kama alivyozaliwa nabii Issa kwenye hori la ng'ombe baada ya wazazi wake kusafiri kutoka Nazareth hadi Bethlehem walipokosa chumba cha wageni.

### 2.3.17 Mama wa Shujaa aghalabu huwa Mnyonge au Maskini na Baba huwa Hajulikani

Mama wa shujaa huweza kuwa mke wa pili au akawa suria. Pia baba huwa hajulikani na kama anajulikana huwa si wa manufaa yoyote katika maisha ya shujaa. Kwa mfano, babake mtume Muhammad aliaga mtoto akiwa bado hajazaliwa, hivyo hajulikani na wengi. Armstrong (2007) anasema kwamba babake Mohammad, Abdullah, aliaga kabla ya Mtume kuzaliwa na mama yake Amina alikuwa katika hali ya kusikitisha kiasi cha kwamba, mwanamke aliyekuja kumsaidia wakati wa kujifungua alitoka katika mojawapo ya familia maskini kabisa huko Uarabuni. Muhammadi aliishi na mwanamke huyo hadi alipotimu umri wa miaka sita, na alikuwa akiishi maisha ya ufugaji. Mama yake alifariki muda mfupi baada ya Muhammadi kurudishwa Makka; alipoishi na babu yake Abd ul- Mutttalib, naye akafariki Muhammad akiwa na umri wa miaka minane.

Syed (1922:8) naye anasema kwamba Abdallah, babake Mtume alikufa safarini akielekea Yathrib (Madina) akiwa na umri wa miaka ishirina na mitano, na baada ya siku chache, mkewe Amina, aliyekuwa amedhoofika na kuteseka sana akamzaa mtoto wa kiume aliyemwita Muhammad. Hii ilikuwa tarehe 12, Rabbiul awal, mwaka wa Ndovu. (Tarehe 29, Agosti 570). Margoliouth (2003:46) naye anasema kwamba Mtume ambaye miaka yake ya kwanza minane ya maisha yake aliyoishi na Abdul al Muttalib, aliishi kama mtoto yatima asiyekuwa na baba, hali ambayo ilisikitisha na haikupendeza sana.

Kwa upande wa Yesu, Mariamu mamake alitoka katika jamii isiyojulikana sana huko Nazareti, naye babake Yusufu, japo ametajwa, hakuwa na manufaa kwa mwanawe. Licha ya kuwa hakuwa babake mzazi, hakuna lolote linalojulikana kumhusu baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Historia inathibitisha kwamba, katika Biblia, Yusufu ametajwa mara chache sana na hajazungumza lolote la maana kwa mwanawe Yesu.

### 2.3.18 Maisha ya Ujana wa Shujaa Hayajulikani kwa Uwazi

Mengi hayajulikani kuhusu ujana wa majagina kama ilivyo kwa vijana wengine. Baada ya kuzaliwa kwa jagina, machache hujitokeza, hasa hadi akiwa na umri wa miaka kumi hivi, kisha anaibuka na vitendo vya kishujaa akiwa mtu mzima. Tukimwangalia Mtume Muhammad, ambaye ndiye shujaa tunayemshughulikia katika mada yetu, tunaona kwamba baada ya kuzaliwa, anatajwa hadi pale ana umri wa

miaka minane, kisha akiwa mtu mzima kuanzia akiwa na umri wa miaka ishirini na mitano anapomwoa Khadija. Tunalolifahamu kumhusu hasa ni kwamba katika ujana wake, alikuwa akiwalisha kondoo wa ami yake ambaye alikuwa mlezi wake.

Armstrong (2007:15) anasema kwamba hakuna lolote linalojulikana kuhusu maisha ya awali (ya ujana) ya Muhammad hadi pale anapoanza kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu akiwa na umri wa miaka arobaini. Pia, ni machache sana yanayojulikana kuhusu maisha yake alipokuwa Makka.

Syed (1922:11) naye anaeleza ya kwamba Muhammad alikaa kwa ami yake aliyekuwa mlezi wake katika biashara zake huko Syria. Akiwa yatima, aliishi maisha ya upweke yenye mawazo mengi akilini. Hivi ndivyo alivyokua tangu utotoni hadi akawa mtu mzima mwenye umri wa miaka ishirini na mitano, alipomwoa Khadija, Mkureshi mwenzake aliyekuwa na umri wa miaka arobaini.

Katika Biblia, baada ya kuzaliwa kwa Yesu, anatajwa tena akiwa na umri wa miaka kumi na miwili alipoenda hekaluni na wazazi wake na baada ya hapo, anatajwa tena akiwa na miaka thelathini anapoanza huduma yake duniani, kisha anaishi kwa miaka mingine mitatu zaidi halafu anakufa.

### 2.3.19 Shujaa na Swala la Ndoa

Shujaa haoi, na akioa familia haiwi na manufaa yoyote kwake kwani jukumu lake kuu ni kuikomboa jamii wala si kutunza familia. Ukweli huu ndio unaoibua sifa nyingine kwamba, shujaa harithiwi na wanawe kwa kuwa hawapo. Katika swala la ndoa, mashujaa wengi waliooa walikuwa na zaidi ya mke mmoja au wakawa na wapenzi wengi. Wanawake hawa ndio wanaochangia vifo vyao ambapo wao ndio huwasaliti kwa wapinzani au maadui zao. Mtume Muhammad, kulingana na *Utenzi wa Vita vya Uhud*, ameoa. Japo hatujaelezwa chochote kuhusu wake zake katika utenzi, jambo hili linadhihirishwa na ukweli kwamba ana binti, Seyyidina Fatima ambaye wakati wa vita alimtibu majeraha yake (ubeti 642). Mamake mtoto huyu ni Bibi Khadija. Katika Biblia, shujaa Samsoni alisalitiwa na kwa maadui zake Wafilisti na mke wake Delila (Waamuzi 16:1-31).

Armstrong (2007:38) anasema ya kwamba Khadija alipokufa, Muhammad alikuwa akiwaimbia wake zake wengine sifa zake (Khadija) nzuri. Hili linadhihirisha kuwa alikuwa na wake wengine. Anaendelea kusema kuwa Khadija alimzalia watoto sita,

wavulana wakafa utotoni, akabaki na wasichana wanne. Mmoja wa wasichana hawa tunamwona kwenye *Utenzi wa Vita vya Uhud*, Bibi Fatima ambaye, wakati wa vita Mtume anapoumizwa sana, anachukua nguo zake zilizochanika, akazichoma na kutumia jivu lake kumtibu babake vidonda. Kufa kwa watoto wavulana wa Mtume nako kunadhihirisha ukweli ya kwamba, shujaa hana warithi. Kwa kawaida, katika jamii nyingi ulimwenguni, warithi wa mtu huwa ni watoto wake wa kiume na tunaona ya kwamba hawa wake walikufa utotoni. Mwandishi huyu anawataja baadhi ya wake wa Mtume (ukurasa 138) ambao ni Khadija, Zaynab, Hafsah, Aisha na Sawdah. Aisha ndiye anayeandamana na Mtume wakati wa vita. Hili ni dhihirisho ya kwamba shujaa huwa na wake wengi.

### 2.3.20 Kifo cha Shujaa

Kifo cha shujaa hakiwi cha kawaida, kwamba, hafi hadi pale anapokutana na jeraha linalosababisha kifo chake. Kifo chake huwa kimetabiriwa na huwa ni cha ajabu. Shujaa anasemekana kwamba hafi. Huwa amepumzika na kisha atarudi kuwachukua watu wake. Hivyo, shujaa hata akifa hasahauliki miongoni mwa jamii. Kwa mfano, katika dini ya Kiislamu, Mtume Muhammad ndiye mwanzilishi wa dini, wafuasi wake wanamkumbuka kila wakati. Hii ina maana kwamba, kazi ya shujaa haiishi pale anapokufa, bali huendelea kizazi baada ya kingine.

Katika dibaji ya Kurani Tukufu, Mirza (1953: vi) anasema: *Nabii aliyeileta Kurani Tukufu katika dunia amekwisha kufa, lakini kuwepo kwake kwa kiroho hii leo kunadhulumiwa zaidi kuliko ilivyokuwa miaka 1,400 kabla, alipokuwa akidhulumiwa katika maisha yake ya kimwili. Yeye anasingiziwa, na mafundisho yake yanaelezwa na yanawekwa mbele ya dunia kwa sura mbaya, ila Mwenyezi Mungu anaona kuwa hayo si haki, kwani Mtakatifu mbele ya Mwenyezi Mungu ni Mtume, ambaye ilimshukia Kurani.* Mtume Muhammad alikufa kutokana na homa na maumivu makali ya kichwa, lakini hajasahaulika katika dini yake. Ndivyo ilivyo katika dini ya Kikristo ambapo mwanzilishi wake, japo alikufa na kuaminiwa kufufuka miaka mingi iliyopita, bado anakumbukwa na wafuasi wa dini hiyo. Baadhi ya vifo vya mashujaa hutokana na kusalitiwa na watu waliowaamini kama wake, watoto wao au watu walio karibu sana nao. Kwa mfano, Yesu katika dini ya Kikristo alisalitiwa na Yudasi, mmoja wa mitume wake. Samsoni naye alisalitiwa na mkewe Delilah. Fumo Liyongo

anauawa na mwanawe baada ya kughilibiwa na Sultani wa Pate. Kifo chenyewe pia huwa kimetabiriwa kama tulivyotangulia kusema.

### 2.4 Maudhui ya Dini Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*

Kwa mujibu wa Kamusi ya karne ya ishirini na moja (2011), dini ni imani inayohusianayna kuwako kwa Mungu au miungu. Dini inayozungumziwa katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* ni ya Kiislamu ambayo mwanzilishi wake ni Mtume Muhammad. Walioasi dini hii ni Makafiri ambao ni Makureshi. Katika vita hivi, Waislamu wanapigana na wasioamini wala kukubaliana na Uislamu. Baadhi ya matukio ni ya kidini au yanayoonyesha imani ya Waislamu. Kulingana na dini ya Kiislamu, vita vya kidini ni vitakatifu na vimeidhinishwa na Allah mwenyewe.

George (2003:3) anatanguliza kwa kunukuu Kurani Tukufu: Kurani 11:126: *Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni cha Kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua, nanyi hamjui.* Anaendelea kusema kwamba (uk 6) wanaopigana kwa ajili ya Allah wameahidiwa paradiso, na kwamba ni baya jeshi linalofukuzwa na adui kuliko lile linalofukuza (Surah IV 74 na 104). Mwandishi huyu anasema kwamba (uk 8) kulingana na Kurani Surah VIII 12-16, Allah atawamaliza wasioamini kupitia kwa askari wake, na kwamba kwa mwanajeshi wa Kiislamu kumkimbia adui ni sawa na kumlaani aende kuzimu. Haya yanadhihirisha ya kwamba kwa mujibu wa dini ya Kiislamu, vita ni vitakatifu na vimeidhinishwa na Allah mwenyewe. Kuna maswala muhimu ya kidini yanayojitokeza katika utenzi huuwa Vita vya Uhud.

#### 2.4.1 Kutanguliza kwa Maombi/ Kumtambua Mungu

Knappert (1967:64-65) anasema ya kwamba, mwanzoni kabla ya chochote kile, Mungu alikuwepo. Jina lake linashirikishwa mwanzoni mwa kila utungo wa Kiswahili na kwamba jina lake linahimidiwa. Anaendelea kusema kuwa beti za mwanzo huwa zinasifu utukufu na upekee wake. Anasema Mungu hakuzaliwa wala kuzaa, anajua lakini hajulikani, anajua yote, anajitosheleza, ni muumba na anaweza yote. Maelezo ya mtaalamu huyu ni ya kweli na yanajitokeza wazi katika *Utenzi wa Vita Vya Uhud* ambapo mtunzi anatanguliza kwa kuutambua upekee na ukuu wa Mungu (ubeti 1-17). Anamshukuru Mungu kwa kumwezesha kutunga. Anamtambua Mungu kwa majina makuu kama vile Mkuu, Mweza, Mtenda haki, Aliyeumbwa

awali, Mpweke, Mwajitenga asiyehitaji msaidizi miongoni mwa mengine. Mungu ndiye pekee wa kuabudiwa kama asemavyo mtunzi.

13. Alwahidu ilahu
    La ilaha ilAlaluhu
    Wa Jalala Jalaluhu
    Allahu Dhulkamali

Mtunzi anamtukuza Allah katika ubeti huo wa 13 kwa kusema: *Wa pekee ni yeye Allah, hakuna Mola ila Allah, na Ametukuka kwa kila Utukufu, Allah ndiye Mkamilifu.*

### 2.4.2 Mtume Muhammad

Katika dini ya Kiisilamu, Mtume Muhammad ni nabii miongoni mwa wengine waliomtangulia lakini ana sifa za kipekee. Mtunzi anampambanua zaidi katika utenzi huu ili kudhihirisha umuhimu na upekee wake katika dini ya Kiislamu. Knappert (1967) anaeleza Mtume Muhammad kama msimamizi, mjumbe wa serikali na mkuu wa sheria. Anamtaja kama mfano wa jua liletalo nuru kwa watu wake. Anaendelea kusema kwamba Muhammad ni mkamilifu, asiye na dosari wala tashwishi, na ambaye ana matendo yaliyo mfano bora kwa Mwislamu, na ambaye kila aliye Mwislamu sharti ayafuate. Nuru ya Mtume ndiyo nyota ya kuwaongoza Waislamu katika maisha na bendera yake ndiyo itawafikisha peponi. Hali ngumu huwepo ili Mtume Muhammad aweze kudhihirisha ukuu wake, naye pia alipitia hali ngumu maishani mwake.

Maelezo haya yanadhihirisha ukuu wa Mtume katika dini ya Kiislamu. Mtunzi, baada ya kutaja ukuu wa Mungu mwanzoni mwa utenzi, anamtambua Muhammad kama Mtume wa Mungu na kumsifu kwa kumpa majina makuu na ya heshima kama vile Tumwa (ubeti 17), Kipamba (19), Saburi (20), Kipendwa (23), Habiba (18), Mtenga (438), Taji, Nuru, Badiru-l-Kamali (25) Rasuli (177), Faridi miongoni mwa mengine. (Maana ya majina haya yametolewa awali katika ukurasa wa 20). Kwa hivyo, Mtume anachukua nafasi kubwa sana kama Nabii wa Mungu na mwanzilishi wa dini ya Kiislamu na pia amiri jeshi wa jeshi la Waislamu katika vita. Kuwepo kwake kwenye utenzi ni dhihirisho tosha kuwa utenzi huu ni wa kidini.

### 2.4.3 Vita Vitakatifu

Mtunzi anaviita vita hivi vita vitakatifu.

87. Na jinale Jihadi
Liitwalo makusudi
Ndivyo vita vya Uhudi
Ambavyo vita vya pili

Jihadi maana yake ni kujitolea kupigana, kwanza kuilinda na dini, na kulinyanyua neno lake Allah na kuhakikisha kuwepo haki na uadilifu katika ardhi, na kama hatua ya mwisho, vita vya silaha vinaweza kuwepo. Katika Kurani Tukufu, neno Jihadi limetumika kumaanisha kujitolea kusimama kidete kulinda dini ya Allah kwa mapambano ya kivita. Vita hivi kwa misingi hii basi ni vita vya kupigania dini ya Mtume, hivyo, ni vita vitakatifu. Kulingana na Kurani Tukufu, Sura 2, aya 190-193, vita vilivyoidhinishwa na Mungu vimekubaliwa. Aya 190 inadhihirisha haya: *Na wapigeni vita katika njia ya Mwenyezi Mungu wale ambao wanakupigeni vita, wala msiruke mipaka, hakika mwenyezi Mungu hawapendi wanaoruka mipaka.* Kulingana na maandiko haya matakatifu, Uislamu unawafundisha Waislamu wawe wenye nguvu ili kujilinda wenyewe, lakini wasiwe wachokozi.

### 2.4.4 Bendera ya Uislamu

Munsabu bin Omar, wa ukoo wa Banu Abdi-Dari, ndiye alichaguliwa na Mtume Muhammad kuongoza jeshi la Waislamu. Alimpatia bendera ya Islamu ambayo haikupaswa kuanguka wakati vita vinapoendelea. Kuanguka kwake na kukosa mtu wa kuichukua kulimaanisha kushindwa na hivyo kuisha kwa vita.

214. Kumtenga Mukhtari
Wa banu Abdi-Dari
Munsabu wa Omari
Sahaba wa Murisali

216. Tumwa alimsalimu
Bendera ya Islamu
Baada hayo fahamu
Wakajipanga rijali

Kwa kawaida, wakati wa vita, jeshi lolote la nchi husika huwa na bendera ya nchi hiyo pamoja na bendera ya jeshi lao. Lakini tunavyoona hapa, jeshi la Islamu lina bendera ya dini yao, ambayo ni dini ya Kiislamu. Hili linadhihirisha ya kwamba vita

hivi vilikuwa vya kidini na kwamba mtunzi ameipa dini nafasi kubwa zaidi kuliko nchi au jeshi lenyewe.

### 2.4.5 Kusilimu kwa Makureshi

Baada ya vita, baadhi ya Makureshi wanasilimu na kujiunga na dini ya Mtume Muhammad, wakawa wafuasi wake.

135. Walikuwa maarufu
Na kwa Tumwa msharafu,
Wakawa ni wapendefu
Wapoacha ujahili

Margoliouth (2003:336) pia anasema kwamba waliofurahishwa na kufaulu kwa Mtume walijiunga naye, akiwemo Abbas bin Mirdas, mwana wa mtunga shairi Al-Khansa anayejulikana sana katika ukoo wa Sulaim.

### 2.4.6 Kupigana Vita Siku ya Ijumaa

Mtunzi anatueleza kwamba Mtume aliamua kwenda vitani siku ya Ijumaa. Hii ndiyo siku ya sala kubwa kwa Waislamu. Pia ni mwezi wa Shawali, ni mwezi wa kwanza baada ya mfungo wa Ramadhan kwa Waislamu. Kama tulivyotangulia kusema, vita vinatokea katika awamu kadhaa ambapo Waislamu wanawashinda Makureshi nguvu katika baadhi yazo. Hivyo kwa maoni yetu, kule kupigana vita siku ya Ijumaa na ukweli kwamba ni wakati wa mfungo ndiko kunachangia pakubwa ushindi huu. Waislamu ni wachache (mia saba) dhidi ya Makureshi elfu tatu. Huu si ushindi wa kawaida bali wanangozwa na Mungu. Pia vita vinapokamilika, Mtume anarudi Madina siku ya Ijumaa. Margoliouth (2003) anasema ya kwamba, baada ya vita kukamilika, Muhammad alirudi Medina siku ya Ijumaa, ambayo ni siku muhimu sana kwa Waislamu.

### 2.4.7 Maombi Kabla ya Vita

Kuomba ni kufanya sala kwa Mola ili kutafuta msaada wake. Waumini wa dini yoyote ile hushiriki kwenye maombi. Hii ni njia ya kuonyesha imani na matumaini kwa Mungu. Usiku wa Ijumaa, wanapofika mlimani Uhud kabla ya vita, Mtume na jeshi lake wanaenda kusali (ubeti 173-174). Tendo hili linaonyesha kuwa wanamtumainia Mungu katika vita. Ikumbukwe ya kwamba Mtume hana na ufahamu wa awali kwamba Makureshi wangemvamia. Kwa hivyo, anapopata habari hiyo, anawakusanya wapiganaji elfu moja na wakaenda vitani wala hawana na wakati wa

kujitayarisha. Ni dhihirisho kwamba wanamtumainia Mungu na wana imani kwa Mungu zaidi kuliko idadi ya wapiganaji na silaha walizo nazo. Ni wakati huu wa sala ambapo Abdallah bin Ubayyi, aliyekuwa Mwislamu mnafiki, (ubeti 178-187) na lile kundi la waasi mia tatu walitoporoka. Mwislamu anayeidhamini dini yake hawezi kufanya haya au kuisaliti.

### 2.4.8 Kujibiwa kwa Maombi na Usamehevu wa Mtume

Mtume anaumizwa sana na Makureshi wakati wa vita. Anapasuliwa uso kwa mawe na kung'olewa meno. Pia ami wake, Bwana Hamzah, anauawa kwa kukatwakatwa vipande vipande. Kutokana na jambo hili, maswahaba wake wanamwambia awalaani waliotenda kitendo hiki, lakini anakataa na kusema kuwa Mungu hakumtuma kulaani, bali kuwaombea viumbe rehema zake. Japo mwanzoni alikuwa ameapa kulipiza kisasi (ubeti 712-714), Mungu anazungumza naye na anamteremshia aya inayomwonya kwamba hapaswi kulipiza kisasi.

717. Mkitesa siteseni
Kama mvyoteswa nanyi
Mkiongeza wa thani
Mkitia fadhili

Aya inayomshukia kuhusu kusamehe inapatikana katika Kurani Tukufu Sura ya 16, Aya ya 127: *Na mkilipiza, basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanaosubiri.*

Anapopokea aya hii, Mtume anavunja kiapo chake na kuazimia kuwa hatolipiza kisasi tena. Pia, anawaombea maadui zake kwa Mungu ili wapate watoto na awalinde wawe watu imara maishani. Anapomaliza dua hii, Allah anamjibu. Maadui zake hatimaye wanawazaa watoto waliosimamia Uislamu kwa dhati. Mmoja wao ni mjukuu wa yule askari aliyemlenga Mtume usoni na kumvunja meno wakati wa vita, ambaye hatimaye alikuja kuwa Immamu wa Sunni.

559. Naomba siku ya leo,
Ndani ya watu hao
Katika migongo yao
Uwatoe aftali

568. Maimamu wa Kisuni,
Ni mjukuwe yakini
Alompiga usoni
Siku huyo Murisali

Jambo hili linaonyesha kuwa Mtume ana imani kubwa kwa Mungu, msamehevu, mwenye upendo licha ya kusalitiwa na watu wake, na anayeijali dini yake zaidi zaidi kuliko kuwachukulia wapinzani wake kama maadui. Kwa hakika, kama Mtume wa Mungu na shujaa, Muhammad ana sifa hizi.

### 2.4.9 Kushuka/Kuteremka kwa Wahyi/Aya za Kurani

Tulivyotangulia kusema, ami wa Mtume, Bwana Hamzah, alikuwa ameuliwa kinyama kwa kukatwakatwa sehemu za mwili wake. Mtume anaapa kulipiza kisasi kwa kuwaangamiza Makureshi sabini kutokana na mauaji haya.

712. Kusema hapo Kipendwa,
Makureshi hawashinda
Sina budi kuwatinda
Ni sabiini kamili

714. Tawakata watu hao
Kwa baba mdogo huyo
Kwa walivyomkatao
Nitwae kwao badali

Mungu anampa wahyi ulio kwenye Kurani Tukufu Sura ya 16 aya ya 127 kama ilivyo kwenye ubeti wa 712 na kama tulivyoonyesha, ambapo Mungu anamwonya dhidi ya kulipiza kisasi. Anapopata aya hii, anaghairi kulipiza kisasi. Pia, zinamshukia aya za kuwasamehe wale waliokimbia wanaposikia kuwa ameuawa na pia wale wanajeshi mia tatu wanaomtoroka wakati wa sala kabla ya vita.

726.Tena siku ile ile
Nazo aya zilishuka
Za kuwasamehe wale
Wakimbiao rijali

Halikadhalika, zinamshukia aya za kuonyesha kushindwa kwao wakati wa vita, ambako kunatokana na kutotii amri ya Mtume.

729. Ndipo aya zikajiri
Kushinda hii safari
Kwa kuiacha amri
Ya Mtume Musirali

Armstrong (2007:17) anasema ya kwamba Muhammad alipokea aya kutoka kwa Mungu, ambayo ndiyo iliwekwa pamoja na kuwa Kurani, ingawa ilimshukia mstari baada ya mstari, sura baada ya sura. Ni katika mistari hii ambapo Mungu anajibu maombi ya Mtume kuhusu

wapinzani wake. Anaendelea kueleza kuwa jinsi mistari ilivyomshukia Mtume, ndivyo Waislamu walivyoielewa mioyoni mwao, na waliojua kuandika wakaiandika. Hivyo, Kurani iliandikwa baada ya Mtume kufariki.

Tunaweza kusema kuwa licha ya kuwa amiri jeshi wa Waislamu, Muhammad ni Mtume halisi wa Mungu kwani anaweza kuzungumza naye na kumshushia aya ambayo inapatikana katika Kurani, kitabu kitakatifu cha dini ya Kiislamu ambayo Mtume mwenyewe ndiye mwanzilishi. Hivyo, baadhi ya matukio yanayojitokeza katika utenzi huu ni ya kidini.

### 2.4.10 Mashahidi wa Kiislamu

Kuna Waislamu wengi wanaouawa wakati wa vita hivi. Mtunzi anawaita Mashahidi ambao ni watu waliokufa wakipigania imani yao na ambao wanakumbukwa kama mashujaa wa kidini katika dini ya Kiislamu. (ubeti 692-697). Margoliouth (2003:305) anasema ya kwamba mashahidi waliokufa katika vita vitakatifu hawajafa bali wanaishi na kufurahia furaha ambayo haijakamilika kwa sababu ndugu zao ambao hawajafa hawajajiunga nao. Anaendelea kusema kwamba vita haviwezi kuwepo bila dini nayo dini haiwezi kuwepo bila vita. Haya ndiyo yanayosababisha historia katika Uislamu.

Maudhui ya dini yanajitokeza wazi katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Kutokana na maudhui haya, ni dhahiri kuwa Mwislamu halisi anapaswa kuwa mtiifu kwa kufuata maagizo ya Mtume, wakuu wa dini au viongozi wake, la sivyo atapatwa na maafa kama yalivyowafika Waislamu wakati wa vita vya Uhud kutokana na kutotii amri ya Mtume alipowaambia wale walenga mishale hamsini aliowaagiza kutotoka mlimani lakini hawakufuata amri.

## 2.5 Maudhui ya Vita na Mauaji

Vita ni mapigano ya silaha baina ya watu, makabila nchi, mataifa au wanyama. Vita vinavyozungumziwa katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* ni vita vya kidini kati ya Waislamu na Makureshi. Makureshi ni makafiri wanaoipinga na kuichukia sana dini ya Islamu. Kama tulivyosema awali, vita hivi vinafanyika kwenye mlima wa Uhud ambavyo ni vya kulipiza kisasi (ubeti 87,88). Kwenye vita vilivyotangulia vya Badr, Waislamu wanawashinda nguvu Makureshi, jambo ambalo linawakera sana Makureshi ambao, chini ya uongozi wa Abu Sufiyyani, wanapanga vita vya kulipiza

kisasi dhidi ya Waislamu. Wanapanga vita kwa siri kwa muda wa mwaka mmoja (ubeti 70,74,97). Abu Sufiyyani anatayarisha jeshi la askari elfu tatu. Wakuu wa wapiganaji hawa wanaandamana na wake zao ambao jukumu lao ni kuwapa motisha wakati wa vita kwa kuwakariria mashairi na kuwapigia vigoma. Wanaamini ya kwamba mwanamume hawezi kukimbia vita wakati mke wake, au mwanamke yeyote anamwona. Wanaliona jambo hili kama la aibu na kudhalilisha sana. Kwa hivyo, kuwepo kwa wanawake hawa kunadhamiriwa kuwaweka waume zao vitani hata vikiwa vikali namna gani.

119. Na kwa kila mkadamu
Kaja na wake harumu
Ili amtie hamu
Ni mbele ya makatili

124. Kwa kuiogopa aya
Nani muweza kimbia
Na hapo watabakia
Zautaji na baali.

Muhammad hana ufahamu kuwa Makureshi wako tayari kumvamia, lakini anapojua tu anaandaa jeshi la wapiganaji hodari elfu moja wanaoitwa 'panga kali' kutokana na ushujaa wao na wakaondoka kuelekea vitani. Kama tulivyosema awali, wakati wa sala kabla ya vita askari mia tatu wanamtoroka Mtume, lakini ameweza kupigana vita na wale mia saba waliobaki.

Huu ni utenzi ambao kwa jumla unazungumzia vita baina ya Waislamu na Makureshi ambao ni makafiri. Ni vita vilivyokuwa katika mlima wa Uhud. Ukali wa vita hivi umedhihirika wazi.

Kuhusu vita vya Badr, Armstrong (2007:32) anasema ya kwamba, vita vyenyewe vilikuwa katika mwezi wa Ramadhani (Machi) 624, ambapo Muhammad aliongoza jeshi la Waislamu 314 kutoka Madina kwenda kushambulia msafara wa Makureshi ulioongozwa na Abu Sufiyyani. Katika vita hivi, Waislamu waliwashinda Makureshi. Kuhusu vita vya Uhud, mwandishi huyu anasema kuwa mnamo Machi 11 625, wanajeshi wa Makureshi elfu tatu, ngamia elfu tatu na farasi mia mbili walitoka Makka kuelekea Medina kwa vita kwenye mlima wa Uhud. Waliambatana na mke wa Sufiyyan, Hindi, pamoja na wanawake wengine wake za majemedari waliowafuata

Makureshi kuwaimbia nyimbo za vita na kuwapigia ngoma. Haya yamedhihirika katika utenzi tunaoushughulikia.

Syed (1922:63) naye anaeleza kwamba Waislamu wanaamini ya kwamba walishinda kwa sababu malaika waliwasaidia.

### 2.5.1 Mtume kama Amiri Jeshi wa Waislamu

Mtume ndiye amiri jeshi wa jeshi la vita vya Waislamu ana jeshi la jumla ya wapiganaji elfu moja.

151. Ili hao walokifu
Jumla watu alfu
Ambao wasio hofu
Wasio shaka mahali

Kwa upande wa Makureshi, kiongozi wao, Abu Suffiyani, ana jumla ya wapiganaji elfu tatu (ubeti 103). Mtume Muhammad, licha ya kuwa kiongozi wa jeshi la Islamu, anahusika katika makabiliano ya vita ambapo anavalia kivita na kukabiliana na Ubayyi na kumwua (ubeti 433).

### 2.5.2 Ukali wa Vita

Vita baina ya Makureshi na Waislamu ni vikali sana. Katika awamu ya kwanza, mtunzi anavifananisha vita hivi na zilizala ambapo Makureshi wanashindwa nguvu na Waislamu na kukimbia.

235. Wa baada hayo tena
Wa Makka na wa Madina
Hapo wakakamatana
Ikawa kizilizali

Waislamu wanawafuata Makureshi nyuma. Wale walenga mishale hamsini mtume aliokuwa amewaweka kushika doria mlimani wanapoona wenzao wameshinda, wanaiacha sehemu yao ya ulinzi na kujiunga nao kuokota ngawira. Jambo hili la kutotii kwa Waislamu ndilo lililosababisha kushindwa kwao mwishoni mwa vita. Knappert (1967:170) anasema kwamba, Mwislamu mwema hapaswi kutamani sana dhahabu na anasa za dunia. Mali ya vitani inapaswa kuokotwa na kupewa wajane na watoto mayatima ambao watu wao wamekufa kwenye vita vitakatifu. Kulingana na maoni ya mtaalamu huyu, waliyofanya Waislamu yalikuwa ni makosa makubwa sana na kama tulivyosema, jambo hili ndilo lilisababisha kushindwa kwao.

### 2.5.3 Vifo

Munsabu bin Omar, Mwislamu anayefanana sana na Mtume, anauawa katika vita hivi (ubeti 339). Makureshi wanapofahamu kwamba siye Mtume aliyeuawa, wanaghadhabika sana na kuapa kumwua. Ubayyi bin Khalifu, shujaa wa kivita wa Makureshi, anaapa kummaliza Mtume, anampanda farasi wake na kuapa kwenda kummaliza. Mtume, anaposikia kwamba Ubayyi anataka kukabiliana naye, anavalia kivita na kuomba kijambia kutoka kwa mmoja wa masahaba wake na kutoka akakabiliane naye. Anamchoma shingoni na baadaye akafa akielekea Makka (ubeti 441,482) mahali panapoitwa Sarifu. Ni mahali hapa ambapo Mtume alitabiri kwamba angemwua Ubayyi.

Bwana Hamzah, ambaye ni baba mdogo wa Mtume, anauawa vitani kwa kukatwakatwa kinyama. Mauaji yake ndiyo yanayomfanya Mtume aape kulipiza kisasi kwa sababu anampenda sana ami wake (ubeti 702,713). Kwa jumla, kulingana na mtunzi Waislamu wanaouawa ni sabini na wanne nao Makureshi wakafa ishirini na watatu.

690. Maiti wao wenzetu
Wafileo si wa kwetu
Ishirini na watatu
Wafileo majahili

694. Watu waliowaona
Hao walopatikana
Aroba u sabiina
Wali hao ukitali

Margoliouth (2003:300-302) naye anasema ya kwamba waliouawa katika vita hivi walikuwa Waislamu sabini na Makureshi ishirini na wawili. Baadhi ya Waislamu walikuwa wameumizwa akiwemo amiri jeshi wao, Mtume Muhammad.

Kwa jumla, utenzi wote tunaoushughulikia unahusu vita baina ya Makureshi na Waislamu, kama mada ya utenzi inavyoashiria. Kama inavyodhihirika, vita vyenyewe vimetokea katika awamu kadhaa ambapo katika awamu ya kwanza, makabiliano makali kati ya jeshi la Mtume na Makureshi yanatokea na Makureshi wanashindwa. Katika awamu ya pili, waislamu waliokuwa wamewekwa na Mtume kushika doria mlimani wanakimbia wanapoona wenzao wameshinda na kujiunga nao kuokota ngawira. Makureshi wanachukua nafasi hii na kuwashambulia Waislamu kutoka mlimani, sehemu ambayo walikuwa wameiacha bila ulinzi. Waislamu wanashindwa

nguvu kwani wamevamiwa bila kutarajia. Ni katika awamu hii ambapo Munsabu bin Omar, Mwislamu aliyefanana sana na Mtume anauawa.

Awamu ya tatu ya vita inazuka Makureshi wanapogundua kwamba waliyemwua hakuwa Mtume, bali Munsabu aliyefanana naye. Jambo hili linawakera sana na wakaamua kummaliza Mtume. Ubayyi bin Khalifu, aliyekuwa adui mkubwa wa Mtume na dini yake, anaapa kumwangamiza. Mtume anakabiliana naye na kumchoma shingoni kwa kijambia alichoomba kutoka kwa mmoja wa maswahaba wake. Kutokana na jeraha hili, Ubayyi anakufa njiani akielekea Makka, mahali panapoitwa Sarifu. Kifo cha Ubayyi kinasababisha awamu ya nne ya vita. Makureshi wanaapa kumwua Mtume kwa vyovyote vile. Ni katika vita hivi ambapo Mtume anaumizwa sana kwa kupigwa mawe na maadui zake. Hili ni kwa sababu hawangeweza kumfikia kwa silaha kama vile panga na mikuki kutokana na ulinzi alio nao wa wafuasi wake. Kwenye vita hivi, kama tulivyosema awali, Makureshi waliwashinda Waislamu. Jumla ya Makureshi wanaouawa walikuwa ishirini na watatu, nao Waislamu wakafa sabini na wanne. Waislamu wengine wengi waliumizwa vibaya sana, akiwemo Mtume Muhammad.

**2.6 Hitimisho**

Katika sura hii, tumechanganua maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad, dini, vita na mauaji. Maudhui haya yamejitokeza wazi katika utenzi. Ni maudhui yanayooana na kuingiliana katika utenzi huu kiasi cha kwamba hakuna moja linaloweza kujitokeza bila kuhusishwa na jingine. Dini ya Kiislamu inahusiana sana na vita na ndio maana wanaviita vita vitakatifu. Wanaamini ya kwamba vita vilihalalishwa na Allah mwenyewe.

Pia, kulingana na utenzi na pia imani ya dini ya Kiislamu, wanaokufa katika vita vya kupigania au kutetea dini ni mashahidi ambao bado hawajafa. Ni dhahiri kuwa vita haviwezi kuwepo bila dini na dini haiwezi kuwepo bila vita.

# SURA YA TATU

# WAHUSIKA NA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*

## 3.0 Utangulizi

Katika fasihi, wahusika ni viumbe vinavyoumbwa na mwandishi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Wahusika wanaweza wakawa watu, mimea, miungu, wanyama, wadudu, majitu au mazimwi, vivuli kwenye mawazo, vibonzo, na kadhalika. Katika baadhi ya tenzi, wahusika huwa ni watu wa kawaida ambao huwa mashujaa wa dini au katika jamii. Kwenye *Utenzi wa Vita vya Uhud*, mtunzi amewatumia wahusika ambao ni binadamu wa kawaida ambao wamemfaa katika kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa hadhira yake. Katika sura hii, tumeangazia jinsi mtunzi alivyowatumia wahusika katika uendelezaji wa maudhui yake. Tumefafanua dhana ya wahusika jinsi ilivyo katika fasihi na kuonyesha aina mbalimbali za wahusika na kueleza sifa zao. Pia, tumeshughulikikia wahusika mbalimbali wa kibinafsi na wa makundi. Tumeonyesha jinsi wanavyochimuza maudhui mbalimbali katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

## 3.1 Dhana ya Wahusika

Wataalam wametoa fasiri mbalimbali za dhana ya wahusika. Dhana hii kwa maoni yetu, inabeba wazo moja kuu kwamba, wahusika ni viumbe vya kisanii ambavyo wasanii wenyewe wameviumba. Vinaakisi sifa na tabia za watu fulani katika maisha ya jamii halisia. Wahusika huwa wanawakilisha watu wenye tabia na mienendo tofauti tofauti katika jamii. Tutawataja baadhi ya wataalam hawa.

Forster (1927) amewagawa wahusika katika makundi mawili: wahusika duara na wahusika bapa. Kulingana na mtaalam huyu, wahusika bapa ni wale wanaokazania wazo fulani tangu mwanzo hadi mwisho na wanaonyeshwa upande mmoja tu wa sifa zao. Wahusika duara, kulingana na Foster ni wale ambao, kwa kiasi kikubwa wanakaribiana na binadamu wa kawaida katika kazi ya fasihi, ila mara nyingine huenda sifa zake zisiakisi za binadamu wa kawaida. Hili hutokea pale ambapo mhusika duara ana sifa za ki-uhalisiaajabu. Aina zote mbili za wahusika zinajidhihirisha katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Mohamed (1995) anasema kuwa mshairi huwa ni mtungaji shairi na mhusika vyote wakati mmoja. Ingawa mhusika huyu haonekani kusimama waziwazi juu ya kurasa za shairi, anajificha nyuma ya mwandishi. Hivyo, wahusika ni viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi. Wahusika huhusika na matendo na matukio kadha katika kazi hiyo. Hupatikana katika tamthilia, riwaya na hadithi fupi na wakati mwingine katika mashairi simulizi kama vile tenzi. Mshairi huyu amewagawa wahusika katika makundi matatu yafuatayo: wahusika vinyago, bapa na mviringo/duara.

Katika utenzi tunaoushughulikia, mtunzi amewatumia wahusika halisi japo kawaumba mawazoni mwake. Wahusika hawa wamechotwa kutoka katika jamii husika ili kuendeleza maudhui aliyodhamiria mtunzi. Hivyo, madai ya Mohamed (kama hapo juu) kwamba wahusika ni viumbe vya mawazoni mwa mtunzi, tunayathibitisha kwani kama tulivyosema awali, mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* amewatumia binadamu halisi wa jamii yake, akiwemo Mtume Muhammad kuwasilisha maudhui na kuendeleza dhamira yake. Si katika utenzi huu pekee ambapo wahusika wa aina hii wametumiwa, bali kwenye kazi nyingine za kifasihi.

Njogu na Chimerah (1999) nao wanasema ya kuwa, wahusika ni sehemu ya fani wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Msanii huwaweka wahusika wake katika mandhari yatakayomsaidia kuwasilisha hoja zake kutokana na vitendo, maingiliano na fikra zao. Wamewagawa wahusika katika makundi yafuatayo: wahusika wakwezi, wa kisaikolojia, wa kimapinduzi, jumui, wasaidizi, wakuu, wajenzi, wa miraba minne, wa mraba mmoja, duara, shinda na wahusika bapa. Ni kweli kuwa wahusika hubuniwa kutokana na mazingira ya msanii, kwa hivyo tunaafikiana na maoni ya mwandishi wetu. Hii ni kwa sababu tukirejelea utenzi tunaoushughulikia, wahusika waliopo ni wa dini ya Kiislamu ambayo ndiyo dini ya mtunzi. Pia kuna wahusika ambao wanaipinga dini yenyewe ambao ni makafiri, nao wanapatikana katika mazingira yayo hayo. Mtunzi ametumia makundi haya mawili kuendeleza maudhui yake ya vita vya kidini, mauaji na ushujaa wa Mtume Muhammad. Utenzi unahusu vita vya kidini (jihadi) ambavyo vinapiganiwa jangwani, kwenye mlima wa Uhud. Haya ni maudhari yanayofaa kwa vita kulingana na maoni ya mwandishi huyu.

Mbatiah (2001) anasema kuwa wahusika ni watu tunaokutana nao katika kazi ya kifasihi na ambao kutokana na matendo na mazungumzo yao, wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika. Amewagawa katika kategoria tano ambazo ni: wahusika bapa, duara, dufu, wasaidizi na wahusika wakuu. Tunakubaliana na mawazo ya Mbatiah, lakini kwa maoni yetu, maelezo yake yamepuuza ukweli kwamba, wahusika wa kifasihi huakisi watu katika ulimwengu halisi wanamoishi kama inavyodhihirika katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

Amata na King'ei (2001) wanasema kuwa wahusika ni viumbe, vitu au watendi wanaotumiwa na mshairi kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Anaendelea kusema kuwa uchambuzi wa mashairi yanayotumia wahusika kama vyombo vya kuwasilisha ujumbe yanapaswa kutilia maanani sifa, tabia na taswira ya wahusika wanaorejelewa katika kusawiri matukio ya shairi na kushadidia maudhui na dhamira ya shairi. Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kwani tukirejelea utenzi huu, mtunzi amewatumia wahusika wake kikamilifu kuuwasilisha ujumbe wake kama tutakavyoona baadaye. Udhaifu wao ni kwamba hawajawagawa wahusika katika makundi yoyote au aina zozote. Wahusika katika kazi yoyote ya kifasihi hawawezi kuwa sawa, wa jumla au wakawa na jukumu moja pekee.

Wamitila (2003) naye anasema kuwa mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida. Mtaalam huyu amewaainisha wahusika katika kategoria kumi na sita ambapo anasema kuwa kuna wahusika akisi, bapa, bapa sugu, bapa kielelezo, batili, duara, ghibu, jumui, kipokeo, kani, mchomozi msaidizi, foili, msimulizi, shinda na wahusika wakuu. Maoni yetu ni kwamba katika kategoria hizi zilizoainishwa na mtaalam huyu, sifa za wahusika wote zimekaribiana sana kiasi cha kwamba baina ya baadhi yazo, hakuna tofauti dhahiri. Hili ni jambo linaloweza kuzua utata kwa mtafiti. Tofauti zinazojitokeza dhahiri ni kati ya kategoria nne ambazo ni kategoria ya wahusika wasaidizi, wahusika wakuu, wahusika bapa na wahusika duara.

Katika tasnifu yake, Kofa (2009) anasema kuwa wahusika ni viumbe vinavyoumbwa na msanii na matendo yao hufanana na matendo ya binadamu. Baadhi ya wahusika hupewa nafasi ya kutenda na mtunzi, kusema, kujiwasilisha na kuitambulisha kwa hadhira. Wanapofanya hivyo, hadhira hupata fursa ya kuwajua na kuwahukumu. Kusawirika kwao hutegemea malengo ya msanii. Watunzi wengine huchagua viumbe visivyo binadamu ili waifumbe hadhira kama ilivyo kwenye riwaya ya *Shamba la Wanyama* (1967) ya George Orwell. Tunakubaliana na maoni haya.

Gatakaa (2012) naye anadai kwamba, wahusika ni viumbe au watendi wanaotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Hutumiwa katika ujenzi na upelekaji mbele wa maudhui. Tunaafikiana na maoni haya kwa sababu yanakubaliana na utenzi tunaoshughulikia ambapo mtunzi, Haji Chum, amechagua wahusika binadamu ambao wanaendeleza maudhui yake. Udhaifu wa mawazo haya ni kwamba, mwandishi hajaeleza endapo wahusika wanapaswa kuchotwa kutoka katika jamii ya msanii ili kuendeleza maudhui yake kama ilivyo katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.*

### 3.2 Aina za Wahusika

Kama tulivyodokeza hapo mwanzo, kuna aina nyingi sana za wahusika kama zilivyoonyeshwa na wataalam mbalimbali. Katika somo letu, hatutachunguza aina zote, bali tumechagua chache tu ambazo tumeona kuwa zitakuwa za manufaa kwetu.

#### 3.2.1 Mhusika Mkuu

Huyu ni mhusika anayeitawala kazi ya fasihi tangu mwanzo hadi mwisho. Huwa kiini cha kazi husika ya fasihi. Hujitokeza waziwazi kuwa ndiye nguzo ya masimulizi kwani ndiye muhimu kuliko wahusika wengine. Matukio yote muhimu katika hadithi humzunguka yeye. Wahusika wengine wanahusishwa naye na wanasaidia katika kumjenga yeye. Kazi moja ya fasihi inaweza kuwa wahusika wakuu kadhaa ambao wanabeba kiini cha dhamira na maudhui ya kazi husika. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*, kuna wahusika wakuu kadhaa akiwepo Mtume Muhammad, Munsabu, Ubayyi na Sufiyani. Tenzi zingine zilizo na wahusika wakuu zaidi ya mmoja ni kama vile *Utenzi wa Adbdirrahmani na Suffiyyani* ambapo wahusika wakuu ni Abdirrahmani, Sufiyyani na Binti Sufiyani. Kwenye *Utenzi wa Ayub*, kuna Ayub na Ibilisi ambao ndio wahusika wakuu.

### 3.2.2 Mhusika Msaidizi

Pia hujulikana kama mhusika mdogo. Humsaidia mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi, kwamba huwa anahusiana kwa karibu na mhusika mkuu na humjenga. Hachukui nafasi kubwa katika kazi ya fasihi lakini hutumiwa kusaidia katika ujenzi wa maudhui na sifa za mhusika mkuu. Huweza kuwa wengi katika kazi ya fasihi au wakawa katika makundi. Mhusika msaidizi aghalabu anapotekeleza nia ya mtunzi, huuliwa au akapotea asitajwe tena. Katika *Utenzi wa Vita Vya Uhud,* baadhi ya wahusika wasaidizi wanajitokeza katika makundi. Kuna wanawake kumi na watano ambao ni wake za majemedari wa jeshi la Makureshi wanaojitokeza na kuandamana nao wakati wa vita wakiwaimbia mashairi na kupiga vigoma, kuna wafuasi/maswahaba wa Mtume, ukoo wa Banu Abdi-Dari ambao ni washika bendera wakati wa vita, askari mia tatu waliotoroka wakati wa sala kabla ya vita, wanawake Waislamu, jeshi la Makureshi na jeshi la Waislamu miongoni mwa mengine.

### 3.2.3 Mhusika Bapa

Huyu ni mhusika ambaye habadiliki. Huwa na sifa mahususi tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Matendo yake ni yale yale, kama ni mabaya au mazuri, yatakuwa vivyo hivyo hadi mwisho wa kazi. Kwa mfano, yupo Mtume Muhammad ambaye ni kielelezo cha dini ya Uislamu katika *Utenzi wa Vita Vya Uhud.* Mhusika bapa huonyeshwa upande mmoja tu. Wahusika bapa wanaweza kugawanywa katika kategoria mbili: bapa kielelezo na bapa sugu. Mhusika bapa sugu ni mhusika anayechukua msimamo sugu au madhubuti ambao anaushikilia katika kazi ya fasihi tokea mwanzo hadi mwisho. Msimamo unaweza kuwa mzuri au mbaya, ambao ndio unaomtambulisha mhusika wa aina hii. Katika utenzi wetu, Sufiyyani na Ubayyi ni makafiri wanaoshikilia msimamo wao wa kuipinga dini ya Mtume hadi mwisho. Munsabu naye ni Mwislamu anayeipigania dini yake. Mhusika bapa kielelezo kwa upande mwingine ni mhusika ambaye, japo habadiliki kitabia, hana msimamo kama alivyo mhusika bapa au sugu. (Katika fasihi ya Kiswahili, Shaabab Robert anafahamika kuwa gwiji wa kuwasawiri wahusika wa aina hii ambao pia ndio wanaopatikana zaidi katika fasihi simulizi). Sifa nyingine ya mhusika huyu ni kwamba yeye hupewa jina linaloakisi tabia yake, yaani matumizi ya mbinu ya majazi. Mhusika bapa kielelezo pia huwa na sifa nzuri ambazo huchukuliwa kuwa kielelezo au kitu cha kuigwa na wanajamii. Kwa mfano, binti Fatima na wanawake Waislamu, maswahaba wa Mtume Muhammad wanaonyesha mfano bora wa maadili katika

jamii. Wanamshughulikia Mtume Muhammad anapoumizwa na Makureshi vitani. Akina mama pia ni kielelezo cha mapenzi na uvumilivu katika jamii.

### 3.2.4 Mhusika Duara

Ni mhusika anayebadilika badilika kitabia kila mara kulingana na mazingira anamojipata. Kubadilika huku kwa tabia ndiko humfanya aonekane kuwa na sifa zinazokaribiana na za binadamu wa kawaida/halisi. Tabia hii ya kubadilika ni njia ya kuonyesha uhalisi wa kijamii kwani ndiyo hupatikana katika binadamu. Mhusika duara ni kinyume cha mhusika bapa. Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* baadhi ya majemedari wa Kikureshi wanasilimu (Ubeti 132-133). Hawa ni wahusika duara kama tutakavyoona baadaye.

## 3.3. Wahusika na Uendelezaji wa Maudhui

Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* kuna makundi mawili muhimu, kuna kundi la Waislamu na kundi la Makureshi. Katika makundi haya, mtunzi amehusisha wahusika wengi sana. Kwa misingi hii, tumewagawa katika makundi mawili: wahusika wa makundi na wahusika binafsi. Hii ni kwa sababu wahusika wengi, hasa tuliowaweka katika makundi wana sifa sawa, wanatekeleza majukumu sawa na wanaendeleza maudhui yale yale mamoja. Wahusika tunaowashughulikia kibinafsi ni kama vile Mtume Muhammad ambaye ndiye mhusika mkuu, Ubayyi, Munsabu, miongoni mwa wengine. Katika makundi, tunaangazia kundi la Waislamu, la Makureshi, wanawake Waislamu miongoni mwa wengine.

### 3.3.1 Wahusika wa Makundi

Makundi yote tunayoyashughulikia ni ya wahusika wasidizi wanaoendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad, ya dini, vita na mauaji.

#### 3.3.1.1 Jeshi la Waislamu

Hili ni jeshi la Mtume Muhammed lenye wapiganaji elfu moja. Mtunzi anawapa jina "panga kali" kutokana na weledi wao kwenye vita. Ni kundi la wanaume watiifu kwa Mtume na wako tayari kuandamana naye vitani kukabiliana na Makureshi licha ya kwamba, hawajapewa muda wa kujitayarisha dhidi ya jeshi la Makureshi lililo na wapiganaji wengi sana (Ubeti 155-157). Mtume hana habari kwamba Makureshi wamgemvamia na hivyo, hayuko tayari kwa vita. Pindi anapopata habari kwamba wamewasili, anakusanya jeshi la wapiganaji elfu moja harakaharaka na wanajihami kwenda kupigana na Makureshi elfu tatu. Japo kikosi cha wapiganaji mia tatu

wanatoroka wakati wa sala kabla ya vita, Mtume na waliobaki mia saba hawafi moyo, wanaendelea kujitayarisha. Baada ya Mtume kuwaweka walenga mishale hamsini juu ya mlima kushika doria chini ya uongozi wa Abdallah Khubeir (ubeti 199-102), wanaobaki mia sita na hamsini wakiongizwa na Munsabu bin Omar (ubeti 214) wanaingia kwenye uwanja wa vita kukabiliana na Makureshi.

Kundi hili linaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammed na ya vita. Tunafahamu kwamba, jeshi la Waislamu limebaki na wapiganaji mia sita na hamsini baada ya kundi la askari mia tatu kutoroka na hamsini kuwekwa mlimani kushika doria. Licha ya idadi yao chache dhidi ya Makureshi elfu tatu, wanawashinda nguvu katika awamu ya kwanza ya vita.

275. Wakenda mbio wenyewe
Ja kukumwakona mwewe
Ila wakatawanyika
Kwa kuona idhilahi

276 Wakenda mbio wenyewe
Kwa mauti kuyahofu
Wakakimbia parefu
Jamii wote ahali

Kupitia kwa jeshi hili, ushujaa wa Mtume unadhihirika kwa kuwa jeshi lake, licha ya uchache wao, linalishinda nguvu lile la Makureshi lililo na wapiganaji wengi zaidi ya mara tatu zaidi ya lao, na kulishinda katika awamu ya kwanza ya vita. Vita navyo ni vikali sana na mtunzi anavifananisha na zilizala ambapo watu wengi wanakufa akiwemo mshika bendera wa jeshi la Kiislamu. (ubeti 235-249).

235. Wa baada hayo tena
Wa Makka na wa Madina
Hapo wakakamatana
Ikawa kizizilizala

249. Na wote ndugu watatu
Wa nyumba mojao watatu
Wote wamekwenda kwetu
Imewapata ajali

Waislamu wanaokufa ni sabini na wanne akiwemo Hamzah, babake mdogo wa Mtume aliyekatakatwa kinyama.

694. Watu waliowaona
Hao walopatikana
Aroba u sabiina
Wali hao ukatili

Idadi hii ya wafu inaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Pia inaendeleza maudhui ya dini kwani mtunzi anawaita waliouawa mashahidi ambao mikono na vichwa vyao vimekatwa vikatengwa na viwiliwili vyao. Mashahidi, kulingana na dini, ni wale wanaokufa wakiipigania dini ya Mwenyezi Mungu.

701. Walivyo Shahidi hao
I mbali mikono yao
Vi mbali vichwa vyao
Pamwe na hiyo rijili

**3.3.1.2 Jeshi la Makureshi**

Ni jeshi la makafiri lililo na jumla ya wapiganaji elfu tatu, farasi mia mbili na ngamia elfu tatu (ubeti 136-139). Azma yao kubwa hasa ni kumwangamiza Mtume.

141. Na azima yao hasa
Mtume kumtakasa
Na asiwepo kabisa
Yeye na wake ahali

Viongozi wao ni pamoja na Khalid bin Walid, Amir bin Alyas, Ukrimu bin Abu-Jahili na Sufiani bin Umayya. Hawa ni mashujaa jasiri na maluuni wanaoliongoza jeshi vitani (ubeti 127-130). Mwanzoni, mtunzi anawasawiri kama kundi la waasi linalomchukia Mtume na dini yake. Mwishowe, baadhi yao wanasilimu na kujiunga na dini ya Mtume na kuwa maamiri jeshi maarufu wanaofanya kazi yao kwa ufasaha (ubeti 132-135).

Hawa wanaosilimu ni wahusika duara kwa kuwa wanadhihirisha tabia ya kubadilika. Mwanzoni, wanapinga dini ya Mtume Muhammad na kumchukia sana, kisha baadaye wanasilimu na kujiunga na dini yake na kumtumikia kwa uaminifu. Kwa misingi hii, kundi hili linachimuza ushujaa wa Mtume kama shujaa wa vita kwa kuwa, kusilimu kwao kunachangiwa na kushindwa kwa jeshi lao lililo na askari wengi. Wanamwona Mtume kama shujaa asiyeshindwa. Pia, wanaendeleza maudhui ya kukua na kuimarika kwa dini ya Kiislamu kwa kuwa kuuasi ukafiri na kujiunga na ile ya Mtume kunaonyesha ukuu na upekee wa dini ya Kiislamu, kwamba ndiyo dini bora.

Ni kawaida shujaa kuchukiwa na kuwa na maadui wengi. Makureshi wanamchukia Mtume Muhammad sana na ndio maana wanaapa kumlipa yeyote atakayemleta mtume kwao akiwa hai au mfu, au hata wapeleke kichwa chake, kwamba wangemzawadia ngamia mia moja.

61. Nani ataempata
Muhammadi kumleta
Japokuwa chake kutwa
Pasina kiwiliwili

62. Amletae yeyote
Kwa uzima na mauti
Tumejaalia sote
Kumpa mia jamali

Mtunzi anaendelea kusema kwamba kila siku, Makureshi walitafuta mbinu mpya ya kumpata Muhammad (ubeti 67). Katika ubeti wa 59, mtunzi anasema kwamba tunazijua sababu zilizomfanya Mtume kutoka Makka kwenda Medina. Armstrong (2007:74-75) anazieleza sababu hizi kwamba, Makureshi walimchukia sana Mtume kwa sababu ya dini yake mpya kwao. Walikuwa wamekubaliana na dini ya Kikristo na ya Kiyahudi kwa sababu zilikubaliana na baadhi ya tamaduni zao. Lakini dini ya Kiislamu, ambayo Mtume aliianzisha, waliipinga vikali kwa kuwa ilikuwa na mafunzo tofauti kabisa na yale ya itikadi zao. Uhasama na chuki cha Makureshi kwa Mtume Muhammad zinamlazimisha ahame Makka aelekee Madina. Kwa kawaida, shujaa huwa na maadui na wapinzani wengi. Makureshi wanampinga na kumchukia Muhammad. Hii pia ni moja ya sifa za shujaa kwamba, shujaa huwa na safari ambapo anaweza kwenda ugenini anapokabiliwa na dhiki, shida na upinzani kwao nyumbani.

Makureshi wanaokufa vitani ni ishirini na tatu, nao vilivile wanaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Idadi yao ni chache sana ikilinganishwa naya Waislamu sabini na wanne waliouawa, hivyo Makureshi walishinda katika vita hivi.

690. Maiti wao wenzetu
Wafileo si wa kwetu
Ishirini na watatu
Wafileo majahili

**3.3.1.3 Wanawake Makureshi**

Ni wahusika wasaidizi ambao mtunzi amewatumia kuwakuza na kuwaendeleza wahusika wakuu akiwemo Mtume Muhammad na majemedari wa jeshi la Makureshi. Hawa ni wake za viongozi wa jeshi la Makureshi. Ni jumla ya wanawake kumi na

watano ambao wanaambatana na waume wao vitani ili kuwatia motisha kwa kuwaimbia nyimbo na kupiga matari na vigoma kama ilivyokuwa ada ya enzi hizo.

119. Na kwa kila mkadamu
Kaja na wake harumu
Ili amtie hamu
Ni mbele ya makatili

125. Tena wanawake wano
Wajao kwenye pigano
Nao kumi na watano
Mabibi wa maliwali

Inaaminika kwamba wanaume wakiwa na wake wao hawawezi kuogopa chochote na watapigana ili kuonyesha ushujaa mbele ya wake wao. Lingekuwa jambo la kufedhehesha kama mwanaume angekimbia vita mbele ya mkewe. Kulingana na mtunzi, mwanaume hapaswi kuonyesha woga mbele ya mkewe.

123. Vita vitakapovuma
Watazame kina mama
Na mume harudi nyuma
Hawezi kwenda mahali.

Seyd (2008:69) anasema kuwa Makureshi walielekea kwenye uwanja wa vita wakibeba sanamu za miungu yao, wakiandamana na wake wa viongozi wao huku wakiwaimbia nyimbo za kivita na kupiga matari na vigoma ili kuwatia motisha. Kundi hili linaendeleza maudhui ya ushujaa wa majemedari wa Makureshi kwa kuwa, ni kupitia kwao wanapotia fora vitani wasije wakajifedhehesha kwa kuonyesha woga. Kuwepo kwao kunawatia waume wao moyo waendelee kupigana na Waislamu. Ni kupitia kwao vita vinapochacha, wanalitia jeshi lao moyo kwa kuliimbia. Mtunzi pia amelipa kundi hili la wahusika jukumu la kuyakuza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad kwenye utenzi. Japo wanawatia waume zao motisha, jeshi la Waislamu linaloongozwa na Mtume lina wapiganaji wachache sana na katika awamu kadhaa za vita, linalishinda nguvu lile la Makureshi. Jambo hili linadhihirisha ukweli kwamba shujaa huwa hodari katika vita. Hindi, mke wa Sufiyani, anaendeleza ushujaa wa mume wake. Anajitokeza na kuimba wimbo wa kumsifu mume wake kabla ya sufiyani kuamuru jeshi la Makureshi kuondoka vita vinapomalizika (ubeti 684-687).

### 3.3.1.4 Wanawake Waislamu

Kuna wanawake wengi wanaojitokeza kwenye utenzi ambao wanasawiriwa kama wanaompenda sana Mtume Muhammad. Hawa ndio wanaofika kumwona mtume

pangoni anaposemekana kuwa amekufa. Miongoni mwao ni Seyyidati Esha (mkewe) na Fatima Batuli (bintiye mpendwa) (ubeti 634). Ni mwenye busara, anampenda na hamwachi babake. Mtume anapoumizwa, Fatima anamvua nguo zilizochanika, anazichoma na kumpaka jivu usoni ili kumtibu.

642. Nae Seyyida Fatima
Pale pale alikwima
Akamgusa vitema
Hapo binti Rasuli

645. Katika vidonda vyake
Vilivyo usoni mwake
Na vyote avibandike
Asipasaze mahali

Mtunzi amewatumia wanawake hawa kuendeleza maudhui ya dini. Ni wafuasi wa Mtume wanaompenda sana pamoja na dini yake. Bintiye, Binti Fatima, anaendeleza ushujaa wa Mtume. Anaonyesha mapenzi kwake kwa kumvua nguo, kuzichoma na kumtibu majeraha kwa jivu, jambo ambalo halingefanywa na mwanamke mwingine. Shujaa huwa kipenzi cha mama na humfariji wakati wa dhiki na ndiyo maana tunamwona Bi Esha, mkewe Mtume akiwa naye wakati anapoumizwa na Makureshi.

### 3.3.1.5 Maswahaba wa Mtume

Hawa ni wafuasi wa Mtume wanaomlinda kwa kila njia na namna (ubeti 514-515). Ulinzi wao unachimuza maudhui ya umuhimu wa Mtume Muhammad katika utenzi huu. Makureshi wanaapa kummaliza Mtume wakati shujaa wao Ubayyi bin Khalif anapouawa, lakini wafuasi wake wanamlinda dhidi ya mahasimu hao katika vita ambavyo vinasemekana kuwa havikuwahi kuonekana mfano wake kabla.

517. Hadi masahaba hao
Siku hiyo pigo lao
Jamii maisha yao
Halijaonwa mahali

518. Wapigana ushujaa
Pigo lenye ritifaa
Kubwa lisilo mithaa
Kwa mfano wa dalili

Mtume anapopigwa jiwe na kuzirai, maswahaba wanajipa moyo na kuwafukuza Makureshi (ubeti 508). Wanaendeleza ushujaa wa Mtume kwamba, shujaa huwa na walinzi dhidi ya maadui zake. Munsabu anapouawa, habari zinaenea kwamba Mtume ndiye kauawa. Wakati huo, Mtume ameumizwa na kuanguka shimoni asionekane

kutokana na uchafu uliomo humo (ubeti 379-381). Talha, mmoja wa maswahaba pamoja na binamu yake Ali bin Abu Talib, wanamsaidia na kumtoa shimoni (ubeti 392). Talha pamoja na Ali bin Talib wanawakilisha Waislamu waadilifu. Mtunzi anawatumia kuendeleza ushujaa wa Mtume kwani hao ni wafuasi wake walio na msimamo thabiti tangu mwanzo hadi mwisho. Shujaa kwa kawaida huwa na wafuasi wake.

Maswahaba wengine wanajiunga na akina Talha na kula kiapo kuwa wangesema ukweli kwamba, Mtume hajafa, kila mtu anajawa na furaha na kama mtunzi anavyosema, wakati wote huo amekuwa shimoni (ubeti 398-400). Ujumbe unapoenea kwamba mtume hajafa, kila mtu anajawa na furaha na kama mtunzi anavyosema, hakuna jema lililoweza kushinda hili.

403. Furaha ikenda mno
Kwao isiyo mfano
Lipi jema lilo pano
La kushinda jambo hili?

Kwa jumla, maswahaba wanaojiunga na Talha ni kumi na watano, akiwemo mwanamke mmoja (ubeti 406). Kula kiapo kwa masahaba kunaendeleza maudhui ya dini ilhali raha inayoenea kote baada ya kufahamu kwamba Mtume hajafa, inaendeleza ushujaa wa Mtume Muhammad kwamba, ni shujaa anayependwa na wengi na kwamba, yeye si wa jamii moja tu, bali waumini wote wa dini ya Kiislamu.

### 3.3.1.6 Abdallah Bin Ubayyi na Wenzake

Abdallah bin Ubayyi ndiye kiongozi wa jeshi la askari mia tatu wanaomtoroka Mtume wakati wa sala kabla ya vita. Ni Mwislamu laghai anayejifanya tu mbele ya Mtume kuwa Uislamu wake ni wa kweli. Huyu kielelezo cha usaliti dhidi ya Mtume na jeshi la Waislamu.

117. Hajesha Sali nabia
Jeshi lilikimbia
La watu thelatha mia
Likamuacha Rasuli

Mtunzi amemtumia Abdallah na kundi lake kuendeleza ushujaa wa Mtume kama shujaa vitani. Hata baada ya kutoroka kwa hao wasaliti mia tatu na Mtume kubaki na wapiganaji mia saba pekee, hajafadhaika wala kufa moyo, bali anaendelea na sala kutayarisha jeshi lake kwa vita dhidi ya Makureshi elfu tatu. Sala ya Mtume na jeshi lake kabla ya vita kunaendeleza maudhui ya dini. Tunafahamu kwamba, hata kabla ya kutoroka kwa wale wanafiki na wasaliti mia tatu, jeshi la mtume lina wapiganaji

wachache sana likilinganishwa na la wapinzani wao. Mtume anaamini uwezo na msaada wa Mungu vitani zaidi ya idadi chache ya wanajeshi wake. Pia, Ubayyi na kundi lake wanawakilisha ukweli kuwa, shujaa husalitiwa na mtu aliye karibu naye. Ubayyi anatoroka na wapiganaji mia tatu na kwenda upande wa Makureshi. Huu ni usaliti.

**3.3.1.7 Ukoo wa Banu Abdi-Dari**

Ni ukoo wa Makureshi mashujaa ambao unapewa mamlaka ya kubeba na kulinda bendera kila vita vinapotokea. Bendera haipaswi kuanguka wakati wa vita, inapoanguka na ikose mtu wa kuinyanyua, ni ishara kuwa vita vimeisha; ishara ya kusalimu amri. (ubeti 224-226). Munsabu bin Omar, ambaye ni swahaba wa Mtume na ambaye ni wa ukoo huu, ndiye anayechaguliwa na Mtume kuwa kiongozi wa jeshi la Waislamu anapokabidhiwa bendera ya Waislamu.

231. Ama kwa hiyo maana
Ndo kufanya Maulana
Kumpa bendera bwana
Isiwe mtu wa mbali

232. Ndo kumpa Mukhtari
Munsabu wa Omari
Ni Bani Abdi-Dari
Hiyo ni yao asili

Omar anapouawa, ndugu yake anachukua usukani na kushikilia bendera, naye pia anauawa. Ndugu wote watatu wa nyumba moja wanauawa wakishikilia bendera ya Uislamu (ubeti 249). Mtoto wa jemedari wa kwanza anaichukua, naye pia anauawa, sawa na wengine wote wanaojitokeza kuiinua (ubeti 253-254).

Wavulana hawa wanaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume na umuhimu wa kuupigania Uislamu. Licha ya kuwa wadogo wa umri, hawaogopi hata baada ya baba zao kuuawa. Baada ya familia ya kwanza kuuawa yote, nyingine ya ukoo huu inajitokeza, nao wanauawa wote (ubeti 255-259). Hili ni dhihirisho la ushujaa wa Mtume kwani wanajitokeza na kupigana kwa kujitoa ili kumtetea kiongozi wao Mtume Muhammad. Mtunzi anaendelea kusema kwamba askari mashujaa wa ukoo wa Bani Abdi-Dari walikataa kukaa licha ya vifo vya wenzao, bali wanapigana hadi mwisho.

258. Ili wao majusuri
Wa Bani Abdi Dari
Roho wakaingia ari
Kukaa wasikubali

259. Nao wakipiganisha
Yakawafuta maisha
Na baada hayo kwisha
Hakusimama rijali

**3.3.1.8 Walenga Mishale Hamsini**

Baada ya Ubayyi kutoroka na wanajeshi mia tatu wakati wa sala kabla ya vita, Mtume anabaki na wapiganaji mia saba pekee. Anachagua walenga mishale hodari kutoka kwa kundi hili na kuwaweka mlimani kushika doria. Anawaonya wasiondoke mahali hapo hadi atakapowaamuru kufanya hivyo au wapate maagizo mengine kutoka kwake.

199. Watu hamsini hao
Kawaweka ili ngao
Wakinge adui zao
Watakapowakabili

207. Tena Tumwa katamka
Akawambia hakika
Wasije wakaondoka
Katika pao pahali

Waislamu wanalishinda nguvu jeshi la Makureshi na kuwafukuza huku wakiokota ngawira (ubeti 278). Walenga mishale wanapoona hivi, wanaamua kuacha mahali pao pa ulinzi na kujiunga na wenzao kuokota ngawira.

288. Wakaiwacha subira
Wakaona kuwa bora
Kwenda kusanya ngawira
Kuliko kulinda jabali

Anayebaki mlimani ni kiongozi wao pamoja na wapiganaji wengine kumi na mmoja pekee (ubeti 299). Wanapoacha jabali na kuwafuata wenzao, Makureshi wanaofukuzwa wanagundua kuwa mlima umebaki bila ulinzi, hivyo walio mbele wanageuka na kikimbia mlimani wakiwaacha wenzao bado wanafukuzwa. Wanapanda mlimani na kuteremkia upande wa vita, hivyo wanalibana jeshi la Waislamu katikati (ubeti 305-309).

309. Ili iwape bahati
Ikihiri tafauti
Wawatie katikati
Ni watu wake Rasuli

Jeshi la Mtume halina ufahamu kuhusu matendo ya Makureshi, wanavamiwa bila kutarajia na wanaumizwa vibaya sana (ubeti 313-317).

313. Hao walitoka hima
Kwa Isilamu kauma
Waliwajia kwa nyuma
Watu wake Murisali

317. Dharuba mahala hapo
Na fazaa zilizopo
Kila mmoja alopo
Hajijui yake hali.

Hili ni kundi la Waislamu ambao hawana subira, wanapenda mali na hawatii wala kufuata amri na maagizo ya Mtume Muhammad. Mtunzi amewatumia kama kielelezo cha usaliti. Anawaagiza wasitoke mlimani lakini wanaghairi amri. Ni kupitia kwao awamu ya pili ya vita inatokea na Waislamu wengi wanachinjwa na Makureshi kwa urahisi bila kutarajia. Tukio hili linaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad kwamba, shujaa husalitiwa na watu walio karibu naye. Anawaamini wapiganaji hamsini hawa na ndio maana anawaweka mlimani kulinda njia zozote ambazo Makureshi wanaweza kupenyezea na kuzunguka jeshi la Waislamu (ubeti 283-284). Wanamsaliti kwa kutotii maagizo na kuacha sehemu zao za ulinzi, jambo linalosababisha kuuawa kwa Waislamu wengi.

329. Kwa vita kusitakimi
Na shitighali adhimu
Kwa wingi wa Isilamu
Walokuwa maktuli

Kutokana na kutotii kwao, Munsabu, anayefanana sana na Mtume anauawa katika awamu ya pili ya vita. Habari zinapoenea kuwa Mtume ameuawa, kundi lingine la Waislamu linatoroka kwa woga na kurudi Madina (ubeti 355-357). Huu pia ni usaliti kwa Mtume Muhammad.

355. Na baadhi yao tena
Walikwenda mbio sana
Hadi huki Medina
Wakwenda wakawasili

Kutotii kwa kundi hili ndiko kunakosababisha kushindwa kwa Waislamu licha ya kuwa na imani imara kwa Mungu. Mwislamu wa kweli anapaswa kuwa mtiifu kwa kiongozi wake katika hali zote ila kumwasi Mwenyezi Mungu.Tukio hili linaendeleza maudhui ya umuhimu na ukuu wa ujumbe wa dini ya Kiislamu na kiongozi wake Mtume Muhammad.

### 3.3.2 Wahusika Binafsi

Hili ni kundi la wahusika wakuu ambao, licha ya kuwa wahusika wakuu, mtunzi anawatumia kumjenga Mtume Muhammed na kuyakuza maudhui.

#### 3.3.2.1 Mtume Muhammad

Ndiye mhusika mkuu katika utenzi huu. Anajitokeza tangu mwanzo hadi mwishoni mwa utenzi. Wahusika wengine, hata wale wakuu, wametumiwa kumkuza yeye. Ni Mtume wa Mungu ambaye, baada ya kumtambua Mungu, mtunzi anamtambua kwa kumpa majina makuu na yenye sifa nzurinzuri kulingana na majukumu anayoyatekeleza maishani mwake. Majina haya ni pamoja na 'kipamba' kumaanisha ni mwenye sura nzuri (ubeti 19), 'Saburi' kumaanisha kuwa Mtume ni mvumilivu (ubeti 20) 'Kipendwa' kuonyesha kuwa anapendwa na wengi (ub 23), 'Nasaha' (ub 24), 'Taji' (ub 25) miongoni mwa mengine.

Katika *Utenzi wa Vita vya Uhud,* mtunzi amemsawiri kama shujaa anayejitokeza tangu mwanzo hadi mwisho na anachukua nafasi kubwa sana kuendeleza maudhui ya dini, ushujaa, vita na mauaji. Kulingana na utenzi wenyewe, Muhammad ana baadhi ya sifa za mashujaa duniani. Ndiye amiri jeshi wa jeshi la waislamu lililo na wapiganaji elfu moja (ubeti 154-156). Kwa hivyo, Muhammad ni shujaa vitani kama walivyo mashujaa wengine. Pia, anapomuua Ubayyi kwa kijambia, Mtume anaonyesha ushujaa wake vitani, kwamba hahitaji zana kubwa za vita. Kijambia chenyewe anakiomba kutoka kwa mmoja wa maswahaba wake.

Kuuawa kwa Ubayy ni kutimia kwa utabiri wa Mtume alipokuwa huko Sarifu (ubeti 492-496). Ubayy anapomlisha farasi wake nje ya mji wa Makka, Mtume anapita karibu naye. Ubayyi anamwonya asitoke nje ya mji tena, la sivyo atamwua. Mtume anamjibu kwamba ndiye atakayemwua akiwa amempanda farasi wake.

498. Pale Tumwa wa I'lahu
Kamwambiaye kabihu
Kampa Inshallahu
Mimi ndo wa kukutuli

Utabiri huu unatimia wakati wa vita Mtume anapomchoma Ubayyi kwa kijambia shingoni akiwa amepanda farasi wake. Anakufa akielekea Makka mahali paitwapo Sarifu.

479. Nae kanipa ahadi
Kunambia Muhammadi
Kuwa atanihusudi
Mimi atanikutuli

484. Shujaa akatilifu
Ni mahala maarufu
Ni mtaa wa Sarifu
Ndipo apotanakali

Shujaa anahusishwa na vitendo vya kimiujiza. Kuuawa kwa Ubayyi kwa kijambia ni muujiza sawa na uchungu anaouhisi ambao mtunzi anasema si wa kawaida.

472. Waama, uchungu wake
Huo mkwaruzo wake
Naona u peke yake
Siuoni mithali

Utuba na Abdillahi bin Shihabi, wapiganaji Makureshi wanamtupia Mtume mawe, wanamuumiza usoni na kumng'oa meno (ubeti 535-540). Tendo hili linamsababishia Mtume uchungu mwingi, damu inamtiririka na anabaki na majeraha mengi mwilini (ubeti 543-545). Mtunzi anaeleza kwamba kovu lililokuwa usoni pake ni ishara na ushahidi kwa ulimwengu kudhihirisha alivyofanyiwa Mtume na Makafiri wa Kikureshi (ubeti 546-548).

546. Hiyo kovu usoni
Haikumwacha Amini
Kwa maana yake kwani
Ili iwe ni dalili

547. Huo ndio ushahidi
Wa mambo yalombidi
Kwa makafiri hasidi
Kumfanyia Rasuli

Ishara hii ya kovu ni dhibitisho la ushujaa wa Mtume katika maisha yake. Pia, hilo kovu usoni pake linaendeleza maudhui ya vita na mateso aliyopitia mikononi mwa Makureshi. Ni dhihirisho kuwa Mtume ni shujaa na maisha ya shujaa ni ya dhiki na mateso matupu. Mtume anapoumizwa, masahaba wake wanamsihi awalaani makafiri

hao wa Kikureshi, lakini anakataa na kusema kuwa Mungu hakumtuma kulaani, bali kutenda mema na kuwasamehe waliokosa.

555. Niletwa kuwaombea
Viumbe maghufuria
Pamwe na rehema pia
Ndo mola kaniwakili.

Anawaombea makafiri waliomtesa wapate watoto ambao watasimamia Uislamu.

559. Naomba siku ya leo
Na ndani ya watu hao
Katika migongo yao
Uwatoe aftali

Mungu anamjibu maombi yake na baadaye Makureshi wanapata watoto wanaosimamia Uislamu. Imam Zuhria ni mjukuu wa mmoja wa wale waliomlenga Mtume kwa jiwe.

568. Maimamu wa Kisuni
Ni mjukuwe yakini
Alompiga usoni
Siku hiyo Murisali

Kupitia kwa maombi na usamehevu wa Muhammad, mtunzi amemtumia kama kiwakilishi cha dini ya Kiislamu. Pia, Mtume vilevile kama tulivyotaja hapo juu, anaendeleza maudhui ya vita vya kidini na mauaji.

#### 3.3.2.2 Munsabu

Ni mhusika msaidizi anayetumiwa kumjenga Mtume Muhammad. Ni shujaa katika jeshi la Kiislamu anayefanana sana na Mtume kimaumbile. Anauawa katika awamu ya pili ya vita ambapo Makureshi wanafurahia sana kwani wanadhani kuwa wamemuua Mtume (ubeti 338-342).

339. Munsabu wa Omari
Shujaa kamhasiri
Na huku yule kafiri
Anadhani Mtume.

Makureshi wanapofahamu kuwa siye Mtume Muhammad waliyemwua, wanaanza vita tena na watu wengi wanauwa.

364. Wakashikana viumbe
Na tena kwa kila pembe
Wakatana kama wembe
Unavyozikata nyweli

Mhusika huyu ametumiwa kuendeleza maudhui ya jinsi hutokea watu wakajitoa mhanga nafsi zao ili kuwanusuru mashujaa wao. Ni kutokana na ukali wa vita ambapo Munsabu anauawa, kisha kifo chake kinasababisha mauaji ya Makureshi wengi sana sawa na Waislamu inapofahamika sio Mtume aliyekufa. Anatumiwa pia kuendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad. Anapouawa, habari zinaenea sana tena kwa haraka kwamba Mtume kafa.

50. Habari ikazagaa
Pasi mahali kusaa
Kama maji na kujaa
Habari ikenda mbali

Kama tunavyofahamu, shujaa hahusishwi na jamii moja. Habari za kifo cha Munsabu, anayedhaniwa kuwa ni Mtume zinaenea kotekote, tena kwa haraka na kumfikia kila mtu. Hili linamaanisha ya kwamba, shujaa akifa kila mtu katika jamii yake hupata kujau habari hiyo.

### 3.3.2.3. Ubayyi Bin Khalifu

Ni mmoja wa viongozi katika jeshi la Makureshi. Ni shujaa, adui na mtesi anayemchukia sana Mtume na dini yake (ubeti 415-417).

416. Ama Mkureshi huyu
Ali adui mkuu
Alikuja yuko juu
Katika wake haili

417. Nae akaja upesi
Ali juu ya farasi
Na yeye ali mtesi
Ali shujaa wa kweli

Anapopata habari kwamba Mtume hajafa, anagadhabika sana na kuapa kwenda kummaliza. Anavaa vazi la kivita na kujifunika mwili wote ila sehemu ndogo eneo la shingoni.

420. Na muwili wake wote
Kureshi kaudhibiti
Hakuusaza popote
Kichwani hata rijali

423. Na huku anabaini
Ali juu farasini
Niacheni niacheni
Na nimuue Rasuli

Mtume anawaagiza masahaba wake wamwache peke yake akakabiliane na Ubayyi. Anaomba kijambia kutoka kwa mmoja wa maswahaba wake na kumchoma nacho shingoni na kumwua. Ubayyi ametumiwa na mtunzi kuendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammed na pia kuthibitisha ule utabiri wa Mtume kuwa angemwua huyo Ubayyi.

Hahitaji zana za hali ya juu kukabiliana na adui, badala yake anaomba kijambia kwa mwenzake anachokitumia kumwua licha ya kuwa amevalia nguo za chuma. Tendo hili linaashiria ushujaa wa Mtume vitani. Mtume anawaomba masahaba wake wamwache peke yaka akabiliane na adui. Hataki msaada wa yeyote. Hili pia ni dhihirisho kwamba, ni shujaa katika vita.

436. Hapa Tumwa kabaini
Kuwaambia jitengeni
Peke yangu niacheni
Sitaki mtu wa pili

Tunaweza pia kusema kuwa kuuawa kwa Ubayyi ni kwa muujiza kwa sababu anapochomwa shingoni, anakimbia kwa jeshi lake akipiga kelele kuwa uchungu anaouhisi si wa kawaida na hauwezi kumithilishwa na chochote duniani.

472. Waama, uchungu wake
Huo mkwaruzo wake
Nao u peke yake
Siuonipo mithali

Anaendelea kusema kwamba uchungu wenyewe ungegawiwa watu wote duniani, wake kwa waume na hata watoto, kila mmoja angepata na ubaki kwa wale walio katika ulimwengu wa pili.

475. Wallahi ingekuwa
Uchungu huu kugawa
Kila mtu akapewa
Ima akali akali

478. Kila mti angepata
Walimwengu wote hata
Na baada ya kupata
Wote wangetanakali

Uchungu unaoelezewa hapa ni wa kimiujiza. Shujaa kwa kawaida anahusishwa na vitendo vya kimiujiza kama vile anavyofanya Muhammad. Ubayyi anaendelea kueleza kuwa Mtume aliahidi awali kuwa angemwua.

479. Nae kanipa ahadi
Kunambia Muhammadi
Kuwa atanihusudi
Mimi atanikutuli

481. Rasuli hasemi kitu
Ila ni kuua watu
Si siku mbili si tatu
Ikampata ajali

Utabiri wa kifo cha ubayyi unatolewa na Mtume anapotembea nje ya mji wa Makka na kumpata Ubayyi akimlisha farasi wake. Ubayyi anamwonya Mtume dhidi ya kutoka nje ya mji, la sivyo angemwua. Lakini mtume anamwambia kwamba ndiye atakayemwua akiwa amempanda huyo huyo farasi wake.

499. Kampa Tumwa Rasua
Ataibudi takua
Mimi ndo wa kukuua
Uli juu ya haili

Utabiri unatimia Mtume anapomchoma Ubayyi kwa kijambia na kumwua. Kwa kawaida, shujaa huwa na uwezo wa kutabiri mambo na yakatimia. Ubayyi, kwa hivyo ni kiwakilishi cha ushujaa wa Mtume Muhammad. Pia, shujaa huwa na wapinzani wengi wanaomchukia. Ubayyi ni mpinzani mkali wa Muhammad amnayemchukia na kutaka kumwua. Kwa hiyo, yeye Ubayyi, ni kiwakilishi cha wapinzani wa Mtume.

424. Nacheni siku ya leo
Niupoze moyo wangu
Na ili mimi na huyo
Tufikiani wawili

Katika ubeti wa 463-466, mtunzi anampa Ubayyi sifa nyingi za ushujaa. Anazitumia kuchimuza ushujaa wa Mtume Muhammed wakati yeye (Mtume) anapomwua Ubayyi. Anasawiriwa kama shujaa aliyeshinda vita vingi, asiye na woga (ubeti 458), asiyekubali kushindwa maishani mwake (ubeti 461), asiyetoroka vita licha ya ukali wake (ubeti 463) na anayevumilia mishale mikali ya maadui (ubeti 464-465). Licha ya ushujaa wake huo, Mtume anamwua kwa kijambia, zana isiyo na umuhimu wowote. Mtume Muhammad kupitia kwa Ubayyi anasawiriwa kama bingwa na shujaa wa vita anayemshinda katili mkuu aliyekuwa hashindwi na mtu wa kawaida. Mtume pia kama shujaa hahitaji usaidizi wa wenzake kupigana na adui. Ubayyi anaendeleza maudhui ya dini, vita na mauaji.

### 3.3.2.4. Utuba na Abdillahi Bin Shihabi

Ni wahusika wasaidizi wanaotumiwa na mtunzi kumkuza Mtume Muhammad na kuendeleza maudhui ya ushujaa, vita na mauaji. Utuba ni kafiri muuaji anayemchukia Mtume. Ni ndugu yake Sadi, ambaye ni jemedari wa jeshi la Mtume. Ni wa ukoo mmoja na Mtume lakini ameasi dini ya Kiislamu. Hana huruma na ndiye anayempiga Mtume kwa mawe na kumng'oa meno.

533. Utuba alisimama
Moyo hauna huruma
Jiwe apolisukuma
Lilimpiga Rasuli

535. Kuja kwakw jiwe lini
Likampasua pano
Na baadhi hayo meno
Likavunja jiwe hili

Mtunzi amemtumia Utuba kuendeleza maudhui ya vita. Pia ni kiwakilishi cha upinzani dhidi ya Mtume Muhammad. Licha ya kuwa ni wa ukoo mmoja na Mtume, anamchukia sana na amejitolea kumwua. Jambo hili linachimuza ushujaa wa Mtume kama shujaa anayepingwa na watu wa jamii yake. Abdullahi bin Shibahi naye anamchukia Mtume na ndiye anamlenga kwa jiwe na kumjeruhi usoni.

537. Ali adui L'lahi
Jinale Abdillahi
Bin Shihabi Kabihi
Adui wa kweli kweli

541. Uso likampasua
Mpasuo ulikuwa
Akaumia Rasuli
Kwa kupigwa jiwe hili

Utuba na Abdullahi ni waasi wa dini ya Kiislamu. Wanaendeleza maudhui ya dini kwa kuonyesha ukatili na uhasama wao dhidi ya Muhammad. Wanaendeleza maudhui ya vita wanapopigana na Mtume na masahaba wake.

### 3.3.2.5 Abu Sufiani na Hindi

Abu Sufiani ni kiongozi wa Makureshi anayemchukia Muhammad na dini yake. Anamkejeli Mtume na wafuasi wake kwamba hawapaswi kuwa hai, na haipo tofauti yoyote kwao wakiwa hai au wafu.

654. Na sauti inanadi
Inasema Muhammadi
Yu hai mbona baridi
Au ametenakali

Wafuasi wa Mtume anaowakejeli ni pamoja na Abu Bakr (Abu Hafsi) na Umari. Sufiani ni kafiri anayemwabudu mungu aitwaye Hubal. Anaendeleza maudhui ya dini kwa kuupinga Uislamu na kuendeleza ukafiri.

671. Ni mkubwa mungu wetu
Ili ya furaha yetu
Leo kutukuka
Ni mungu wetu Hubali

Sufiani pia anaendeleza maudhui ya vita. Anapigana vitani, kisha vita vinapomalizika, anajitokeza na kuwakejeli Waislamu kwa kuwaambia kwamba, amewaletea habari njema kwamba wamgekutana mwaka uliofuata kwa vita vingine. Hii ni baada ya Waislamu kushindwa na wengi wao kuuawa.

680. Na sasa tunakupeni
Habari twakwambieni
Kuwa tunakutakeni
Katika mwaka wa pili

Hindi ni mke wa Sufiani, ni mmoja wa wale wanawake kumi na watano wanaoandamana na waume wao vitani ili kuwapa motisha. Ni mwanamke mwenye ujeuri na majigambo mengi na anampenda mume wake. Ndiye mwanamke wa pekee anayetajwa baada ya vita kati ya wale kumi na watano waliokuwepo mwanzoni mwa vita. Anajitokeza kishujaa juu ya jabali na kuimba wimbo wa kumsifu mume wake. Anapomaliza kuimba ndipo mume wake anapozungumza, kuonyesha nafasi na jukumu kubwa la mwanamke wa enzi hizo vitani na pia katika maisha ya mumewe.

685. Nae huyo nisiwani
Mke wa Abu Sufyani
Akaimba akaghani
Juu ya jabali

686. Baada ya hapo kuimba
Mwanamke kujigamba
Na mumewe akawamba
Abu Sufyani kakuli.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia wahusika na maudhui ya dini, ushujaa, vita na mauaji katika *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Tumewaweka wahusika katika makundi mawili makuu ambayo kuna kundi la wahusika wa makundi na wahusika binafsi. Tumeonyesha majukumu ya makundi haya mawili na jinsi yanavyochangia katika kukuza, kuendeleza maudhui ya utenzi huu wetu na jinsi yalivyojenga dhamira ya mshairi.

Imebainika kuwa wahusika kama viumbe wa msanii au mtunzi ni nyenzo muhimu sana katika kazi yake. Imebainika wazi kuwa wahusika wote hao, wametumiwa kumjenga Mtume Muhammad kama shujaa au nguli sawa na mashujaa wengine ulimwenguni. Makundi hayo mawili zaidi yametumika kuchimuza sifa hizo za Mtume Muhammad kama Mtume wa Mwenyezi Mungu na shujaa wa jamii yake ya Waarabu na Waislamu kwa jumla.

## SURA YA NNE

## VIPENGELE VYA KIMTINDO NA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA VITA VYA UHUD*

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutashughulikia vipengele vya kimtindo na kuonyesha jinsi vinavyoendeleza maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Maudhui tunayoshughulikia ni yale ya ushujaa, dini, vita na mauaji. Tutaangalia tamathali za semi pamoja na mbinu nyinginezo za kimtindo. Kuna tamathali nyingi za semi katika kazi za kifasihi, lakini tutashughulikia chache ambazo tumeziona kuwa za manufaa kwetu na zile ambazo mtunzi amezitumia kuchimuza maudhui tuliyotaja katika utenzi.

### 4.1 Tamathali za Semi

Huu ni ukiushi katika viwango vya kisemantiki au kisintaksia. Huwezesha kupanua maana ya ujumbe unaodhamiriwa kuwasilishwa. Ni mbinu inayotoa maana mpya au pia kutia msisitizo katika jambo fulani. Tamathali za semi anazotumia mtunzi huacha athari fulani kwa msomaji au kwa hadhira lengwa. Tamathali alizozitumia mtunzi katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* zinachimuza maudhui ya dini, ushujaa wa Mtume Muhammad, vita na mauaji. Baadhi ya tamathali za semi zinakaribiana sana kimaana na kimatumizi.

Mohammad (1990) anazieleza kama mbinu mojawapo ya matumizi ya lugha ya mkato na ya kisanii na humwezesha mtunzi kusema mambo mengi kwa maneno machache nay a mvuto. Mbatiah (2001) anasema kuwa tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango mbalimbali vya lugha ili kuleta msisitizo. Wamitila (2003) naye anasema kuwa tamathali za usemi hutumiwa kueleza fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine mpya.

Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kuwa tamathali za semi hutumiwa na mtunzi kuifanya kazi iwe ya kuvutia, iwe na msisitizo fulani na iwe na mnato kwa msomaji. Tamathali za semi ni kama vile taashira, sitiari, tashihisi, balagha, paradoksi (kwelikinzani), kinaya, chuku, tabaini, miongoni mwa zingine. Mtunzi wa *Utenzi wa Vita vya Uhud* ametumia baadhi ya tamathali hizi ili kuchimuza maudhui

anayodhamiria kupitisha kwa hadhira yake. Kama tulivyotangulia kusema, tumechagua baadhi tu ya mbinu hizi ambazo tumeziona kuwa zitatufaa katika mada yetu.

### 4.1.1 Sitiari

Njogu na Chimera (1999), Mbatiah (2001) na Wamitila (2008) wanakubaliana kuwa sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi ambapo vitu viwili vilivyo tofauti kitabia na pia kimaumbile vinalinganishwa kwa njia ya moja kwa moja ili kuleta msisitizo katika maelezo. Sitiari hutumia sifa za kitu kimoja kueleza kingine bila kutumia vilinganishi kama vile 'kama', 'ja', 'mfano wa' na kadhalika. Tunakubaliana na maoni ya wataalamu kwamba sitiari ni tamathali ya usemi ambapo kitu, tabia ya kitu au vitu vyenye tabia inayofanana hulinganishwa kwa njia ya moja kwa moja bila kutumia vilinganishi. Zinaelezea sifa kwa kukipa kitu jina la kitu kingine. Kitenzi 'NI' hututumiwa katika ulinganishi huu.

Katika ubeti wa 155 wa *Utenzi wa Vita vya Uhud,* mtunzi ametumia sitiari kuwarejelea wale askari hamsini Mtume aliowaweka mlimani kushika doria na wale wanajeshi Waislamu elfu moja.

155. Kuitwa kwao wakija
Walifika mara moja
Nao ndo wenye kutajwa
*Ziitwazo panga kali*

201. *Ndizo panga madhubuti*
Na zisizo tofauti
Zinakamishe chochote
Kitakacho kukabili

Wapiganaji anaowachagua Mtume anapoarifiwa kuwa Makureshi wamefika kumshambulia wanaitwa *panga kali,* nao wale hamsini Mtume anaowaweka kushika doria mlimani wanaitwa *panga madhubuti*. Mtunzi anawasawiri kama wapiganaji hatari wasioogopa ndio sababu ya kulinganishwa na panga. Makundi haya yanachimuza ushujaa wa Mtume kama aliye shujaa na hodari vitani kwani ndiye kiongozi wao. Pia yanaendeleza maudhui ya dini kwa kuwa licha ya uchache wao, Mtume ana imani kwamba, wataweza kuwashinda Makureshi walio wengi.

Katika ubeti wa 347, Makureshi wanamwita Muhammad *Shina la Fitina.*

347. Nae kafurahi sana
*Kuwa shina la fitina*
Limekatika hakuna
Mti hauna jivuli

Munsabu anapouawa na kusemekana kuwa ni Mtume aliyeuawa, Makureshi wanafurahi sana. Mtunzi anamfananisha Muhammad na shina la mti wa fitina ambalo limekatwa na mti wenyewe ukakosa kivuli baada ya kukauka. Kulingana na Makureshi, kufa kwa Mtume ambaye ndiye shujaa wa jeshi la Kiislamu kungeliangamiza jeshi hilo, sawa na mti ukatwao na kunyauka. Waislamu wanabaki bila kiongozi wala matumaini. Tamathali hii inachimuza ushujaa wa Mtume katika vita. Kwamba, yeye ndiye shujaa wa Waislamu na kuanguka au kufa kwake kunalifanya jeshi kushindwa kwani kulingana na Makureshi Mtume ndiye chanzo cha matatizo yao kwa sababu ya kutangaza dini mpya iliyopinga na kutishia dini yao ya jadi. Pia inaendeleza maudhui ya dini. Mtume ndiye mwanzilishi wa dini ya Kiislamu na kufa kwake kungeliashiria kufa kwa dini yenyewe, jambo ambalo ndilo lengo kuu la Makureshi waliokuwa makafiri.

### 4.1.2 Tashbihi

Ni tamathali ya kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno kama vile "kama", "mithili ya", "ja", na kadhalika. Mtunzi ametumia tashbihi mbalimbali. Katika ubeti wa 70, mtunzi anawalinganisha Makureshi walioshindwa na kufedheheshwa na Waislamu katika vita vya Badr na ng'onda. Anasema kwamba *Makureshi walirudi kama ng'onda.* Anawafananisha na samaki huyu kuonyesha kuwa Makureshi walikuwa wamekauka na kufedheheka wasiwe na tumaini. Tamathali hii inaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume kwani katika vita vya Badr, Makureshi walishindwa. Shujaa huwa hodari vitani. Inaendeleza pia maudhui ya vita kati ya Waislamu na Makureshi.

Katika ubeti wa 196, tashbihi *wazagaa kama ramli* imetumiwa.

196. Makureshi wamesiri
Na jeshi lao kabiri
Nao ni watu kathiri
*Wazagaa ja ramli.*

Inarejelea wingi wa Makureshi dhidi ya Waislamu walio wachache. Inaashiria ushujaa wa Mtume vitani. Hata baada ya wale mia tatu kutoroka, vita vinaendelea kati ya Waislamu wachache na Makureshi elfu tatu. Kwenye ubeti wa 235, vita kati ya Makureshi na Waislamu vinafananishwa na zilizala. Mtunzi anasema kwamba *walikamatana kama zilizala* kuashiria ukali wa vita. Inachimuza maudhui ya ushujaa wa Mtume kama hodari vitani na pia maudhui ya vita na mauaji kwa sababu katika awamu hii ya vita, watu wengi wanauawa akiwemo mbeba bendera ya Islamu. Mtunzi anafananisha kuanguka kwa kiongozi huyu wa ukoo wa Bani Abdi-Dari na gogo. *Kuangukakwe kama gogo*... ni tamathali inayoendeleza maudhui ya vita na mauaji. Ukali wa vita ndio unaosababisha vifo vya watu hawa wengi.

Katika ubeti wa 276, washika bendera wanapouawa wote na ikachukuliwa na mwanamke ambaye pia anauawa, jeshi la Makureshi linatoroka. Mtunzi anafananisha kutoroka kwao na kule kwa kuku amwonapo mwewe.

276. Wakenda mbio wenyewe
*Ja kuku mwakona mwewe*
Fahamu wasizijue
Na kurukwa na akili

Ni mbinu inayoendeleza maudhui ya woga wa makafiri na kuchimuza ushujaa wa Mtume Muhammad na jeshi la Waislamu. Watu wengi wanakufa katika awamu hii ya vita. Ushujaa wa Mtume pia unajitokeza. Tunafahamu kuwa jeshi la Makureshi lina wapiganaji elfu tatu dhidi ya lile la Waislamu waliokuwa mia sita hamsini baada ya hamsini kuwekwa kulinda eneo la mlimani. Makureshi, licha ya wingi wao wanatoroka vita. Hili linonyesha kuwa Mtume ni shujaa na hodari vitani.

Mtunzi anafananisha wingi wa Makureshi na moshi katika ubeti wa 284. Mtume anawaweka walenga mishale hamsini mlimani kuzuia jeshi la Makureshi elfu tatu lisipite hapo na kuwazunguka. Wanaagizwa kuzuia jeshi la Kureshi *lizungukapo kama moshi*. Kwa kawaida, moshi unapofuka huenea na kuzagaa kotekote. Hii inadhihirisha ushujaa wa Mtume vitani kwa kuwa ana imani kuwa jeshi lake litaweza kuzuia Makureshi elfu tatu. Mtunzi anasema kwamba *watu walianguka kama gogo likatwalo kwa ncha mbili*. Gogo linapokatwa huanguka kwa vishindo, hivyo ndivyo watu walivyoanguka wakati wa vita. Kuanguka kwa askari kunamithilishwa na kule kwa gogo linapokatwa. Mbinu hii inaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Vita ni vikali na

watu wanauana bila kubaguana na kuangukaanguka kila mahali sawa na magogo ya miti.

Mtunzi katika ubeti wa 350, anafananisha kuenea kwa habari za kifo cha Mtume na kusambaa kwa maji ya bahari anaposema: *Habari ikazagaa...kama maji na kujaa.* Kuenea huku kwa habari kunaonyesha umuhimu wa Mtume Muhammad kwa Uislamu, Waislamu na jamii yake pia. Tunafahamu ya kwamba mojawapo ya sifa za shujaa ni kuwa hahusishwi na jamii moja, bali anahusishwa na ulimwengu mzima. Kama shujaa wa Kiislamu, inaposemekana kuwa amekufa, habari zinaenea kotekote na kwa haraka. Maudhui ya vita na mauaji pia yanaenendelezwa na tamathali hii. Kifo cha Mtume kingetokana na ukali wa vita.

Mtunzi katika ubeti wa 365 anasema kuwa wapiganaji *walishikana na kukatana kama wembe unavyozikata nywele*. Wembe kwa kawaida huwa mkali na huzinyoa nywele zilizo laini kwa urahisi. Mtunzi anaashiria kwamba watu waliuana kwa urahisi kutokana na silaha kali walizokuwa nazo na pia ukali wa vita. Maudhui ya vita na mauaji yanachimuzwa. Katika ubeti wa 469, Ubayyi anapochomwa shingoni kwa kijambia, *anapiga kelele kama za kuku anayechinjwa.* Kelele za kuku anapochinjwa huwa nyingi na kali kutokana na woga wa kufa. Ubayyi ni shujaa, lakini anaumizwa kwa kijambia na kupiga kelele za kuogofya ambazo mtunzi anazifananisha na za kuku anayechinjwa. Hii inaendeleza ushujaa wa Mtume kwamba, yeye ni shujaa wa vita na hata anapotumia kifaa duni, anawashinda wengine kama anavyomshinda Ubayyi hata akiwa amevalia nguo za kivita. Ubayyi anapoumizwa kwa kijambia na kutoroka, mtunzi anasema kwamba *anaenda kama mpumbavu.* Kwa kawaida mpumbavu hana mwelekeo na hivyo ndivyo mtunzi anavyomsawiri Ubayyi. Uchungu kutokana na kijambia cha Mtume unamweka katika hali ya kuchanganyikiwa. Kwa hivyo, kitendo cha Mtume ni cha kimiujiza kwa kuwa mkwaruzo wa kijambia ndio unaomwua Ubayyi. Muhammad kama shujaa anatenda kitendo cha kimiujiza.

### 4.1.3 Chuku

Ni tamathali ya usemi inayotumia maneno ya kutia chumvi katika usemi au kauli fulani. Sababu kuu huwa ni kuchekesha au kusisitiza. Ni mbinu ambayo ikitumiwa hukuza sifa ya kitu kuliko hali yake ya kawaida. Mtunzi ametumia mbinu hii katika utenzi ili kuchimuza maudhui mbalimbali. Katika ubeti wa 77, Mtunzi anasema

kwamba Makureshi walijiandaa na zana mbalimbali za vita zikiwemo saifu (panga) *ambazo zingeweza kuvunja jabali.*

77. Wakaziunda saifu
Njema ziso hitilafu
Zipigazo zisihofu
*Zivunje japo jabali*

Istilahi hii inaendeleza maudhui ya vita vikali ambavyo walikuwa wakijitayarishia. Kwa kawaida, panga haiwezi kukata wala kuvunja jiwe.

Kwenye ubeti 474-478, Ubayyi anapochomwa na Mtume kwa kijambia shingoni, anasema kuwa *uchungu aliouhisi hauna mizani, na ungegawiwa watu wote ulimwenguni, kila mmoja, wake kwa waume na hata watoto, angepata na hata wafikiwe walio katika ulimwengu ujao.* Uchungu huo unatiliwa chumvi ili kuonyesha kuwa ni jambo lisilo la kawaida, kuna muujiza unaohusika. Kwa hiyo, mtunzi anatumia chuku kuendeleza ushujaa wa Mtume kama anayetenda miujiza. Mtume anatumia kijambia tu, na Ubayyi, kama shujaa asiyeshindwa, anahisi uchungu usiomithilika.

### 4.1.4 Uhuishaji/Tashihisi

Hii ni mbinu ya kunafsisha au kufanya kitu kiwe na maumbile au tabia ya mwanadamu. Ni kule kukipa uhai kitu kisichokuwa nao, hivyo kukifanya kiwe na sifa za binadamu. Mtunzi katika ubeti 267-268 anasema kwamba *bendera ilikuwa ikimtafuta mtu wa kuiokota ila haikumwona wala haikuona fahari ya kuchukuliwa.* Bendera inapewa sifa za binadamu za kutafuta na kuona. Vita ni vikali na kila mtu anaogopa kuokota na kuinua bendera, hivyo, inabaki chini baada ya waliokuwa na mamlaka ya kuiinua na kuipokezana kuuawa. Maudhui ya vita na mauaji yanachimuzwa na mbinu hii.

### 4.1.5 Maswali ya Balagha

Ni maswali ambayo mtunzi anayatumia ili kumtanabahisha msomaji. Ni maswali yasiyohitaji majibu kwani majibu tayari yapo na yanafahamika. Madhumuni ya maswali haya hasa ni kuwabeza wahusika, kuamsha nadhari ya msomaji ili kumfanya atafakari zaidi. Pia hutumiwa kusisitiza jambo.

Kwenye ubeti wa 203, walenga mishale hamsini wanawekwa mlimani kushika doria. Mtunzi anauliza Makureshi watakapokuja na wapate hawawezi kusonga mbele, *pa kwenda ni wapi mahali?* Mtunzi anaendeleza ushujaa wa Mtume kupitia kwa hamsini hawa. Anawekwa kuzuia Makureshi elfu tatu, ambao ana imani kwamba, hawataweza kupenyeza watakapowapata hapo. Katika ubeti wa 273, mtunzi anauliza swali: *Ili nani asimame kwa jeshi la mwanaume?* Kutokana na ukali wa vita, hakuna mtu hata mmoja anayeweza kujitokeza kuinua bendera baada ya wanaopaswa kuiinua kuuawa. Swali hili linaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Washika bendera wote wa ukoo wa Bani Abdi-Dari wanauawa pamoja na watoto wao. Kwa hivyo, hakuna anayeweza kujitokeza kwa kuogopa ukali wa vita.

Makureshi wanamuuliza Ubayyi maswali mfululizo anaporudi akilia kwa uchungu wa kijambia. *Mara ngapi tumepata kukuona vitani na hujasita? (ubeti 463), Siku ngapi tumebuga hatujakuona mwoga? (ubeti 459), Mingapi kwako mishare, kwako imekuwa bure? (465).* Maswali haya yanaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume kama bingwa vitani na kuudunisha ushujaa wa Ubayyi. Kwa mkwaruzo wa kijambia, Mtume anamua Ubayyi shujaa wa Makureshi. Pia, yanamsawiri Mtume kama shujaa anayetenda miujiza. Ubayyi anasema kuwa uchungu anaouhusi si wa kawaida na hata kama ungegawiwa watu wote duniani na pia walio kwenye ulimwengu ujao, kila mmoja angepata na bado ungebaki.

### 4.1.6 Tabaini

Ni mbinu ya kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yasiyoonyesha msisitizo huo kwa uwazi. Ni mbinu ya kiusemi inayotumia kiungo *SI.* Hutumiwa kueleza msisitizo wa sifa za mhusika au kitu fulani. Mtunzi wa utenzi huu hajaitumia sana mbinu hii. Katika ubeti wa 481, mtunzi anatumia mbinu hii anaposema, *Si siku mbili si siku tatu.*

481. Rasuli hasemi kitu
Ila ni kuua watu
*Si siku mbili si tatu*
Ikampata ajali

Ubayyi anapochomwa shingoni na Mtume, anakiri kwamba Mtume alikuwa amemwambia kuwa angemuua. Anaendelea kusema kuwa Mtume akisema jambo, hazitapita siku nyingi kabla ya jambo hilo kutimia. Ubayyi anakufa kutokana na mkwaruzo wa kijambia cha Mtume. Mbinu hii inachimuza maudhui ya ushujaa wa Mtume kama shujaa wa vita anyetumia kifaa duni kumwua shujaa msifika. Mtume pia

kama shujaa ana uwezo wa kufanya miujiza. Kumwua Ubayyi kwa kijambia ni tendo la kimuujiza. Pia, Mtume kama shujaa anaweza kutabiri mambo na yakatimia.

### 4.1.7 Urudiaji na Takriri

Leech (1969) anasema kuwa urudiaji ni takriri ya neno au kirai bila kuzingatia utaratibu wowote kimpangilio. Haufuati ruwaza yoyote maalum bali hutokea mahali popote katika shairi. Wamitila (2002) anasema kuwa urudiaji hautarajiwi kuwa ule ule bali lazima pawepo na mageuzo katika urudiaji huo ili usilete ukinaifu na uweze kuteka makini ya msomaji na pia kuwasilisha mawazo mepesi kwa msukumo mkubwa. Tunaafikiana na mawazo haya na tunayathibitisha kutoka kwenye utenzi. Katika ubeti wa 533-534, mshororo wa mwisho katika ubeti wa 533 ni *Lilimpiga Rasuli*, nao mshororo wa kwanza wa ubeti wa 534 ni *Likampiga Amini.*

533. Utuba alisimama
Moyo hauna huruma
Jiwe alipolisukuma
*Lilimpiga Rasuli*

534. *Likampiga Amini*
Mdomo wake wa chini
Kwa upande wa yamini
Halikupiga shimali

Mtunzi anarejelea jiwe lililompiga Mtume usoni na kumuumiza vibaya. Urudiaji unaendeleza maudhui ya vita ambapo Mtume aliumizwa na Makureshi. Pia, unachimuza maudhui ya dini. Makureshi, ambao ni makafiri, wanapinga dini ya Uislamu ambayo mwanzilishi wayo ni Muhammad, hivyo wanataka kumwua ili waimalize.

Takriri ni mbinu ya kukariri herufi, neno au maneno fulani kwa minajili ya kusisitiza jambo. Mtunzi ametumia takriri neno. Ubeti wa 544, Ubayyi anapochomwa kwa kijambia, analia akisema: *Mtume kaniua, kaniua, kaniua*. Mtunzi anarudia neno hili ili kusisitiza maumivu aliyo nayo Ubayyi kutokana na mkwaruzi wa kijambia. Inaendeleza maudhui ya vita na ushujaa wa Mtume. Ni kutokana na vita kati yao ambapo Ubayyi ambapo anaumizwa. Pia, inaonyesha ushujaa wa Mtume kwa sababu ametumia kijambia na kusababisha maumivu na hatimaye kifo. Tendo hili ni la kimiujiza. Pia, kwenye ubeti wa 423, Ubayyi anawaambia askari wake wamwache akamwue Mtume. Anasema*: Niacheni niacheni*, na nimuue Rasuli.

#### 4.1.8 Semi/Misemo

Msokile (1993) anaeleza misemo na nahau kama istilahi za kifasihi ambazo huzaliwa, hukua na hufa. Nahau ni misemo iliyojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida na aghalabu huwa imesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno yaliyotumiwa. Mtunzi ametumia misemo kadhaa kwenye utenzi. Katika ubeti wa 81, Makukeshi wanajiandaa kwenda kukabiliana na Mtume. Anaeleza zana za vita walizo nazo. Siku zinapokaribia, ndivyo *roho zinaingia kasi*, kumaanisha kwamba walikuwa na msisimko na taharuki kuhusu vita. Ni msemo unaoendeleza maudhui ya vita. Katika ubeti wa 353, mtunzi anasema kwamba walipopata maneno hayo, *Jamii walikufa nyoyo*. Kufa moyo ni kukata tamaa au kukosa matumaini. Waislamu wanapopata habari kwamba Mtume ameuawa, wanahuzunika sana. Kutokana na haya, kuna kundi linalokosa matumaini kabisa na kukimbia kurudi madina (ubeti 355-356). Msemo huu unaendeleza maudhui ya ushujaa wa Mtume Muhammad. Ndiye tegemeo la wafuasi wake Waislamu na hawawezi kufanya lolote bila uongozi wake.

Misemo *ama faima na potelea pote* imetumiwa katika beti za 602 na 603 mtawalia. Mtume anapoumizwa kwa mawe na Makureshi na kuanguka shimoni, masahaba wake wanaamua kwa vyovyote vile kumpigania na wakajitoa kupigana na Makurishi kufa kupona. Hawajali kufa, muhimu kwao ni kumwaokoa kiongozi wao kutokana na madhara zaidi. Wanawafukuza Makureshi (ubeti 608) mbali na alipokuwa Mtume. Misemo hii inaendeleza maudhui ya vita ambavyo vinatokea baada ya Mtume kuumizwa. Pia, inaendeleza ushujaa wa mtume, yeye ni shujaa anayelindwa na wafuasi wake kutokana na hatari yeyote kama ilivyo na mashujaa wengine duniani.

#### 4.1.9 Ukiushi wa Kisintaksia

Ukiushi ni uvunjaji kimakusudi wa kaida za matumizi ya lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza na kusababisha athari fulani ya kiujumi pamoja na kukoleza maana. Ukiushi wa kisintaksia unahusu kubadilisha mpangilio wa kawaida wa maneno katika vishazi vya sentensi. Mtunzi katika utungo tunaoushughulikia ametumia mbinu hii ili kuchimuza ujumbe anaodhamiria kuwasilisha kwa msomaji. Mbinu hii inajitokeza katika beti kadhaa.

97. Na tena ikawa kimya
*Pasi neno kusema*
Jumla mwaka mzima
Kureshi wakija hali

Baada ya vita vya Badr, Makureshi wanajitayarisha kwa vita vya kulipiza kisasi dhidi ya Waislamu waliowashinda kwa mwaka mmoja. Jeshi lao ni kubwa sana lililo na wapiganaji elfu tatu. Hata hivyo, wanajitayarisha kwa siri ili Mtume asije akapata ufahamu kwamba wangemvamia kwani wanafahamu kuwa yeye ni bingwa vitani. Mtunzi anasema kuwa walijitayarisha *pasi neno kusema* badala ya pasi kusema neno. Amekiuka kanuni ya mpangilio wa sentensi ambapo kitenzi kwa kawaida hufuatwa na nomino. Uzito umetiwa kwenye nomino 'neno' ambayo haipaswi kutangulia kitenzi. Kwa kufanya hivi, mtunzi anaonyesha ya kwamba kwa kipindi cha mwaka mzima, hakuna aliyepaswa kutoa taarifa yoyote kwa Mtume kuhusu kujitayarisha kwao kwa ajili ya vita. Kwa kuwa Mtume ni shujaa na mashujaa huwa hodari vitani, Makureshi wanajua kwamba Mtume akijua atatayarisha jeshi lake na bila shaka angewashinda.

Kwenye ubeti wa 101, mtunzi anasema *ili wengi Makureshi* badala ya *ili Makureshi wengi.*

Anatanguliza usemi kwa kielezi 'wengi' ili kusisitiza ya kwamba jeshi la Makureshi lina wapiganaji wengi (Elfu tatu) wakilinganishwa na Waislamu walio mia saba tu. Uzito wa usemi unawekwa mwanzoni mwa sentensi ili kuchimuza ushujaa wa Mtume. Mbinu hii pia imetumiwa katika sehemu nyingi kwenye utenzi ili kuchimuza maudhui ya vita, ushujaa wa mtume na dini na mauaji. Mifano *Hamu na chao kishindo* (ubeti 100), *Farasi limechukua* (ubeti136), *Makureshi kufukuza,* (ubeti 281), miongoni mwa nyingine.

### 4.2. Dayolojia

Haya ni mazungumzo baina ya wahusika. Mazungumzo ya aina hii ni mengi katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Ubayyi anapofahamu kwamba, aliyeuawa alikuwa Munsabu wala si Mtume Muhammad, anaghadhabika sana, anavaa kivita na kuondoka kwenda kukabiliana ana kwa ana na Mtume. Anaapa kwa sauti kwamba jambo litakaloutuliza moyo wake ni kummaliza Mtume.

423. Na huku anabaini
Ali juu ya farasi
*Niacheni niacheni*
*Na nimuue Rasuli*

424. Niacheni siku ya leo
Niupoze wangu moyo
Na ili mimi na huyo
Tufikiane wawili.

Matamshi yake yanaendeleza ushujaa wake. Tumemtaja Muhammad kama shujaa wa vita, lakini Ubayyi ana ujasiri wa kukabiliana naye akiwa peke yake. Hivyo, Ubayyi ni shujaa wa Makureshi mwenye moyo wa ushujaa, asiyeogopa na aliye tayari kumwangamiza shujaa wa jeshi la Kiislamu.

Maswahaba wa Mtume wanaposikia Ubayyi akimwita Mtume wapigane, wanafadhaika na kuanza kumzuia Mtume asiende vitani asije akafikwa na hatari yoyote. Mtume hata hivyo anavalia kivita, akaomba kijambia kutoka kwa mmoja wa maswahaba wake (ubeti 429-430) na kuwaamuru wamwache akapigane peke yake wala asifuatwe na yeyote (ubeti 435-437). Matamshi haya yanaonyesha ushujaa wa Mtume. Japo ana maswahaba wanaomlinda, anataka aachwe akapigane peke yake. Mwishowe anamchoma Ubayyi shingoni na akafa baadaye akielekea Madina. Hili linaonyesha kuwa shujaa hahitaji msaada, bali anajiweza.

Ubayyi bin Khalif ni Kureshi anayemchukia Mtume sana. Mtume anapomchoma shingoni, anatoroka akilia kwa sauti.

454. Kureshi akitongoa
Muhammadi kaniua
Kaniua kaniua
Emekwisha nikutuli

455. Waama kimeniua
Kijambia cha Rasua
Na huku anaongoa
Alipochomwa mahali

Matamshi haya pia yanachimuza ushujaa wa Mtume kwamba ni shujaa vitani anayeweza kumuumiza mtu kwa ala duni. Pia kuna tendo la kimuujiza. Pia kuna tendo la kimiujiza linalojitokeza. Ubayyi anaporudi kwa Makureshi wenzake, wanamkejeli kwamba analizwa tu na mkwaruzo wa kijambia cha Mtume ilhali kwa muda wote wamemfahamu kama shujaa (ubeti 460-461). Matamshi haya yanachimuza ushujaa wa Mtume na kudunisha ule wa Ubayyi. Japo ni shujaa wao ambaye hajawahi kushindwa, anaumizwa na hatimaye kuuliwa kwa kifaa duni na wanamwambia kuwa anawaonyesha ujinga (ubeti 459). Hivyo, Muhammad ni bingwa na ameshinda kafiri katili mkuu wa Makureshi bila kutumia nguvu.

Ubayyi anamwambia Mtume asitoke nje ya mji wa Makka na akifanya hivyo atamwua (ubeti 494-497). Matamshi ya Ubayyi yanaashiria chuki na uadui dhidi ya Mtume. Hili ni dhihirisho la ushujaa wa Mtume kwamba, shujaa huwa na maadui na wapinzani. Kwa kumjibu Ubayyi, Mtume anamwambia kuwa ndiye atakayemwua akuwa amempanda farasi (ubeti 498-499). Utabiri huu ulikuja kutimia wakati Muhammad anapomchoma Ubayyi kwa kijambia akiwa amepanda farasi (ubeti 501). Dhihirisho kuwa Muhammad ni shujaa aliye na uwezo wa kutabiri mambo na yakatimia. Pia inaendeleza maudhui ya dini katika utenzi.

Muhammad anapoumizwa sana kwa jiwe, masahaba wake wanamtaka awalaani waliomtendea kitendo hicho, lakini anawajibu kwa kusema kuwa Mungu hakumtuma duniani kulaani, bali kutenda mema (553-555). Matamshi ya Mtume yanaendeleza maudhui ya dini, kwamba, katika dini yake, Allah anawataka watu wawatendee wengine mema badala ya kulipiza kisasi. Kutokana na haya, Mungu anamshushia Mtume aya za Kurani kuhusu kutolipiza kisasi. Aya hizi ndizo zilizowekwa pamoja baadaye na kuwa Kurani, kitabu kitakatifu cha dini ya Kiislamu. Mtume pia ni kielelezo cha maadili na uadilifu katika dini ya Kiislamu. Sala ya Mtume (ubeti 557-562) inachimuza maudhui ya dini kwenye utenzi mzima. Mara anapomaliza sala, Mungu anamjibu.

563. Mtema kasha jawabu
Kuomba alo Habibu
Assami ul Mujibu
Dua akaikubali

564. Palepale ye wasia
Akaikubali dua
Hii ya Tumwa shafia
Tena Rabi akajaali.

**4.3 Taswira**

Taswira ni dhana inayotumiwa kueleza neno, kirai au maelezo ambayo huunda picha fulani akilini mwa msomaji. Picha hii huundwa na maelezo fulani anayoyasoma msomaji. Hivyo, tunaweza kusema kuwa taswira ni maelezo yanayojenga picha ya hali au jambo akilini mwa msomaji au pia msikilizaji. Utenzi huu unahusu vita, hivyo umetanda taswira nyingi inayoendeleza maudhui hasa ya vita na mauaji. Katika ubeti wa 104-105, mtunzi anaeleza jinsi wapiganaji elfu moja wa jeshi la Kiislamu wanavyovalia kivita kwa haraka baada ya kupata habari kwamba, jeshi la Makureshi lilikuwa limefika tayari kuwashambulia. Walivalia nguo za chuma, kanzu na masuruali. Taswira hii inaibua maudhui ya vita.

Kwenye ubeti wa 245-268, mtunzi anaeleza kuhusu wale wabeba bendera wa ukoo wa Banu Abdi-Dari. Anaeleza jinsi ndugu watatu wa familia moja wanavyouawa kwa muda mfupi sana huku wakianguka kama magogo. Anaendelea kueleza jinsi bendera ya Uislamu inavyoanguka na kuachwa ikipepesa ardhini kwa kukosa mtu wa kuichukua hata baada ya wale wavulana watatu kuuawa (uk 250-254) na pia kuuawa kwa yule mwanamke aliyekuwa amejitolea kuiinua (ubeti 269-272). Watu wote wanaogopa ukali wa vita na kukimbia kutoka medani ya vita. Taswira hii inaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Pia, inaendeleza ushujaa wa ukoo wa Banu Abdi-Dari ambao, hata baada ya familia mbili kuuawa zote, panatokea mwanamke anayeinua bendera ambaye baada ya kuuawa, wavulana wanne wachanga wanajitokeza. Huu ni ukoo wa mashujaa wasioogopa vita licha ya ukali wake.

Mtunzi katika ubeti wa 332-335 anaeleza jinsi wapiganaji wanavyopigana bila yeyote kumjali mwenzake. Anaeleza vile watu walikatana bila kujali na kuanguka kama magogo ya miti iliyokatwa kwa panga kali. Taswira hii inaendeleza maudhui ya ukali wa vita na mauaji.

334. Tena pakawa chavugo
Kwa wingi wa tirivyogo
Watu kwanguka ja gogo
Likatwalo ncha mbili.

Mashahidi wamekatakatwa kinyama kama anavyoelezea mtunzi katika ubeti wa 332-335. Mikono, miguu na vichwa vyao vimetapakaa mbali na viwiliwili vyao. Hii ni taswira inayoendeleza maudhui ya vita na mauaji na kuonyesha unyama wa makafiri Makureshi. Hamzah ami yake Mtume Muhammad, naye pia amekatwakatwa kinyama kiasi cha kwamba, hakuna maneno yanayoweza kueleza hali ya mwili wake uliokuwa vipandevipande (ubeti 702-703). Taswira hii pia inaendeleza maudhui ya vita na mauaji. Baada ya vita, Hindi, mkewe Sufiani, anasimama juu ya jabali na kuimba nyimbo za kumsifu mumewe kwa kejeli na majivuno mengi. Ni taswira inayoendeleza maudhui ya ushujaa wa Sufiani, ujahili wao na jinsi jeshi zima la Makureshi lilivyosherehekea ushindi wao (ubeti 684-686).

### 4.4 Hitimisho

Kwenye sura hii, tumeshughulikia jinsi baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyoendeleza maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Vipengele tulivyoshughulikia ni pamoja na taswira, dayolojia na tamathali za semi. Tamathali tulizoziangazia ni sitiari, tashbihi, chuku, uhuishaji, maswali balagha na tabaini. Mbinu nyingine za kimtindo ni urudiaji, takriri, semi na ukiushi wa kisintaksia. Vipengele hivi vimechimuza maudhui ya ushujaa, vita na mauaji kama tulivyoeleza hapo juu na kwingineko.

# SURA YA TANO
# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia matokeo ya utafiti wetu ili kudhihirisha kuwa tumejikita katika malengo yetu ya utafiti. Tumetoa muhtasari wa mambo tuliyoyashughulikia katika utafiti wetu na hatimaye, tukatoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusu *Utenzi wa Vita vya Uhud* na tungo za zamani za Kiswahili.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kuchunguza jinsi mtunzi wa *Utenzi la Vita vya Uhud* alivyotumia vipengele vya kimtindo kuwasilisha maudhui na kujenga dhamira zake kwa msomaji au hadhira yake. Katika sura ya kwanza, tumetaja vipengele vya utafiti huu ambapo tumeangazia maswala ya kimsingi ya utafiti ambayo ni mada ya utafiti, tatizo la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete, malengo/madhumuni ya utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mwisho, tukaeleza njia tutakazotumia katika utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tumeangazia maudhui yanayojitokeza katika utenzi yakiwa ni pamoja na yale ya ushujaa, dini, vita na mauaji. Japo kuna mashujaa wengine wengi katika utenzi huu, tumetilia uzito zaidi ushujaa wa Mtume Muhammad kwa sababu ni shujaa wa dini ya Kiislamu na mtunzi amemkuza kama shujaa wa kipekee akilinganishwa na wengine waliojitokeza katika utenzi. Mtume kama shujaa ana sifa nyingi ambazo mashujaa wengine wa kijamii ulimwenguni wanazo. Utenzi wote kwa jumla unazungumzia vita vya kidini kati ya Waislamu na Makureshi ambao ni makafiri wanaopinga dini ya Muhammad ambayo ni ya Kiislamu. Kwa hivyo, maudhui ya dini, ushujaa, vita na mauaji yamechukua nafasi kubwa katika utenzi huu na tumeyashughulikia kiasi tulichoweza.

Katika sura ya tatu, tumeangazia dhana ya wahusika kama mojawapo wa mbinu za kimtindo na jinsi mtunzi alivyowatumia kuendeleza maudhui. Wahusika wamegawanywa katika makundi ya kibinafsi na kimakundi, wakuu na wasaidizi na aina za mviringo au duara, bapa na shinda au mafoili. Katika kila kundi, la Waislamu na Makureshi, mtunzi amewahusisha wahusika wengi kwa hivyo, tumewaweka baadhi yao katika makundi na wengine tukawashughulikia kibinafsi. Mtunzi

amefanikiwa kuwatumia wahusika hawa kuibua maudhui ya ushujaa, dini, vita na mauaji kikamilifu.

Katika sura ya nne, tumeangazia jinsi mtunzi alivyotumia vipengele zaidi vya kimtindo kuendeleza maudhui ya dini, ushujaa, vita na mauaji. Tumeshughulikia dayolojia, taswira na tamathali za semi. Tamathali za semi tulizoshughulikia ni pamoja na sitiari, tashbihi, chuku, uhuishaji na tabaini. Mbinu nyingine ni maswali ya balagha, urudiaji, takriri, na ukiushi wa kisintaksia. Pia tumeshughulikia semi. Mtunzi amezitumia mbinu hizi kikamilifu kuchimuza maudhui na kuupa utungo ladha na ujumi kama kazi ya kifasihi.

Kutokana na uchunguzi wetu wa *Utenzi wa Vita vya Uhud*, tumegundua ya kwamba, mtunzi ametumia vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo vimemwezesha kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Imedhihirika wazi kwamba, vipengele vya kimtindo na maudhui ni dhana mbili ambazo hazipaswi kutenganishwa kwani zinajengana, kuendelezana na kukamilishana.

Kuhusu wahusika, tumegundua kuwa mtunzi amewatumia kikamilifu kuuwasilisha ujumbe wake vilivyo kama tulivyodhihirisha. Kwa upande wa mbinu za utunzi, mwandishi ameonyesha umahiri wake wa kutumia mbinu za kimtindo ambazo, licha ya kwamba zinaifanya kazi ivutie, amezitumia kuchimuza maudhui ya utungo wenyewe.

## 5.2 Changamoto

Tumekumbana na changamoto mbalimbali katika utafiti huu. Kwanza, muda tuliokuwa nao haukutosha. Pili, kazi hii ilihitaji kuchapishwa kila baada ya kufanyiwa marekebisho ili kuiboresha zaidi, hivyo, tulikumbwa na tatizo la kifedha. Kazi nyingi zilizopo hasa kuhusiana na mada yetu zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwa hiyo tulijitahidi kuzisoma, kuzielewa ndipo tutie maoni yaliyotufaa katika kazi yetu. Hata hivyo, tulijaribu kadri ya uwezo wetu kuifanikisha kazi yetu kwa wakati uliostahili.

### 5.3 Mapendekezo

Utafiti wetu umejikita katika uchunguzi wa mtindo na maudhui katika *Utenzi wa Vita vya Uhud* tukitumia nadharia za Umuundo na Uhalisia. Hii ni sehemu ndogo tu kuhusu utenzi huu. Kuna haja ya kuufanyia utungo huu uhakiki wa kina zaidi wa kifani. Pia, kuna haja ya kuufanyia utafiti zaidi kuhusu maudhui.

Kwa maoni yetu, mambo haya ni muhimu sana lakini hatungeweza kuyashughulikia yote kwani kwa kufanya hivyo, tungekuwa tumekiuka upeo na mipaka ya kazi yetu. Iwapo utafiti wa aina hii utafanywa, basi utakuwa wa manufaa sana kwa wasomi wa siku za halafu na utawafaidi pakubwa. Ni utafiti ambao pia utauboresha mtalaa wa fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M.H. (1968). 'A note on the Language of the Poem', katika Lienhardt, P. (Mhariri) *The Medicineman*. Clarendon: Oxford University Press.

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Allen, J. W. T. (1971). *Tendi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Amata, K. na King'ei, K. (2001). *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Armstrong, K. (2007). *Muhammad, Prophet of Our Time*. Great Britain: Clays Ltd, St Ives Plc.

Chum, H. (1962). *Utenzi wa Vita vya Uhud.* Dar-es Salaam: East African Literature Bureau.

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Gaster, T.H. (1987). 'Heroes'. Eliade, M. (Mhariri), The Encyclopeadia of Religion. New York: Mackmillan Publishers.

Gatakaa, G. (2012). 'Uhakiki wa Maudhui Teule Katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*'. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

George, F. N. (2003). *Islam at War*: *A history*. Westport: Connecticut/ London.

Gichamba, J. (2005) 'Sifa za Mashujaa na Umuhimu Wao Katika Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford: Oxford University Press.

International Bible Society. (1978). *The Holy Bible*. *New International Version*. Colorado Springs: Colorado.

Kadenge, K. (1982) 'Deviation and Foregrounding in chosen Swahili Texts'. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry. An Investigation into the Concept of East African Islam as Reflected in the Utenzi Literature*. Leiden: E.J. Brill.

_____________. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse. A Literary History and Anthology*. London: Darf Publishers.

_____________. (1983). *Epic poetry in Swahili and Other African Languages*. Leiden: E.J. Brill.

Lambert, H. E. (1959). (Mha.). *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.

Lienhardt, P. (1968). *The Medicineman*. Clarendon: Oxford University Press.

Lugwiri, P. O. (2011). 'Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Maina, V. (2005). 'Nafasi ya mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Margoliouth, D. S. (2003). *Mohammed and the Rise of Islam*. New York: G. P Tutnams.

Massamba, D. P. B. M. (1983). *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili, Toleo la 3*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books.

Mishra, K. (2011). 'A study of form and content'. *Journal of English and Literature*. India: I.S.S.N Publishers.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mubarak, A. A. H. A. (1971). *Kurani Tukufu Pamoja na tafsiri na maelezo kwa Kiswahili.* Lahore: Pakistan Printing works.

Mohamed S. A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi.* Nairobi: Evans Brothers Limited.

__________ (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: East African Educational Books.

Mukuthuria, M. (2007). 'Upekee wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali'. Nordic Journal of African studies Vol. 16(3) 298-319.*

Mulokozi, M. (1999). *Tenzi tatu za kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Mungai, P. (2005). 'Ulinganishi wa kifani wa Tenzi za *Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa*'. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Murumba, J. B. (2011). 'Mtindo katika *Watu wa Gehena'*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Murungi, G. K. (2011). 'Mtindo unavyoendeleza Maudhui katika *Natala'*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Muthoni, M. (2014). 'Uhakiki wa Maudhui na Mtindo Katika *Tikitimaji'*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu K, na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omwayo, O. (1997). 'Fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa *Upisho wa Malenga* na *Dafina ya Umalenga.'* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Senkoro F. E. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Swaleh, A. (1992). Maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Syed, A. (1922). *The Spirit of Islam. A history of the Evolution and Ideals of Islam with a Life of the Prophet*. London: Mutheuen & Co Ltd.

Tola, K. (2009). Uhakiki wa fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wa Mberia, K. (1989). "Fumo Liyongo", Katika *Mulika, No. 21*. Dar es Salaam: TUKI. Uk 25-43.

Wa Mutiso, K. (1985). Hurafa na Uyakinifu katika *Hamziyyah*. Tasnifu ya shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

_____________. (1996). "Archaetypal Motifs Swahili Islamic Poetry: *Kasida ya Burudai*" Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

_____________. (1999). *'Sira ya Majagina: Buddha na Muhammad'*. Wasilisho katika Kongamano la Kiswahili. University of Bayreuth, Germany.

_____________. (2005). *Utenzi wa Hamziyyah.* Dar es Salaam: Insitute of Kiswahili Research. University of Dar as Salaam.

Wamitila K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Focus Publishers.

_____________. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

_____________. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

_____________. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi I.* Nairobi: Vide-Muwa Ltd.

Wesah, E. (2005). 'Uhakiki wa kifani katika *Utenzi wa Mwana Fatuma'*. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).